# FANI KATIKA MAULIDI YA NUNI

**NA**

**SOUD ZAHRA**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A) KISWAHILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**IDARA YA KISWAHILI**

**OKTOBA 2016**

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote

__________________________ __________________________

SOUD ZAHRA TAREHE

NAMBARI YA USAJILI C50/67141/2013

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii wa Chuo Kikuu cha Nairobi.

Profesa Kineene Wa Mutiso Tarehe

(Msimamizi)

Profesa Rayya Timammy Tarehe

(Msimamizi)

# TABARUKU

Kazi hii nawatabarukia babangu Mohamed Soud, mamangu Fatuma Abdalla, mume wangu Bakari Khamis, wanangu: Aisha, Fatma, Sumeiya, na Munira pamoja na kakangu Ahmed Soud na mjombangu Hemed Mohamed  Khamis. Mwenyezi Mungu awahifadhi.

# SHUKRANI

Shukrani zangu kwanza ni kwa Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kukamilisha kazi hii. Vilevile nawashukuru wasimamizi wangu Profesa Kineene wa Mutiso pamoja na Profesa Rayya Timammy kwa kunipa mwongozo thabiti na motisha kukamilisha kazi hii. Mwenyezi Mungu awajaze heri. Nitakuwa mtovu wa shukrani ikiwa sitawashukuru wafuatao kwa mchango wao mkubwa katika kazi hii ambao ni: Sheikh Abdulrahman Suleiman, Amina Twaha, Hamud Mbarak na Virginia Gaithuma. Mwenyezi Mungu awajaze heri.

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| A.S | Aleihi salam/ amani iwe juu yao |
| K.M | Kwa mfano |
| K.V | Kama vile |
| M.M | Mwenyezi Mungu |
| N.K | Na kadhalika |
| S.A.W | Salallahu aleihi wasalam/ rehma na amani zimshukie Mtume Muhammad (S.A.W) |
| S.W.T | Subhana Wataala/ Jina la Mwenyezi Mungu aliye mmoja. |
| R.A.A | Radhi Allahu anhu /anha/ radhi za Mwenyezi Mungu ziwafikie wanaume na wanawake wema waliotangulia mbele za haki ambao ni maswahaba wa Mtume (S.A.W). |

# IKSIRI

Somo letu la utafiti limekuwa fani katika *Maulidi ya Nuni*. Malengo yetu ya utafiti yalikuwa ni kuchunguza nafasi ya wahusika na uhusika katika *Maulidi ya Nuni* na vilevile kuchanganua matumizi ya lugha, tamathali za usemi, muundo na mandhari katika *Maulidi ya Nuni.* Tumetumia nadharia ya mtindo ambayo ni mwafaka katika utafiti wetu. Tumeweza kuchunguza nafasi ya wahusika na uhusika kwa kutumia mbinu ya usimulizi ambapo mhusika amesawiriwa kupitia usimulizi, wasifu wake, msukumo wa matendo yake, tabia na amali zake. Katika matumizi ya lugha tumechunguza lahaja ya Kiamu, Kingozi na lugha ya Kiarabu. Katika tamathali za usemi tumechunguza ukiushi ambapo kifungu fulani hutumiwa kwa maana ambayo ni tofauti na maana ya kimsingi. Kutokana na hali hii, tumechunguza matumizi ya takriri, tashbihi, istiari, tashihisi pamoja na chuku. Vilevile tumechunguza matumizi ya taswira au jazanda na tumeona kuna picha zinazojitokeza ambazo zimefafanua tukio au hali fulani ya mhusika. Katika muundo, tumerejelea umbo na mpatano, mshikamano na uhusiano wa visehemu tofauti vya kazi hii ambavyo huleta sifa zinazotenganisha na kutambulisha mtunzi. Vilevile tumechunguza uhuru wa kishairi kwa kushughulikia inkisari, mazida pamoja na tabdila. Wahusika wameweza kuwekwa wazi kwa njia ambayo inadhihirika sana na mandhari. Utafiti huu ni wa kifasihi na umejikita katika fasihi andishi, kwa hivyo tumefanya kazi nyingi maktabani kwa kusoma kwa kina *Maulidi ya Nuni* yenye beti 130. Pia tumesoma kazi mbalimbali zilizogusia vipengele vya fani tulivyovishughulikia kama vile tasnifu mbalimbali, makamusi, vitabu vya ushairi na miswada mbalimbali. Tumeweza kusoma vitabu mbalimbali vya dini vikiwemo Qur’an Tukufu na vitabu vyengine vya dini vilivyotusaidia. Tumewajumuisha walimu wa madrasa wakiwemo mashehe ambao walitupa mwongozo na mawazo. Tumepitia mtandaoni ili kupata yaliyofanywa kuhusu mada yetu ya utafiti. Matokeo ya utafiti huu yameonyesha kuwa kuna wahusika aina mbalimbali waliojitokeza katika kazi hii na wamejitokeza kama wahusika wa kawaida, wasiokuwa wa kawaida, wahusika wakuu, wahusika wasaidizi na pia wahusika wadogo kulingana na sifa zao. Katika matumizi ya lugha, tumebaini matumizi ya lahaja ya Kiamu, Kingozi na pia maneno ya Kiarabu. Kwa upande wa tamathali za usemi tumebaini matumizi ya takriri, tashbihi au tashbiha, istiari, uhuishaji au tashihisi, pamoja na chuku. Pia tumebaini matumizi ya taswira au jazanda. Katika muundo tumebaini umbo na mtindo wa utungo huu na pia uhuru wa kishairi  kutokana na matumizi ya inkisari, mazida na tabdila. Katika mandhari au mahali tumebaini mandhari ya kijiografia, mandhari yasiyo halisi, mandhari ya kiishara, mandhari ya Uarabuni na pia mandhari ya kimapatano.Utafiti wetu umejikita kwenye fani katika *Maulidi ya Nuni*. Tunapendekeza kuwa watafiti wa baadaye washughulikie kipengele cha maudhui ambacho hatukukigusa. Vilevile tumetumia nadharia ya mtindo katika kushughulikia kazi hii. Tunapendekeza watafiti wa baadaye watumie nadharia tofauti na yetu katika kuchunguza utungo huu au tungo zengine.

**YALIYOMO**

**UNGAMO** ..... ii

**TABARUKU** ..... iii

**SHUKRANI** ..... iv

**ORODHA YA VIFUPISHO** ..... v

**IKSIRI** ..... vi

**SURA YA KWANZA** ..... 1

1.1 Utangulizi ..... 1

1.2 Tatizo la Utafiti ..... 5

1.3 Malengo ya Utafiti ..... 6

1.4 Maswali ya Utafiti ..... 6

1.5 Sababu za Kuchagua Mada ..... 6

1.6 Upeo na Mipaka ..... 7

1.7 Msingi wa Nadharia ..... 8

1.8 Yaliyoandikwa Kuhusu Somo la Utafiti ..... 10

1.9 Njia za Utafiti ..... 13

1.10 Hitimisho ..... 13

**SURA YA PILI** ..... 15

2.1 Misingi ya Uhakiki wa Fani ..... 15

2.2 Utangulizi ..... 15

2.3 Maulidi ya Nuni ..... 15

2.4 Wahusika na Uhusika ..... 17

2.5 Matumizi ya Lugha ..... 19

2.5.1Lahaja ya Kiamu ..... 20

2.5.2 Kingozi ..... 21

2.53 Lugha ya Kiarabu ..... 21

2.6 Tamathali za Usemi ..... 21

2.6.1 Takriri ........ 21
2.6.2 Tashbihi au Tashbiha ........ 22
2.6.3 Istiari ........ 22
2.6.4 Tashihisi ........ 22
2.6.5 Chuku ........ 22
2.6.6 Taswira au Jazanda ........ 22
2.8 Muundo ........ 24
2.9 Umbo la Utungo ........ 24
2.10 Mandhari au Mahali ........ 24
2.11 Hitimisho ........ 25
**SURA YA TATU ........ 26**
3.1 Nafasi ya Wahusika na Uhusika Katika Maulidi ya Nuni ........ 26
3.2 Utangulizi ........ 26
3.3 Mwenyezi Mungu ........ 26
3.4 Mtume Muhammad (S.A.W.) ........ 30
3.5 Jibril ........ 35
3.6 Munkar ........ 36
3.7 Malaika Wengine ........ 37
3.8 Wanawake kwa Jumla ........ 38
3.8.1 Amina ........ 38
3.8.2 Thuweiba ........ 39
3.8.3 Halima ........ 39
3.8.4 Mariyamu Binti Imrani ........ 40
3.8.5 Mwana Asiya ........ 41
3.8.6 Khadija ........ 42
3.8.7 Maisara ........ 43
3.8.8 Maria Kibtiya ........ 43

3.9.9 Wanawake Wema ........ 43
3.10 Wanaume kwa Jumla ........ 44
3.10.1 Abdalla ........ 44
3.10.2 Abdulmuttalib ........ 44
3.10.3 Abutalib ........ 44
3.10.4 Mjombake Thuweiba ........ 45
3.10.5 Abubakar ........ 45
3.11 Mitume ........ 46
3.12 Watoto wa Mtume Muhammad (S.A.W) ........ 47
3.13mahurulaini ........ 49
3.14 Maswahaba ........ 49
3.15 Muhajirun na Ansar ........ 50
3.16 Wanyama, Miti ya Mitende na Majabali ........ 51
3.17 Wahusika Wengine ........ 52
3.18 Hitimisho ........ 54
**SURA YA NNE ........ 55**
4.1 Matumizi ya Lugha, Tamathali za Usemi, Taswira au Jazanda, Uhuru Wa Mtunzi, Muundo na Mandhari katika Maulidi ya Nuni. ........ 55
4.2 Utangulizi ........ 55
4.3 Matumizi ya Lugha ........ 55
4.3.1 Lahaja ya Kiamu ........ 55
4.3.2 Kingozi ........ 56
4.3.3 Maneno ya Kiarabu ........ 57
4.4 Tamathali za Usemi ........ 60
4.4.1 Takriri ........ 60
4.4.2 Tashbihi/Tashbiha ........ 62
4.4.3 Istiari ........ 64

4.4.4 Uhuishaji/ Tashihisi .... 64
4.4.5 Chuku .... 66
4.5 Taswira/ Jazanda .... 66
4.7 Muundo .... 71
4.8 Umbo la Utungo .... 72
4.9 Mandhari/Mahali .... 72
4.10 Hitimisho .... 73
**SURA YA TANO .... 74**
5.1 Hitimisho .... 74
5.2 Utangulizi .... 74
5.3 Muhtasari wa Utafiti Wetu .... 74
5.3 Ufaafu wa Nadharia .... 75
5.4 Mapendekezo .... 75
**MAREJELEO .... 76**

# SURA YA KWANZA

## 1.1 UTANGULIZI

Maulidi ya Nuni ni utungo uliotungwa na Sharifu Mansabu bin Sharifu' Abdu Rahmani al Husaini mnamo tarehe sita Jamadul Awal mwaka 1309 A.H tarehe 8, Desemba 1891. Utungo huu ulitungiwa sehemu ya Pate, Lamu na kulingana na mtunzi wake ni tafsiri ya *Maulidi ya Barzanji* (Knappert 1971).

Kulingana na Nassir (2002), maulidi ni neno linalotokana na neno la Kiarabu "mawlid" lenye maana ya mazazi au kuzaliwa kwa mtu. Kwa kawaida linapotumiwa na waislamu huwa na maana ya siku aliyozaliwa Mtume Muhammad (S.A.W.) au kikao kinachoekwa kusheherekea siku ya kuzaliwa kwa Mtume Muhammad (S.A.W.). ifikapo tarehe kumi na mbili ya mfungo sita kulingana na kalenda ya Kiislamu, Waislamu wa ulimwengu mzima husoma maulidi na kusheherekea siku hiyo kwa furaha kubwa. Sherehe hizi kwa desturi huwa haziishi tarehe hiyo tu bali huendelea hata kwa muda wa miezi miwili au hata mitatu baada ya tarehe kama tulivyoelezea. Sababu kuu ikiwa Waislamu wa kila nyumba, kila mtaa na kila nchi hutaka kushiriki katika sherehe hizi ili kupata baraka na pia huwapa Waislamu nafasi ya kutembeleana na kushirikiana katika sherehe hizi jambo ambalo lisingewezekana lau watu wote wangeliamua kufanya sherehe hizi kwa siku moja pekee.

Kulingana na Al- Busiri (2006), mazazi ya Mtume Muhammad (S.A.W.) yalidhihirisha kuja kwa ukweli na ucha Mungu ulimwenguni ikizingatiwa kuwa wakati wa ujahiliya watu katika sehemu za Uarabuni walikuwa wakifanya matendo maovu na machafu kama vile uasherati, kuzikwa kwa watoto wa kike pindi walipozaliwa wakiwa hai na maovu mengine mengi. Mazazi ya Mtume (S.A.W.) yalikuwa nuru iliyoangaza ulimwengu mzima na yalifinika kiza kilichokuweko wakati huo na wakati wa sasa na kuendelea hadi siku ya malipo. Nuru hii inafananishwa na ukweli uliokuwa umedhihirika kuhusu aliyokuja nayo Mtume Muhammad (S.A.W.) kwa waumini wake yakiwemo nguzo tano za Kiislamu ambazo ni shahada kwa kuamini kuwa hakuna Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, kuswali swala tano kwa siku, kufunga katika mwezi mtukufu wa Ramadhan, kutoa zaka kwa wenye uwezo kwa kuwapa wasiojiweza katika jamii ya Kiislamu na pia kwenda kutekeleza nguzo ya Hajj kwa kuzuru mji mtukufu wa Makka na kutekeleza ibada mbalimbali kwa wale wenye uwezo katika jamii. Kilele cha kuja kwa Kiumbe huyu mtukufu ilikuwa ni kukamilisha nguzo ya swala ambayo alikabidhiwa wakati wa safari yake ya kwenda mbinguni.

Nassir (2002) amesema kuwa maulidi huweza kuleta kumbukumbu kwa kuitukuza siku aliyozaliwa mbora wa viumbe wote, aliyewatoa walimwengu kutoka katika kiza na kuwaelekeza kwenye nuru. Kiza hiki bila shaka ni wakati ambapo maovu ya kila aina yalikuwa yamekithiri ulimwenguni na nuru ilijitokeza wakati wa kuletwa kwa Uislamu kupitia kwa Mtume Muhammad (S.A.W.), na kusoma maulidi ni njia moja ya kutoa shukrani kwa neema hiyo.

Kupitia kwa sherehe hizi, hupatikana fursa ya kukumbushana maisha ya Mtume Muhammad (S.A.W.) na mafunzo yake ambapo ni jukumu la kila Mwislamu kuzingatia na kuyafuata ili kupata malipo mema hapa duniani na kesho ahera. Mafunzo haya yamejikita katika nguzo tano za Uislamu na nguzo sita za Imani ambazo ni jukumu la kila Mwislamu kuzifuata.

Vilevile vikao hivi vya maulidi huleta madhehebu mbalimbali ya Waislamu kutoka mataifa mbalimbali kushirikiana na kuweka tofauti zao kando na hali hii huleta athari kubwa kwa wasiokuwa Waislamu kuupenda Uislamu na hata kusilimu. Kuna aina mbalimbali za maulidi kama vile *Maulidi ya Nuni, Maulidi ya Barzanji, Maulidi ya Mansabu, Maulidi ya Jambeni,* na mengineyo mengi. Maulidi tuliyoyataja yote yanazungumzia kuhusu mazazi ya Mtume (S.A.W.) na safari yake hadi uwingu wa saba. Tofauti ni kuwa watunzi wake ni tofauti. *Maulidi ya Nuni* yametungwa na Sharifu Mansabu, *Maulidi ya Barzanji* yametungwa na Ja'far bin Hassan al Barzanji, *Maulidi ya Mansabu* yametungwa na Sayidi Mansabu nayo *Maulidi ya Jambeni* yametungwa na Mohamed Jambeni.

Licha ya kuwa maulidi yana umuhimu mkubwa kwa Waislamu kama tulivyoeleza, kuna baadhi ya Waislamu wanaopinga maulidi kama tutakavyoona. Kulingana na Nassir (2002), wanaopinga maulidi wanadai kuwa sherehe hizi hazikuadhimishwa wakati wa Mtume Muhammad (S.A.W.) na hawaoni sababu ya wao kusheherekea wakati Mtume (S.A.W.) hayupo tena ulimwenguni na hakusisitiza sherehe hizi zifanywe. Vilevile wanadai kuwa kisomo hiki hakikusomwa wakati wa maswahaba na waliowafuata ambao walikuwa mstari wa mbele katika kutekeleza yote aliyokuja nayo Mtume Muhammad (S.A.W.). Kwenye sherehe za maulidi, hufanywa baadhi ya mambo ambayo hayastahili kufanywa kulingana na sharia za Kiislamu kama vile kutangamana kwa wanawake na wanaume na mengineyo. Pia hakuna ushahidi wowote katika Qur'an na hadithi za Mtume Muhammad (S.A.W.) unaothibitisha kutekelezwa kwa kisomo hiki.

Baada ya kueleza maana ya maulidi, umuhimu wake na sababu wanazotoa wapingao maulidi, hatuna budi kugusia fani kulingana na wataalamu mbalimabali na vipengele vinavyojihusisha ambavyo vina umuhimu katika utafiti huu.

Kulingana na Wamitila (2008), fani ni jumla ya nyenzo zinazotumiwa katika kazi yeyote ya fasihi kuwasilisha maudhui. Maudhui katika kazi ya kifasihi hayawezi kumfikia msomaji bila kuwepo na nyenzo za kuyapitisha. Uhusiano uliopo kati ya fani na maudhui ni wa kutegemeana kwani bila fani maudhui hayapo na maudhui nayo hayawezi kuwasilishwa bila ya kuwepo kwa fani. Uhusiano uliopo kati ya dhana hizi mbili ni muhimu kiasi kwamba fani inaweza kuhusishwa moja kwa moja na ujumbe au maudhui yenyewe kwa hivyo ni rahisi kusema kuwa fani ni ujumbe.

Katika kazi yoyote ya fasihi lazima kuwepo muundo, usanii wa lugha, ubunaji wa visa na vituko, ufinyazi wa wahusika na wasilisho la wakati, majira na mabadiliko ya mazingira katika hali ya kumteka msomaji au msikilizaji bila ya kumpa nafasi ya kuvuta pumzi. Jumla ya nyenzo hizi zote twaziita fani. Wanazuoni wa kisoshalisti wanalaumiwa sana na wanazuoni wa kibwanyeye kwa kusahau kwamba fani ina umuhimu katika kazi ya fasihi na kama kazi ya fasihi itakosa haki ya kuundwa katika fani inayostahili huwa si kazi ya fasihi. Kwa kweli wanazuoni wanasoshalisti hawakatai wala hawapingi umuhimu wa fani katika kazi ya fasihi lakini wanapinga ule mtindo wa kubuni kazi ya fasihi pamoja na wasilisho lake kwa njia ya kuitukuza bila ya kufikiria umuhimu wa maudhui. Maelezo haya ni kulingana na Issa na wenzake (1981).

Senkoro (1982), amesema istilahi nyingi zimetumiwa na wanazuoni kuelezea dhana ya fani kuwa ni kiumbiumbi cha nje kana kwamba haimo katika kazi ya kifasihi. Wahakiki wengine wameueleza uhusiano baina ya fani na maudhui kuwa sawa na ule wa kikombe (fani) na maji au chai iliyopo ndani ya kikombe hicho (maudhui). Baadhi ya wananadharia wamehusisha mahusiano hayo na yale ya sehemu ya ndani ya chungwa ambayo inaliwa (maudhui) na sehemu ya ganda la chungwa (fani). Udhaifu mkubwa wa istilahi na nadharia hizo ni kuwa zinatenganisha vitu ambavyo kimsingi havitenganishwi. Fani na maudhui ni sura mbili za sarafu moja.

Kulingana na Madumulla (1991), uchambuzi wa fani katika kazi ya fasihi ni njia moja ya kuielewa kazi ya fasihi. Anaendelea kusema kuwa fani ni aina ya uchambuzi ambayo hujumuisha sehemu zote zinazounda kazi ya fasihi na kutokea kuwa mkusanyiko ambao unaweza kuonyesha upekee wa mwandishi mmoja. Kujua fani husaidia kujifunza na kuifahamu kazi moja ikihusiana au kufananishwa na nyengine hasa kwa vile huzingatia lugha, dhamira wahusika, umbo la kazi hiyo na sehemu nyengine. Kwa sababu hii, fani husaidia kuielewa kazi moja kwa undani zaidi. Sehemu hizo tofauti za kazi ya fasihi huchunguzwa kwa mwingiliano unaokubaliana kulingana na kazi hiyo ilivyoundwa.

Kingei (2001), amesema kuwa fani ni vipengele vinavyodhihirisha ufundi wa kisanaa katika tungo zozote na ni kama chombo cha kuwakilisha ujumbe kwa wasomaji au wasikilizaji. Fani na maudhui ya utungo hutegemeana na kuathiriana. Mvuto na mnato wa utungo hutegemea uhodari wa mtunzi katika utungaji. Vipengele vya fani ni pamoja na muundo, mtindo, wahusika, mandhari, tamathali za usemi na matumizi ya lugha.

Maelezo haya yanatupa ufafanuzi kuhusu fani na kwamba kuna uhusiano mkubwa kati ya fani na maudhui kiasi kwamba kipengele kimoja hakiwezi kufanya kazi bila kuwepo kingine. Vipengele vyote viwili vinachangiana na kukamilishana ili kutekeleza dhamira ya fasihi. Kinachobainika ni kuwa mtunzi yeyote huwa na njia ambazo hutumia ili kufikia hadhira yake na njia hizi ndizo zinazojulikana kama fani.

Vipengele vya fani ni pamoja na muundo, mtindo, wahusika, mandhari na matumizi ya lugha. Katika utafiti wetu tumeshughulikia fani katika Maulidi ya Nuni na vipengele tulivyovishughulikia ni wahusika na uhusika, matumizi ya lugha, tamathali za usemi, taswira au jazanda pamoja na muundo na mandhari.

Wahusika waliojitokeza katika utungo huu ni pamoja na Mwenyezi Mungu, Mtume Muhammad (S.A.W.), Jibrili, Munkar na Malaika wenzake, Amina, Thuweiba, Halima, Mariyamu binti Imrani, mwana Asiya, Khadija, Maisara, Maria Kibtiya, wanawake wema, Abdalla, Abdulmutalib, Abutalib, mjombake Thuweiba, Abubakar, mitume, watoto wa Mtume Muhammad (S.A.W), mahurulaini, maswahaba, muhajirun na ansar, wanyama, miti ya mitende na majabali pamoja na wahusika wengine.

Katika matumizi ya lugha tumeshughulikia Kiamu, Kingozi na maneno ya Kiarabu. Katika tamathali za usemi tumeangalia takriri, tashbihi au tashbiha, istiari, uhuishaji au tashihisi, pamoja na chuku pia tumeshughulikia taswira au jazanda. Katika muundo tumerejelea umbo na mpatano, mshikamano na uhusiano wa visehemu tofauti vya kazi hii pamoja na uhuru wa mtunzi ambapo tumeshughulikia inkisari, mazida na tabdila. Katika mandhari tumechunguza nafasi ya mahali tukizingatia kwamba kila jambo au tukio hufanyika mahali fulani.

## 1.2 TATIZO LA UTAFITI

Tatizo letu la utafiti ni fani katika *Maulidi ya Nuni*. Fani ni kiungo kimojawapo kinachoipa kazi ya fasihi mvuto na mnato wa aina yake. Ni kupitia kwa fani ambapo mtunzi hufikia hadhira yake kulingana na dhamira husika. Matumizi mazuri ya vipengele vya fani huipa kazi husika hadhi, nayo matumizi mabaya ya kipengele hiki huishusha hadhi kazi husika. Ndiposa tunasema kuwa mtunzi wa utungo wowote huhitaji ubunifu wa hali ya juu ili kufanikisha malengo yake. Na hii ni sababu moja ya kutafiti *fani katika Maulidi ya Nuni* ili kuziba pengo lililopo.

Tungo nyingi za kale hazijashughulikiwa katika karne ya ishirini na moja ndiposa Wamutiso (1996), anahoji kwamba zinaogopewa na wanafunzi wengi hata wale ambao Kiswahili ni lugha yao ya kwanza. Kulingana na Wamutiso, woga wa wanafunzi hawa unatokana na sababu kwamba lugha inayotumiwa ni chakavu na ni mchanganyiko wa lahaja nyingi mno. Hatuafikiani moja kwa moja na maoni haya ya Wamutiso kwa sababu kuna ushahidi unaonyesha kuwa tungo za kale zimeshughulikiwa upande wa tafsiri hususani na Knappert (1964,1967,1971,1979), Harries (1962), na Allen (1971), Jambo hili pia limetutia mshawasha katika kutafiti utungo huu ili kujaliza pengo lililopo.

Watafiti wengi walioshughulikia tungo za kale hasa za Kiislamu wametumia nadharia ya uhalisia ajabu ikizingatiwa kuwa tungo nyingi za kidini zina sifa za kiuajabu ajabu hasa zinapowasawiri wahusika wao. Kwa mfano Vutagwa (2013) ameshughulikia *Sifa za Kiuhalisiajabu katika Utenzi wa mwana Fatuma*. Jambo hili pia limetushawishi kutumia nadharia ya mtindo katika utafiti wetu ili kujaza pengo lililopo. Japokuwa wako watafiti ambao wameegemea upande wa fani katika tungo nyengine za kidini kama vile *Utenzi wa Ayubu, Utenzi wa mwana Fatuma, Utenzi wa Nabii Issa, Kutawafukwe kwa Mtume, Ukawafi wa Miiraji* n.k, kwa maoni yetu, tumeamua kushughulikia swala la *fani katika Maulidi ya Nuni* ili kujaza pengo lililopo.

Tumetambua kuwa kuna uhaba mkubwa sana wa marejeleo ya miswada hasa ya kimtindo katika tungo za kale ndiposa watafiti wengi wameegemea katika uhakiki wa riwaya na tamthilia wakitumia nadharia tofautitofauti kuliko uhakiki wa tungo za kale za Kiswahili. Kwa hivyo hili ni pengo ambalo linahitaji kuzibwa.

## 1.3 MALENGO YA UTAFITI

1 Kuchunguza nafasi ya wahusika na uhusika katika *Maulidi ya Nuni.*
2. Kuchanganua matumizi ya lugha, tamathali za usemi, taswira au jazanda, muundo na mandhari katika *Maulidi ya Nuni.*

## 1.4 MASWALI YA UTAFITI

1. Wahusika na uhusika una nafasi gani katika *Maulidi ya Nuni?*
2. Matumizi ya lugha, tamathali za usemi, taswira au jazanda, muundo na mandhari zimetumika vipi katika *Maulidi ya Nuni?*

## 1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA

*Maulidi ya Nuni* ni utungo wa kale ambao mtunzi wake anatoka katika sehemu ya Afrika Mashariki. Utungo huu una mafunzo mengi ambayo binadamu yeyote, awe Mwislamu au la angependa kufahamu kuhusu mazazi na vilevile safari ya Mtume (S.A.W.) kutoka uwingu wa kwanza hadi wa saba. Mazazi yake, kukua kwake hadi kwenda safari ya usiku mmoja kuna thibitisha ukubwa na utukufu wa Mwenyezi Mungu, kuwa Yeye anafanya alitakalo bila kushurutishwa na kiumbe yeyote. Pia ana hiyari ya kumchagua yeyote bila kuulizwa sababu. Hali hii inathibitishwa na Mtume Muhammad (S.A.W.), kwa kuchaguliwa kuwa Mtume wa mwisho kwa walimwengu wote, kupewa kitabu cha mwisho ambacho ni Qur'an Tukufu kilicho na mwongozo kamili kwa wamchao Mwenyezi Mungu, na kupewa nguzo ya swala ambayo ni nguzo muhimu kwa waumini wa Kiislamu. Kule kuwa haya maulidi yana umuhimu sana kwa Waislamu ni sababu moja inayotushawishi kuufanyia utungo huu utafiti.

Utungo huu umejaa mafunzo mengi kwa binadamu wote, lakini mafunzo haya yameandikwa kwa msamiati wa kale (Kingozi) na wa Kiarabu, ambapo ni vigumu kwa wengi kuelewa. Jambo hili pia limetutia motisha tufanye utafiti huu ili iwe rahisi kwa wanafasihi au wote wanaotaka kupata mafunzo kuhusu utungo huu hususan katika maswala ya fani.

Utungo huu umeshughulikiwa na wanafasihi kama vile Knappert (1979) katika upande wa tafsiri na kwa maoni yetu, suala la fani katika *Maulidi ya Nuni* halijashughulikiwa na mwandishi yeyote japokuwa linajitokeza katika utungo wote. Kupitia kwa fani, dhamira ya mtunzi inatimizwa kwa sababu ni kiungo muhimu cha kufanikisha kazi yoyote ya kifasihi. Sababu hii vile vile imetupa mshawasha wa kuendelea na utafiti huu.

Tunaamini kwamba utafiti wetu utakuwa msingi wa kuwaongoza watafiti wa baadaye, hususan kwa wale watakaokuwa na nia ya kuchanganua vipengele vingine vya fani au maudhui katika *Maulidi ya Nuni* au tungo nyengine zozote.

Kwa maoni yetu utafiti huu umechangia sihaba katika nyanja ya tungo za Kiswahili za kale ambazo kulingana na WaMutiso (1996:2), wasomi wengi wa Kiswahili wanaonekana kupoteza hamu katika fasihi ya Kiswahili ya Kiislamu (kale), siajabu imeonekana na kuchukuliwa kama ngeni. Tunaamini kwamba utafiti huu umetoa changamoto kwa watafiti na wasomi wa fasihi ya Kiswahili kutafiti vipengele vingine vya fani sio tu katika *Maulidi ya Nuni* bali pia katika tungo za Kiswahili, haswa za Kiislamu na za jadi.

## 1.6 UPEO NA MIPAKA

Kuna aina mbalimbali za Maulidi kama vile *Maulidi ya Nuni*, *Maulidi ya Jambeni*, *Maulidi ya Barzanji*, *Maulidi ya Mansabu* n.k. Utafiti huu unahusu fani katika *Maulidi ya Nuni* yenye beti mia moja na thelathini. Japokuwa fani ni nyenzo zinazotumiwa katika kazi yoyote ya fasihi kuwasilisha maudhui, hatutashughulikia swala la maudhui isipokuwa pengine katika kuelezea vipengele vya fani tulivyovishughulikia ambavyo ni nafasi ya wahusika na uhusika, matumizi ya lugha, tamathali za usemi, taswira au jazanda, muundo na mandhari. Wahusika tuliowashughulikia ni: Mwenyezi Mungu, Mtume Muhammad (S.A.W.), Jibrili na Malaika wenzake, wanawake kwa jumla: Amina, Thuweiba, Halima, Mariyamu binti Imran na mwana Asiya, Hadija, Maisara, Maria Kibtiya pamoja na wanawake wema. Wahusika wanaume kama: Abdalla, Abdulmuttalib, Abutalib, mjombake Thuweba na Abubakar, mitume na manabii, watoto wa Mtume Muhammad (S.A.W.), mahurulaini, maswahaba, muhajirun, ansar na wahusika wengine. Kwa upande wa matumizi ya lugha tumeangalia: Kingozi, Kiamu, na maneno ya Kiarabu. Katika tamathali za usemi tumeangalia: Takriri, tashibihi, istiari, uhuishaji/tashihisi na chuku pia tumeshughulikia taswira au jazanda. Katika uhuru wa mshairi tumeshughulikia: inkisari, mazida na tabdila. Vilevile tumeshughulikia muundo, umbo la utungo na mandhari katika *Maulidi ya Nuni*.

## 1.7 MSINGI WA NADHARIA

Nadharia ya mtindo ambayo ni mwafaka katika utafiti wetu hurejelea jinsi lugha inavyotumiwa katika muktadha fulani ikihusisha mtu fulani na kwa lengo fulani. Maelezo haya ni kwa mujibu wa Leech na Short (1981:10), ambayo yanaafikiana na yale ya Ferdinand de Saussure aliyefafanua na kutofautisha dhana za "langue" na "parole" ambapo alijikita kwenye mkabala wa lugha. Aliendelea kusema kwamba, "langue ni mfumo wa lugha ya jamii husika na "parole" inahusisha matumizi ya lugha ya mzungumzaji binafsi na ndiposa huitumia kwenye uandishi na vilevile uzungumzaji.

Kulingana na utangulizi huu, mtindo unaweza kushabihishwa na "parole" kwa vile unajikita kwenye utaratibu wa kanuni zinazojitokeza katika lugha teule na ndiposa inasemekana kuwa kanuni za lugha huundwa kutokana na lugha ya msemaji yaani "langage" na vilevile kanuni za lugha yaani "langue" inapojumuishwa na matumizi yake kimazungumzo na kimaandishi. Maelezo haya ni kulingana na Leech na Short (1981: 10-11).

Crystal na Davy (1969), wanadai kwamba mtindo hujikita kwenye uzoefu wa lugha husika na huenda ikawa lugha ya mtu binafsi au ya jamii kwa ujumla. Kwa maana hii, mtindo ni utaratibu mzima wa kujieleza katika maandishi au mazungumzo. Leech na Short (1981) wanasema mtindo ni ukiushi katika ujumla wa matumizi ya lugha iwe ya kifasihi au isiyo ya kifasihi na hususan huhusisha lugha za kimapokeo.

Mwasisi wa nadharia hii ni Leech na athari za nadharia hii zilipatikana katika tasnifu yake ambayo isimu ya kisasa ilihusishwa na usomaji na vilevile ufundishaji wa lugha ya fasihi. Viwango vinavyojitokeza katika uchanganuzi wa nadharia hii, ni matumizi ya lugha ambapo kuna vipengele mbalimbali katika upande wa msamiati, sarufi, lahaja, sajili, fonolojia, maandishi, historia na semantiki. Katika kazi yetu, tumetumia kiwango cha matumizi ya lugha na hususan tumejikita katika maandishi, muundo wa masimulizi hali kadhalika mbinu za uwasilishaji usemi na mawazo.

Kulingana na Wamitila (2008) na Leech (1969), vipengele muhimu vinavyochunguzwa katika kiwango cha matumizi ya lugha ni vipengele vya kifonetiki, kifonolojia na vilevile kimaandishi na huonyesha jinsi lugha inavyotamkwa au kuandikwa.

Aghalabu, kazi za kifasihi ikiwemo utungo huu huwa na sifa za matumizi ya lugha ambazo hutilia uzito msamiati . Msamiati hautumiwi tu kumaanisha maneno magumu katika lugha bali ni jumla ya maneno yanayopatikana katika lugha. Msamiati ni nyenzo ya kimsingi aliyo nayo mwandishi na nyenzo hii ina nafasi na umuhimu mkubwa katika utunzi na uandishi wake. Uwasilishaji wa ujumbe, dhamira na tasnifu hutegemea msamiati wake na jinsi anavyouteua msamiati huo. Kwa msingi huu basi ni muhimu kuchunguza suala zima la uteuzi na mpangilio wa msamiati. Uteuzi wa msamiati unahakikisha kuwa hadhira lengwa imeathiriwa na utungo wowote ule. Kulingana na maelezo haya, kuna matumizi ya lahaja ya Kiamu, maneno ya Kiarabu na pia matumizi ya Kingozi ambapo mtunzi ametumia ili kufanikisha dhamira yake.

Wamitila (2008), amesema tamathali za usemi aghalabu huhusisha ukiushi au ukiukaji wa aina fulani ambapo neno au kifungu fulani hutumiwa kwa maana ambayo ni tofauti na maana ya kimsingi. Tamathali za usemi huchukua nafasi muhimu katika uchanganuzi wa mtindo katika kazi za fasihi na zinatumiwa kwa upana usiokuwa wa kawaida ili kujumlisha sifa nyingi za kimtindo ambazo hutumiwa katika kazi za kifasihi. Katika kazi yetu tumechanganua tamathali za usemi zifuatazo: takriri, tashibihi, istiari, uhuishaji/tashihisi, pamoja na chuku pia tumeshughulikia taswira au jazanda.

Katika kazi ya kifasihi, muundo wa masimulizi  hurejelea hali au matukio katika kazi yoyote ya kifasihi na ni lazima yafuate ruwaza fulani. Msuko huweza kuwa wa moja kwa moja au changamano. Mpangilio wa matukio huandamana na wakati toka mwanzo hadi mwisho. Vilevile kuna maelezo au masimulizi na wakati mwingi huwepo sauti inayotoa masimulizi ama ya mwandishi au mhusika. Masimulizi huweza kutolewa katika nafsi ya kwanza au ya tatu ambapo mhakiki atabainisha sifa za kimtindo na athari yake kwa wanaosimuliwa. Wamitila (2008), amesema kuwa kazi za kifasihi huwa na muundo wenye sehemu tatu, ambazo ni mwanzo, kati, na mwisho na ambapo katika tungo aghalabu mwanzo wake huwa dua au maombi, dhamira na maudhui na mwisho kumalizia na dua au maombi. Sehemu zote tatu zinahusisha wahusika na uhusika katika hali zote.

Kulingana na Wamitila (2008), mbinu za uwasilishaji usemi na mawazo huchunguza mazungumzo au usemezano baina ya wahusika na mbinu nyengine ambazo zinatumiwa katika mazungumzo hayo kwa lengo la kuwasilisha usemi na mawazo ya wahusika.

Ngara (1982), amesema wahusika wanawakilisha matumizi ya lugha ya kawaida katika jamii kama binadamu wa kawaida. Binadamu hutumia lugha kwa njia ambazo zinatofautiana katika viwango vya msamiati, miundo ya sentensi, mkazo n.k. Tofauti hizi za kimatumizi huonekana katika tungo za kifasihi. Kutofautisha wahusika katika misingi ya matumizi ya lugha ni sifa nzuri ya uandishi na matumizi yao yanaakisi matumizi ya lugha katika jamii.

Katika kazi yetu, tumeshughulikia dhana ya wahusika na uhusika kwa kutumia mbinu ya kisimulizi ambapo mhusika anasawiriwa kupitia kwa usimulizi, wasifu wake, msukumo wa matendo yake, mazingira yake, tabia na amali zake zinazosimuliwa na msimulizi ambaye anataka msomaji auone mtazamo huo na labda hata akubaliane naye. Kwa kiasi kikubwa mhusika mwenyewe anakuwa kiumbe asiyekuwa na uwezo wa kuathiri mtazamo huo ambao unamwangalia kwa nje. Huu ni mtindo ambao unatumiwa na watunzi wengi wa kifasihi na ambao kwa kiasi kikubwa unafungamana na jinsi binadamu wanavyowaangalia binadamu wenzao kwa nje. Maelezo haya ni kulingana na Wamitila (2008).

Kwa upande wa muundo, tumerejelea umbo na mpatano, mshikamano na uhusiano wa visehemu tofauti vya kazi hii na kuleta sifa ambazo zinatenganisha na kutambulisha mtunzi. Pia tumechunguza uhuru wa mtunzi ambapo tumeshughulikia matumizi ya inkisari, mazida pamoja na tabdila.

Wahusika wamewekwa wazi kwa njia ambayo inadhihirika sana na mandhari. Uhusiano unaotokea baina ya mhusika na mandhari unaweza kuwa wa kimapatano, wa kukinzana au ukazua mgogoro. Katika kazi yetu, kuna mandhari ya kijiografia, mandhari yasiyo halisi, mandhari ya Uarabuni, na mandhari ya kimapatano.

## 1.8 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO LA UTAFITI

Kuna tafiti mbalimbali zilizoshughulikia tungo mbalimbali kama ambavyo tumeeleza. Knappert (1979) anatupa maelezo kuhusu *Utenzi wa Tambuka* unaohusu vita baina ya Waislamu na Wakristo huko Syria. Kulingana na Knappert, mtunzi wa utungo huu ni Mwislamu aliyeelewa vyema mihimili ya dini ya kiislamu na utamaduni wake. Maelezo haya yametupa mwelekeo katika kazi yetu haswa ikizingatiwa kwamba utungo tunaoushughulikia una mihimili ya Kiislamu na vilevile umetusaidia kujua utenzi huo unahusu nini. Maelezo haya ya Knappert yanatupa mwelekeo kuhusu utenzi lakini hayatoi mchango mkubwa katika kazi yetu kwa sababu kipengele cha fani hakikushughulikiwa ila fasiri tu.

Mung'ania (1985), alishughulikia maudhui mbali mbali katika ushairi wa Mathias E. Mnyampala (Penda Chako). Alichunguza jinsi Mnyampala alijitokeza kuendeleza harakati za mapambano ya jamii yake. Anasema kwamba jazanda anazotumia Mnyampala zinayafanya mashairi yake yaeleweke kwa urahisi. Maelezo haya yametusaidia katika kazi yetu kwa sababu *Maulidi ya Nuni* vilevile yametumia jazanda au taswira na hivyo kueleweka vyema licha ya kuwa yameandikwa katika lahaja ya Kiamu. Tofauti ni kuwa utungo wetu umejikita katika mihimili ya dini ya Uislamu ambapo wao umejikita katika maswala ya kijamii.

Omwoyo (1997), alitafiti *fani katika ushairi wa Hassan Mwalimu Mbega* ambapo alishughulikia *Upisho wa Malenga* na *Dafina ya Malenga*. Katika matokeo yake ya utafiti, amesema kwamba fani ina mchango mkubwa katika kueleza malengo ya msanii na pia ni kipengele muhimu sana cha fasihi. Maelezo haya yanalingana na utafiti wetu lakini tofauti ni kwamba sisi tumeangalia fani katika *Maulidi ya Nuni.*

Wa Mutiso (1985), ameshughulikia maudhui ya hurafa na uyakinifu katika *Utenzi wa Hamziya*. Katika tasnifu yake ya Uzamili ameshughulikia sifa apewazo Mtume Muhammad (S.A.W) na zile za mashujaa wengine duniani. Kazi yake hii imetusaidia katika kushughulikia mada yetu kwa sababu ni kupitia kwa kipengele cha fani ambacho kimemwezesha kuchambua maudhui. Vilevile wahusika ni kipengele kimoja cha fani na miongoni mwa wahusika tuliowashughulikia ni Mtume Muhammad (S.A.W). Tofauti ni kuwa wao wameshughulikia kipengele cha maudhui ambacho sisi hatukukigusa.

Wa Mberia (1989), ameshughulikia *Utenzi wa Fumo Liyongo* kwa kutathmini sifa za Fumo Liyongo kama shujaa wa masimulizi. Katika kazi yake sifa hizi ni tofauti na mhusika Mtume Muhammad (S.A.W) katika utungo huu, ikizingatiwa kwamba ni mhusika anayekuzwa katika mihimili ya dini ya Kiislamu kwa hivyo kazi hii imetusaidia katika kutofautisha sifa za shujaa wa kidini na wa kiulimwengu.

Kasilu (2003), ametafiti mwingiliano wa fani na maudhui katika ushairi wa Kithaka wa Mberia ambapo alijikita katika diwani za *Mchezo wa Karata na Bara Jingine*. Matokeo ya utafiti huu ni kwamba, uteuzi wa vipengele vya fani una mchango mkubwa katika kazi yake na aliangazia vipengele vya fani kama vile; tashbihi, takriri, sitiari, taashira, maswali ya balagha na msisitizo bayana. Kazi yake imetupa mwelekeo kwa sababu matokeo ya kazi yetu

yamedhihirisha kwamba baadhi ya vipengele vya fani alivyotafiti vilevile vimejitokeza katika utafiti wetu kama vile tashbihi, takriri na sitiari. Tofauti ni kwamba, sisi tumeshughulikia fani katika *Maulidi ya Nuni*

Mungai (2005), ameshughulikia fani katika *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa* akilinganisha na *Utenzi wa Nguvumali*. Utafiti wake umetusaidia katika kazi yetu kwa sababu vipengele vya fani alivyotafiti ndivyo tulivyotafiti kwa hivyo kazi yake imetusaidia vilivyo japokuwa sisi tunaangalia fani katika *Maulidi ya Nuni.*

Vilevile wa Mutiso (2005), katika *Utenzi wa Hamziya* ameshughulikia kipengele cha fani na baadhi ya dhana alizozishughulikia ni; matumizi ya lugha, tamathali za usemi, muundo au mpangilio wa matukio, mandhari au mazingira, uhusika na wahusika n.k. Kazi yake imetupa mwongozo katika somo letu la utafiti kwa sababu ni mambo yaya haya tuliyoyashughulikia na pia utungo huu umejikita katika mihimili ya kidini na unasadifiana na kazi yetu. Tofauti ni kuwa kazi yetu imejikita katika *Maulidi ya Nuni.*

Wesa (2005), ameshughulikia uhakiki na uchambuzi wa fani katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*. Utafiti huu umetusaidia kutambua vipengele muhimu vya fani baadhi yake vikiwa wahusika na sitiari ambavyo pia tumevishughulikia katika kazi yetu. Vilevile utenzi huu umejikita katika mihimili ya kidini japokuwa maelezo yake ni tofauti na yaliyomo katika *Maulidi ya Nuni.*

Mwilaria (2011), ameshughulikia fani katika *Utenzi wa Ayubu* na ameangazia vipengele mbalimbali vya fani ambavyo tumeshughulikia vikiwa ni tamathali za usemi na wahusika. Kazi hii vilevile imetusaidia katika utafiti wetu kwa sababu tungo zote mbili zimejikita katika mihimili ya kidini na kuna baadhi ya wahusika kama vile Mwenyezi Mungu na malaika Jibrili ambao pia sisi tumewashughulikia. Tofauti ni kuwa utafiti wa Mwilaria umeongozwa na nadharia ya urasimu wa Kirusi nao utafiti wetu umeongozwa na nadharia ya mtindo.

Omar (2012), ameshughulikia uchambuzi wa tamathali za usemi pamoja na mbinu nyengine za matumizi ya Lugha katika *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa.* Kazi hii vilevile imetusaidia kwa kutupa mwongozo wa jinsi ya kuchunguza matumizi ya lugha kama vile taswira, jazanda n.k na vilevile jinsi ya kuchunguza tamathali za usemi kama vile takriri, chuku tashbihi n.k tofauti ni kuwa sisi tumeshughulikia *Fani katika Maulidi ya Nuni* .

Kulingana na Vutagwa (2013), kuna wahusika aina mbili, ambao ni binadamu na viumbe ambao si binadamu. Wahusika binadamu ni pamoja na Mtume Muhammad, Ali na Fatuma nao wahusika ambao si binadamu ni Allah, Malaika Jibrili, Mikail na malaika wengineo. Kazi hii imetusaidia kwa sababu sisi pia tumewashughulikia wahusika kama Mtume Muhammad (S.A.W.), Malaika Jibrili na wengineo. Tofauti ni kuwa amewashughulikia wahusika hawa kupitia majukumu yao na sisi tumewashughulikia wahusika kupitia sifa zao.

## 1.9 NJIA ZA UTAFITI

Utafiti huu ni wa kifasihi na umejikita katika fasihi andishi. Kwa hivyo, tumefanya kazi nyingi maktabani. Tumesoma *Maulidi ya Nuni* yenye beti 130 na hali kadhalika tumesoma kazi mbali mbali zinazogusia vipengele vya fani kama wahusika, matumizi ya lugha, tamathali za usemi, taswira au jazanda, muundo na mandhari hususan zinazojikita katika dini zilizotusaidia katika utafiti wetu, zikiwemo tasnifu mbali mbali, majarida, diwani za ushairi na miswada mbalimbali.

Kwa kuwa *Maulidi ya Nuni* yameandikwa katika mtazamo wa dini ya Kiislamu, tumevisoma vitabu mbalimbali vikiwemo *Qur'ani Tukufu* na vitabu vya dini vilivyotusaidia kuelewa utungo huu. Vilevile tumewajumuisha walimu wa madrassa wakiwemo mashehe ambao wametupa mwongozo na mawazo mengi katika somo letu la utafiti.

Hali kadhalika, tumechunguza fani katika *Maulidi ya Nuni* na mchango wake katika kufanikisha kazi hii. Hatukuwa na budi kupitia mtandaoni ili kupata yaliyofanywa kuhusu mada yetu ya utafiti na vilevile tumeangalia yaliyofanywa hususan kuhusu nadharia ya mtindo ambayo tumeitumia.

## 1.10 HITIMISHO

Katika sura hii, tumeshughulikia somo letu la utafiti ambalo ni fani katika *Maulidi ya Nuni*. Katika sehemu ya utangulizi, tumeelezea muhtasari kuhusu *Maulidi ya Nuni*, vilevile tumeelezea kuhusu maulidi kwa ujumla, umuhimu na aina zake na tumetoa sababu za wapingao maulidi. Pia tumetoa maoni ya wataalamu mbalimbali kuhusu fani pamoja na kipengele cha wahusika. Tumejadili tatizo letu la utafiti kwa kuonyesha pengo lililopo, huku tukipiga hatua kwa kueleza malengo ya utafiti hali kadhalika maswali ya utafiti. Vilevile, tumetoa sababu za kuchagua somo la utafiti hali kadhalika upeo na mipaka. Pia tumeangalia

msingi wa nadharia iliyotuongoza katika utafiti wetu ambayo ni mtindo. Tumejadili mihimili ya nadharia hii na kuonyesha jinsi tulivyoitumia. Tumeangazia yaliyoandikwa kuhusu somo letu la utafiti kwa kupitia kazi mbalimbali zilizofanywa zikiwemo tasnifu na makala mbalimbali na vilevile tumetilia maanani njia za utafiti kwa kueleza jinsi tulivyotatua tatizo letu la utafiti.

## SURA YA PILI

### 2.1 MISINGI YA UHAKIKI WA FANI

### 2.2 UTANGULIZI

Katika sura ya kwanza, tumejadili dhana za maulidi na fani. Katika sura hii tutashughulikia dhana zinazojikita katika fani ambazo tumezishughulikia katika kazi yetu. Tumeanza kwa kutoa muhtasari kuhusu *Maulidi ya Nuni.*

### 2.3 MAULIDI YA NUNI

*Maulidi ya Nuni* yanafungua kurasa kwa kueleza mambo muhimu yanayotekelezwa ambayo miongoni mwao ni kusoma Qur'an ikitangulizwa na suratul Fatiha, sala za Mtume (S.A.W.) na salamu za Maulana. Kulingana na utungo huu, maulidi yanayosifiwa ni *Maulidi ya Barzanji* ambayo yametungwa katika lugha ya Kiarabu ili kueleweka vyema na wenyeji na hivyo kufikisha ujumbe kwa hadhira lengwa.

Kulingana na utungo huu, maswahaba hawakuadhimisha maulidi mpaka alipofariki Mtume Muhammad (S.A.W.) ambapo kulichangiwa na Mudhafari aliyetumia dinari laki tatu na watu walipouliza kuhusu umuhimu wake, walielezwa kwamba watapata amani na baraka mwaka mzima, hawatapatikana na balaa yoyote ikiwemo wezi hali kadhalika nyumba kuchomeka. Vilevile watakayopata wakiondoka ulimwenguni ni kuwa hawatapata shida wakati watakapoulizwa maswali na malaika Munkar wakiwa kaburini. Kulingana na maulidi haya, mavazi ya asomaye maulidi haya yatakuwa yametengenezwa na hariri na vilevile atafufuliwa na mitume na mashahidi. Mtunzi anatoa kisa cha kijana ambaye babake alifariki na kumwachia kidinari na aliposikia maulidi yakisomwa alikaa na kusikiliza. Hali kadhalika kuna mtu aliyepata nyumba lakini kijana akaona nyumba nzuri zaidi ambayo alitamani lakini akaambiwa kwamba ni malipo ya wanaosoma maulidi pekee. Baada ya miujiza hii, kulipopambauka kijana huyu alitumia dinari akaandaa chakula na kusoma maulidi. ambapo hatimaye alimuota mamake akimuombea ili apate jaza njema kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Baada ya mama kuona jitihada ya mwanawe, alijipulizia manukato na hatimaye kumbusu mwanawe kwenye bapa la uso kwa sababu ya kitendo alichokifanya.

Kabla ya maulidi haya kusomwa, maandalizi hufanywa ambayo ni pamoja na mahali pazuri, kuwasha taa katika mkusanyiko wa watu, kuvaa nguo nzuri zilizotiwa manukato, kufunga

kilemba ambacho ni ishara ya kuonyesha heshima, vilevile suratul Fatiha hutangulizwa na baadaye yatajwe majina tisini na tisa ya Mwenyezi Mungu. Inatakikana kuwe na vitu vya tamu na vilevile mayatima washughulikiwe ili kusheherekea mazazi ya Mtume Muhammad (S.A.W.). Mambo haya yote hufanywa ili kuonyesha heshima na ukarimu kwa waumini wote ikizingatiwa kuwa hizi ni baadhi ya sifa alizokuwa nazo Mtume Muhammad (S.A.W.) na kusheherekea mazazi yake kunathibitisha kuwa wafuasi wake hawajaachwa nyuma.

Utungo unatupa maelezo kuhusu Amina ambaye alipopata ujauzito hata wanyama wa Makureishi walisikika wakitamka na kila miezi ilipoongezeka wanyama hawa walizidi kuitangaza mimba ya Muhammad (S.A.W.). Vilevile, Malaika wa mbinguni walikuwa na ufahamu kuhusu mimba ya Mtume Muhammad (S.A.W.).

Ujauzito wa Amina ulipokamilika, walioshuhudia mazazi yake walikuwa wanawake wanne ambao uzuri wao haujawahi kuonekana; wawili wao walikuwa mahurulaini wa peponi na wawili wa duniani ambao walikuwa ni Mariyamu wa Imrani na mwana Asiya. Mtume (S.A.W) alipozaliwa, sala na salamu zilimshukia na uzuri wake haukuweza kuelezwa na sifa zote zilimshukia kwa kuwa ndiye Mtume wa mwisho.

Baada ya Mtume (S.A.W) kuzaliwa, babu yake Abdulmutalib alimchukua na kumpeleka kwenye Al-Kaaba kumuombea ili awe na afya njema. Mamake alimnyonyesha kwa muda wa siku saba na baadaye Thuweiba ambaye alikuwa mwanamke mwongofu, alimlea Mtume ambaye alifuatiwa na Halima ambaye alimnyonyesha. Kukua kwake kulikuwa kwa maajabu, ambapo alipofika miezi mitatu alianza kutembea.

Mtume (S.A.W.) alipokuwa anatoka safarini, Bi Khadija aliyekuwa ghorofani na wenzake alimuona Mtume (S.A.W.) akiandamwa na Malaika kutoka mbinguni ambaye alimhifadhi na mbawa zake kutokana na miale ya jua, na hatimaye bi Khadija alimtuma Maisara kwa Mtume (S.A.W.) akitaka kuolewa naye. Baada ya Mtume (S.A.W) kuwaelezea wazee wake upande wa baba alikubaliwa. Bi Khadija alizaa naye watoto sita.

Mwanzo wa kuteremshwa wahyi kupitia ndoto kulikuwa bayana; mwanzoni kulimtishia Mtume (S.A.W) lakini baadaye alizoea. Hatimaye alielekea safari ya mbinguni kupitia msikiti wa Makdisi na kwenda kukabidhiwa nguzo ya swala na Mwenyezi Mungu. Alipokuwa msikiti wa Makdisi, Mtume (S.A.W) aliwaongoza mitume na manabii pamoja na

malaika na maruhani katika sala; alifupisha sala na kupanda ngazi ambayo ilikuwa imepambwa na alipita uwingu mmoja hadi mwengine mpaka uwingu wa saba.

Baada ya safari hii tukufu, Abubakar alimwamini Mtume (S.A.W), lakini Makureishi wa Makka hawakumwamini aliyokuja nayo baada ya safari yake ya mbinguni yakiwemo yote aliyoyaona na aliyopewa ikiwemo nguzo ya swala. Nao malaika na majini hawakuwahi kumuona mzuri wa sura na tabia kama Mtume ambaye alikuwa mvumilivu katika maisha yake. Vilevile aliahidiwa kila aina ya ukwasi mpaka milima ilisema itageuka dhahabu lakini alikataa kwani lengo lake kuu lilikuwa Janna.

Mtunzi anamalizia kwa maombi kwa Mola, ili Waislamu wapate taufiki, haja zao zikidhiwe, wapate amani neema na saada na mwisho kabisa sala na salamu zimwendee Mtume, jamaa zake, maswahaba zake na wote wanaomfuata na baraka na kila jema la duniani na ahera na mwishowe makazi yawe janna**.**

## 2.4 WAHUSIKA NA UHUSIKA

Uhusika ni umithilishaji wa vitendo vya viumbe katika kazi za kifasihi na vile vya viumbe katika ulimwengu razini. Vitendo vya viumbe hawa husababishwa na kuingiliana kwao na mazingira ya ubunifu, kama ambavyo vitendo vya viumbe razini huwa vimesababishwa na maingiliano baina wao wenyewe na mazingira yao, ambayo ni razini. Maelezo haya ni kulingana na Njogu na Chimera (2008).

Kulingana na Wamitila (2008), mhusika ni mtendaji katika kazi ya kifasihi na huwa kielelezo cha viumbe wanaopatikana ulimwenguni ingawa si lazima sifa zote za mhusika zifungamane moja kwa moja na za wanadamu. Mwelekeo wa kuwahusisha wahusika wa kifasihi na binadamu wanaopatikana katika hali halisi huathiri kwa kiasi fulani matarajio ya usawiri wa uhusika. Maelezo haya yanasadifiana na jinsi wahusika na uhusika unavyojitokeza katika *Maulidi ya Nuni* na athari zake, mazingatio makuu yakijitokeza katika kuendeleza dini.

Kulingana na Wa Mutiso (2005), wahusika wanaweza kusawiriwa kama wahusika wa kawaida au wahusika wasio wa kawaida. Katika *Maulidi ya Nuni* kuna wahusika wa kawaida hususan wa kibinadamu kama vile Mtume Muhammad, Abdalla, Amina mama yake Mtume (S.A.W), babu yake Mtume, waumini waliomcha Mwenyezi Mungu, Makureishi, mayatima, maswahaba, Thuweiba, Mjombake Thuweiba, ami yake Mtume, Halima, Khadija,

wanawake wema, Maisara, Mariamu, Asya, Ibrahim, Abubakar, wafalme, mitume, manabii, Ibrahim, Musa, Ismail, Issa, Suleiman, mashahidi, kijana, mamake kijana, Maria Kibtiya, Ansar, Muhajirun, Fatuma na Hussein. Vilevile kuna wahusika wasio wa kawaida kama vile, Mwenyezi Mungu, viumbe wa mbinguni kama malaika: Jibrili, Munkar na mahurulaini. Kuna wahusika wanyama na vilevile miti ya mitende lakini wenye tabia na matendo ya kibinadamu. Hatimaye kuna wahusika wema na wabaya.

Kuna usawiri wa wahusika unaojitokeza katika vikundi viwili ambavyo vinakinzana kama ifuatavyo. Kuna mhusika mkuu ambaye ni Mtume Muhammad, ambaye anasaidiwa na Mwenyezi Mungu na malaika Jibrili. Vilevile kuna wahusika ambao ni Makureishi ambao baadhi yao hawaamini safari ya mbinguni ya Mtume na yote aliyopewa na Mwenyezi Mungu.

Kulingana na Wamitila (2002), wahusika ni viumbe wanaopatikana katika kazi yoyote ya kifasihi na huwa ni sehemu ya kazi nzima. Vilevile anadai kwamba, wahusika ni viumbe wanaopatikana ulimwenguni lakini si lazima sifa zote za mhusika zifungamane moja kwa moja na za binadamu na kulingana na kazi yetu, miti ya mitende, wanyama hali kadhalika milima imesawiriwa na kuchukua nafasi ya binadamu. Hali kadhalika, kuna wahusika ambao wamejitokeza kama maadui wa Mtume Muhammad (S.A.W) ambao wanatoka katika kabila la Mtume ambalo ni Kureishi kama vile Abujahali ambao aghalabu wanasaidiwa na shetani. Kila mhusika ana nafasi yake kama tulivyoeleza.

Kuna aina mbalimbali za wahusika kama walivyojitokeza katika kazi hii. Wahusika wakuu huhusishwa kutoka mwanzo hadi mwisho wa kazi yoyote ya kifasihi na hususan hujenga maudhui. Wahusika wasaidizi nao humjenga mhusika mkuu na huweza kuwa na visa vyao. Wahusika wadogo aghalabu hufanya kazi ndogo sana katika fasihi kama vile kujenga maudhui au mandhari. Wahusika hawa wakitolewa, kazi ya kifasihi inaweza kuendelea bila kubadilika sana. Wahusika bapa ni wale wenye kujenga tabia moja tu na ni wahusika wasiobadilika kutoka mwanzo hadi mwisho. Sifa zao huweza kutambulika mwanzoni mwa kazi za kifasihi na huwakilisha sifa halisia za binadamu. Hii inamaanisha kuwa mhusika mbaya anabakia kuwa mbaya kutoka mwanzo hadi mwisho.

Aristotle (1965), amesema ni lazima mhusika aonyeshe hali ya juu ya kimaadili. Katika karne zilizotangulia fasihi ilitazamwa katika misingi ya kimaadili ambayo ilipaswa kuwa ya hali ya juu na ilikuwa ni lazima mhusika apewe sifa zinazohusiana na kushikamana vizuri na matendo yake, lazima sifa zake zimtambulishe kama mhusika na awe kama binadamu kwa kuwa na uthabiti ulio bayana.

Senkoro (1982), amesema kuwa wahusika wa fasihi ni wa aina tatu kuu ambao ni wahusika wakuu, wahusika wadogo na wahusika bapa. Wahusika wakuu ni wale wanaojitokeza katika kazi za kifasihi tangu mwanzo hadi mwisho, maudhui ya kazi husika huwa yanamzungukia na hutegemea wao. Wahusika wadogo nao hujitokeza kwa uchache na huchangia katika kuikuza dhamira. Wahusika bapa huwa hawabadiliki na hawaonekani kuchukua hatua mbalimbali za mabadiliko katika maisha yao. Wanabaki kuwa wale wale katika kazi yote ya fasihi.

Kulingana na Forster (1927), wahusika wamegawanywa katika makundi mawili makuu, wahusika bapa na duara. Wahusika bapa huwa hawabadiliki tangu mwanzo hadi mwisho. Kuna aina mbili za wahusika bapa nao ni bapa sugu na bapa vielelezo. Bapa sugu ni wale ambao wanajulikana kutokana na maelezo ya mtunzi na jinsi wanavyoelezwa ni vilevile wanavyojitokeza katika kazi za kifasihi. Wahusika bapa vielelezo hawabadiliki na hupewa majina ambayo yanaafikiana na matendo yao na tabia zao. Majina ya wahusika hawa huwa kama kielelezo cha ufupisho wa wasifu wao.

Forster (1927), amesema kuwa wahusika duara hukaribiana na binadamu wa kawaida na mabadiliko yanayowatokea husababisha uduara wa hisia mbalimbali kama vile  kijamii, kisaikolojia n.k. Mhusika duara anamwakilisha binadamu halisi lakini wakati mwingine huzua sifa zisizolingana na binadamu wa kawaida. Tungo nyingi za kidini huwa na wahusika wenye sifa hizi haswa katika matendo yao.

## 2.5 MATUMIZI YA LUGHA

Kulingana na Wamitila (2008), lugha huundwa na msamiati na msamiati ni jumla ya maneno yanayopatikana katika lugha. Ni nyenzo ya kimsingi aliyo nayo mwandishi na ina nafasi na umuhimu mkubwa katika utunzi na uandishi wake.

Watunzi wa tungo kwa kawaida hupenda lugha ya kale. Kwa watunzi wengi wa Kiislamu na wa Kiarabu, Kiarabu ni lugha takatifu na kubadilisha maneno ya kale na ya kisasa ni kuvuruga lugha. Jambo hili huzifanya tungo nyingi zisieleweke kwa sababu watunzi hutumia istiara, tashbiha, jazanda alhasili lugha ya kitamathali ya zamani za giza. Maneno haya ni kulingana na Wamutiso (2005).

Kulingana na Senkoro (1982), matumizi ya lugha ndiyo mzizi wa kazi ya fasihi na mtunzi wa utungo wowote hutumia ili kuyaibusha mawazo yake na kuonyesha ukomavu katika kazi husika. Kwa hivyo mtunzi hutumia njia hii ili kufikisha ujumbe wake kwa hadhira lengwa.Kuna aina nyingi za matumizi ya lugha lakini katika utafiti wetu tumeshughulikia lahaja ya Kiamu, Kingozi na maneno ya Kiarabu.

### 2.5.1 LAHAJA YA KIAMU

Kulingana na Crystal (1997), lahaja ni mtindo bainifu wa lugha kieneo na kijamii unaobainishwa na seti maalumu za maneno na miundo ya kisarufi. Maelezo haya ni mwafaka katika kueleza lahaja lakini tatizo linatokea pale ambapo tunaelezwa kuwa lahaja ni mtindo. Maelezo haya hayalingani kwa sababu lahaja si ya kiuteuzi ilhali mtindo huteuliwa katika matumizi fulani.

TUKI (1990) imesema kuwa lahaja ni kitarafa cha lugha kinachobainika kijamii au kijiografia na kinachodhihirishwa na vipengele vya kisauti na kimuundo. Kulingana na Iribemwangi na Mukhwana (2011), lugha nyingi hugawika kutokana na masuala ya kijamii kama vile matabaka ya kiuchumi, hadhi ya kitaalamu, umri, jinsia, dini na mengineyo. Maswala haya ya kijamii hujitokeza na lahaja mbalimbali za kijamii. Katika kila lugha ni rahisi kutambua matumizi ya lugha katika viwango vya sarufi, msamiati na matamshi yanayojikita katika kundi fulani la kijamii.

Kulingana na Bakari (1982), lahaja za Kiswahili za pwani ya Kenya zinatofautiana kimofofonolojia. Bakari ameonyesha kwamba lahaja za kusini Uswahilini Kenya na ambazo ni Kivumba, Chichifundi, Kijomvu na Kimvita zinakaribiana kimofofonolojia kuliko zile za kaskazini ambazo ni Kiamu, Kisiu na Kitukuu.

### 2.5.2 KINGOZI

Kulingana na Massamba (2002), waswahili wana madai yao kuwa Kiswahili cha asili ni Kingozi na kulikuwa na Ngozi, Wangozi na Kingozi. Kulingana na Chiragdin katika Massaamba, watu hawa Wangozi walikuwa wakipima mashamba kwa kanda za ngozi. Kulingana na maelezo haya, Kingozi ni Kiswahili cha kale ambacho kilikuwa kikitumiwa katika mwambao wa Pwani. Lugha hii imetumika sana katika tungo za kale ikiwemo *Maulidi ya Nuni.*

### 2.5.3 LUGHA YA KIARABU

Lugha hii imefungamanishwa na Uislamu na maneno mengi hususan katika tungo za Kiislamu yametoholewa ili yasipoteze ule ujumbe uliodhamiriwa na pia kwa sababu Kiarabu ni lugha takatifu na ndiyo iliyotumiwa katika kitabu kitakatifu ambaacho ni Qur’an Tukufu ambayo kwa maoni ya Waislamu wote, haiwezi kutafsiriwa ila kutafsiriwa Kiislamu.

## 2.6 TAMATHALI ZA USEMI

Wamitila (2008), amesema tamathali za usemi hujumlisha sifa nyingi za kimtindo ambazo hutumiwa katika kazi za kifasihi. Tamathali za usemi hurejelea lugha na kuifanya iwe ya mvuto mkubwa, uelezaji wa kinachohusishwa na kazi husika. Tamathali za usemi hurejelea mbinu ambayo inahusisha maana kwa sababu kuna maana ambayo haiko wazi na ambayo msomaji anahitaji kuielewa.

Kulingana na Senkoro (1982), tamathali za usemi ni maneno, nahau au sentensi ambazo hutumiwa na wasanii wa fasihi ili kutia nguvu katika kazi husika kwa kupitisha ujumbe uliodhamiriwa. Ni njia mojawapo ya kuongeza utamu wa lugha kutokana na jinsi mtunzi anavyopitisha ujumbe wake kwa hadhira lengwa.

### 2.6.1 TAKRIRI

Kulingana na King’ei na Kemoli (2001), takriri ni marudio ya sauti fulani za vokali, konsonanti au maneno katika mistari ya utungo ili kuleta athari fulani katika akili ya msomaji au masikio ya msikilizaji kwa lengo la kuiteka nadhari ya hadhira.

Wamitila (2008) amesema kuwa takriri ni mbinu inayorejelea urudiaji au ukariri wa neno au sauti fulani. Kimsingi takriri ni sehemu ya urudiaji. Lengo kuu la mtunzi kutumia mbinu hii ni kusisitiza ujumbe aliodhamiria kwa hadhira lengwa.

### 2.6.2 TASHBIHI AU TASHBIHA

Senkoro (1982), amesema tashbihi au tashbiha ni tamathali ambayo watu au vitu viwili hulinganishwa na watu au vitu vigine kwa kutumia maneno kama, mithili ya, kama, kwamba n.k. Maelezo haya yanalingana na Wamitila (2008) na King'ei na Kemoli (2001).

### 2.6.3 ISTIARI

Wamitila (2008) amesema istiari ni tamathali ya ulinganishi wa bila ya kutumiwa maneno yanayoashiria ulinganishi kama 'ni' ja, mfano wa, mithili ya n.k. Kingei na Kemoli (2001) wamesema mbinu hii hutumiwa kufumba maana ili kutilia mkazo jambo linaloelezwa kama pambo la lugha. Vitu viwili hulinganishwa kwa kutumia neno 'ni'.

### 2.6.4 TASHIHISI

Senkoro (1982), amesema, hii ni mbinu ambayo vitu visivyo na sifa za kibinadamu hupewa sifa za kibinadamu. Maelezo haya yanalingana na ya King'ei na Kemoli (2001) ambao wamesema tashihisi pia huitwa uhuishaji na ni matumizi ya lugha ambapo vitu visivyokuwa na uhai vinaelezwa kana kwamba vina uhai.

### 2.6.5 CHUKU

Hii ni tamathali inayoeleza hali ya sifa za kitu kuelezwa kwa namna inayokuza sifa zake au kuzidunisha sifa hizo kuliko hali yake ya kawaida. Huwa pana ukinzani kati ya hali inayosemwa na ukweli wenyewe. Hii ni sifa ambayo inahusishwa kwa kiasi kikubwa na kinaya. Maelezo haya yamesemwa na Wamitila (2008).

### 2.6.6 TASWIRA AU JAZANDA

Ni mfano wa vielelezo vya kufikirika vinavyoundika akilini kutokana na maelezo fulani katika utungo. Mtunzi mara nyingi hutumia mbinu hii kutupa picha kamili za kimawazo za yale anayoyasimulia. Picha hizi hufafanua tukio, hali fulani ya mhusika au kisa fulani. King'ei na Kemoli (2001).

Wamitila (2008), amesema jazanda ni neno ambalo hutumiwa kurejelea ile hali ya kutumia picha au taswira katika kazi ya kifasihi. Jazanda hutokana na matumizi ya lugha, maelezo ya msimulizi au mtunzi. Kuna aina mbili za jazanda ambazo ni jazanda za kimaelezi na jazanda za kiishara. Jazanda ya kimaelezi huundwa kutokana na maelezo ya msimulizi na jazanda za kiishara huunda picha katika akili ya msomaji lakini taswira au picha hizo huwa na maana nyengine za ziada. Hizi ni taswira ambazo kimsingi zinafanya kazi ya ishara na msomaji au mhakiki anatakiwa kuzihusisha taswira zenyewe na utungo mzima ili apate ujumbe unaokusudiwa.

## 2.7 UHURU WA MTUNZI

Kulingana na King'ei na Kemoli (2001) uhuru wa mtunzi ni kibali walichonacho watunzi wa tungo kutumia mtindo, msamiati au mpangilio wa lugha kisanaa bila kukiuka misingi ya lugha kwa lengo la kuujenga utungo husika. Katika mbinu hii mtunzi ana uhuru wa kutumia mbinu zingine zinazotumiwa katika fani kama vile lugha ya mkato, kurefusha maneno, kufupisha maneno n.k.

### 2.7.1 INKISARI

Inkisari ni uhuru wa kufupisha baadhi ya maneno kwa kupunguza mizani. Mbinu za kufupisha maneno ni kama vile kutotumia viwakilishi vya nafsi na virejeleo vya majina k.m ninalisoma inakuwa nasoma, kubadilisha muundo wa vitenzi k.m aliyekupa inakuwa alokupa, kubadilisha tahajia ya baadhi ya maneno k.m taabu inakuwa tabu n.k. Maelezo haya ni kulingana na King'ei na Kemoli (2001).

### 2.7.2 MAZIDA

Katika mbinu hii, mtunzi hurefusha mizani ili kutosheleza urari wa mizani katika mshororo. Mtunzi hufanya hivyo kwa madhumuni ya kusawazisha mizani ya mishororo yote katika mizani.

### 2.7.3 TABDILA

Mbinu hii hutumiwa kubadilisha tahajia za maneno au mtunzi hubadilisha sauti fulani katika neno ili kuleta uwiano fulani bila kupunguza wala kuzidisha mizani kwa lengo la kupata vina.

## 2.8 MUUNDO

King'ei na Kemoli (2001) wamesema muundo hutumiwa kueleza sura ya nje na ya ndani ya utungo kama inavyoonekana au kusikika kutokana na midundo ya mapigo yake.

Mbatiah (2001), ameeleza muundo kuwa ni uhusiano wa elementi za kazi ya kifasihi katika mpangilio thabiti unaoshikamanisha elementi hizo. Maelezo ya Mbatiah yanalingana na ya Wamitila (2003) ambaye amesema kuwa muundo hutumiwa kuelezea sifa za nje zinazoipa kazi ya kifasihi sura ya kutambulikana. Hata hivyo si lazima elementi za kimuundo ziweze kuonekana kijuujuu kwani baadhi ya elementi hizi huwa za kindani. Kutokana na sababu hii, sharti hadhira isome kazi husika ili kuelewa elementi hizo. Hali hii husababisha kuwepo kwa aina mbili kuu za muundo nazo ni muundo wa nje na muundo wa ndani.

## 2.9 UMBO LA UTUNGO

Wamitila (2008) amefafanua umbo la utungo kuwa ni sura ya utungo husika na jinsi unavyoonekana. Kulingana na dhana hii, msingi wa mizani umetumiwa ili kuanisha idadi ya mizani katika kila ubeti.

## 2.10 MANDHARI AU MAHALI

Kulingana na Wamitila (2008), mandhari hurejelea wakati na mazingira ya kijiografia ambayo yanakuwa msingi muhimu katika kazi za kifasihi. Mandhari huwa nguzo muhimu ya uhusika pale ambapo matendo ya wahusika yanafungamana na mazingira wanamojikuta. Katika baadhi ya kazi za kifasihi, mhusika anaweza kuwekwa wazi ambapo inadhihirika sana na mandhari.

Uhusiano unaotokea baina ya wahusika na mandhari unaweza ukawa wa kimapatano au wa kiknzani. Kuna mandhari aina mbalimbali kama vile mandhari ya kijiografia ambayo inasisitiza uhusiano wa karibu kati ya ulimwengu wa kibunifu na ulimwengu halisi kwa kuifanya hadhira kuamini kuwa matukio, mazingira na maingiliano ya wahusika yanayotokea katika ulimwengu huo wa kibunifu yanaweza kukubalika. Mandhari ya kiishara hutumiwa kwa namna ambayo inayafanya kuwa aina fulani ya ishara, mandhari ya kidhanifu hayawezi kuhusishwa na uhalisi, mandhari ya kidokezi huishia kuwa ishara ya udokezaji katika kazi inayohusika, nayo mandhari ya kiajinabi huonekana kama kitu kigeni ambacho kina sifa zinazokiuka matarajio ya kawaida uliozoeleka (Wamitila 2008).

Gill (1985) amesema kuwa mandhari ni neno pana linalojumlisha mahali ambapo wahusika wamewasilishwa katika muktadha wa kijamii. Wahusika kama vile familia, marafiki, matabaka, tamaduni, imani na kaida za jamii kitabia. Mandhari huchangia katika kueleza mengi kuhusu sifa na tabia za wahusika, hali waliyomo na hata husaidia katika kutambua maudhui yaliyo katika kazi ya kifasihi.

Wamutiso (2005) amefafanua mandhari kuwa mazingira ya utendaji au usimulizi katika kazi za kifasihi. Anaendelea kusema kuwa mandhari ni pale ambapo matukio yanayosimuliwa hutokea. Mtunzi hurejelea mandhari mbalimbali kama vile ya kijiografia, ya kinyumbani n.k.

## 2.11 HITIMISHO

Katika sura hii, tumeelezea dhana za kimsingi zinazofungamana na utafiti wetu. Tumeanza kwa kutoa muhtasari kuhusu *Maulidi ya Nuni*. Tumepiga hatua kwa kueleza dhana ya uhusika na wahusika kulingana na maoni ya wataalamu mbalimbali. Tumepata kuwa uhusika ni umithilishaji wa vitendo vya viumbe katika kazi za kifasihi nao wahusika ni viumbe wanaopatikana katika kazi za kifasihi. Baadhi ya aina ya wahusika tuliyowaangazia ni kama vile wahusika wakuu, wahusika wadogo, wahusika wa kawaida na wahusika wasiokuwa wa kawaida, wahusika wasaidizi, wahusika bapa n.k. Pia tumeshughulikia dhana nyingine za fani kama vile matumizi ya lugha kwa kugusia lahaja ya Kiamu, Kingozi na lugha ya Kiarabu. Tumeeleza dhana ya tamathali za usemi kwa ujumla na vilevile kutoa maelezo kuhusu takriri, tashbihi, istiari, tashihisi, chuku pamoja na taswira au jazanda. Tumeangazia uhuru wa mtunzi na tumeangalia inkisari, mazida na tabdila. Dhana ya muundo imeshughulikiwa kupitia maelezo kuhusu umbo la utungo. Tumemalizia kwa kutoa maelezo kuhusu mandhari au mahali kwa kueleza kuwa mandhari au mahali hurejelea wakati na mazingira ya kijiografia ambayo yanakuwa msingi muhimu katika kazi za kifasihi.

## SURA YA TATU

### 3.1 NAFASI YA WAHUSIKA NA UHUSIKA KATIKA MAULIDI YA NUNI

### 3.2 UTANGULIZI

Katika sura ya pili tumeangazia maoni ya wataalamu mbalimbali kuhusu dhana ya wahusika na uhusika katika mawanda ya kifasihi. Kulingana na maelezo tuliyoyatoa, uhusika ni umithilishaji wa vitendo vya viumbe katika kazi za kifasihi nao wahusika ni viumbe wanaopatikana katika kazi yoyote ya kifasihi. Pia tumepata maelezo kuhusu aina mbalimbali za wahusika kama tulivyoeleza katika sura ya pili.

Katika utafiti wetu, wahusika pamoja na uhusika wao wamejitokeza kwa aina tofauti tofauti kama vile wahusika wasiokuwa binadamu na wahusika binadamu, pia wameweza kujitokeza kama wahusika wakuu, wahusika wasaidizi na vilevile wahusika wadogo. Wahusika pamoja na uhusika wao umejitokeza kupitia sifa zao kama zinavyojitokeza katika utungo huu.

Wahusika ambao wamejitokeza katika utungo huu ni pamoja na Mwenyezi Mungu, Mtume Muhammad (S.A.W), Jibril, Munkar, Malaika wengine, wanawake kwa jumla kama vile Amina, Thuweiba, Halima, Mariyamu binti Imrani, Mwana Asiya, Khadija, Maria Kibtiya, Wanawake wema, wanaume kwa jumla kama vile Abdalla, Abdulmuttalib, Abutalib, Mjombake Thuweiba, Abubakar, Mitume, watoto wa Mtume Muhammad (S.A.W), Mahurulaini, Maswahaba, Muhajirun na Ansar, wanyama, miti ya mitende na majabali pamoja na wahusika wengine.

Wahusika katika utungo huu wamesawiriwa katika mawanda ya dini ya Kiislamu kwa hivyo hatukuweza kutoa maoni kulingana na wataalamu wa kifasihi bali tumejikita katika utungo wenyewe na vitabu vya dini ya Kiislamu kama vile Qur’ani Tukufu na vitabu vyengine vya dini ya Kiisilamu vilivyotupa mwongozo thabiti katika kutalii suala la wahusika na uhusika katika *Maulidi ya Nuni.*

### 3.3 MWENYEZI  MUNGU

Mwenyezi Mungu (S.W.T.) anasawiriwa kama mhusika asiyekuwa wa kawaida na pia mhusika mkuu na kulingana na *Maulidi ya Nuni*, Mwenyezi Mungu ana majina tisini na tisa ambayo yanafafanua utukufu wake. Yeye ndie ajuaye yote, ya siri na ya dhahiri, yaliyopita na

yajayo, na vilevile yeye ni mkwasi na viumbe vyote vilivyomo ardhini na mbinguni ni wenye kumtegemea yeye na marejeo bila shaka ni kwake. Katika ubeti wa 17, Mtunzi anasema:

Kisa asma u li husuna isome pia
Jalla jalalahu usiwate kuliswifia
na kulla isimu utayapo na hilo taya
ndio adabuye la kutaya la Mungu yina

Ubeti huu umetupa maelezo kuhusu Mwenyezi Mungu kuwa, katika kila tendo jema ni muhimu kumtaja Mwenyezi Mungu kupitia majina yake mazuri tisini na tisa. Mtunzi wa utungo huu anatupa taswira kwamba ni muhimu katika kisomo hiki cha maulidi kianze kwa kumtaja na kumsifu Mola Mtukufu. Katika ubeti wa 22 na 23 Mtunzi anaendelea kusema:

Nandeleza mbele kukuswifu muabudiwa
nitamusha nami nitamuke tamu zenewa
ulimi fasiha ushukuru zako zipawa
kwa umezotupa zipawazo dini wa duna

Naomba kwa Mungu zitukufu zipawa zake
zenyi taadhimu rehemaze zimiminike
salamu ya radhi radhi yake izifunike
sala na salamu na radhiyo zimetangana

Maelezo haya yametupa undani zaidi kuhusu Mwenyezi Mungu ambapo yeye ndiye mweza wa kila kitu kilichoko ardhini na mbinguni. Mtunzi anasema ni muhimu kutanguliza na kuendeleza kumtaja, kumsifu na kumshukuru Mwenyezi Mungu katika hali zote ili kisomo cha maulidi kikubaliwe. Vilevile ni muhimu kuzingatia na kutumia majina yake matukufu ili kupatikane rehema na radhi zake Maulana. Aghalabu kukosekana kwa radhi na rehema zake Mwenyezi Mungu kunaweza kusababisha balaa mbalimbali ikiwemo kukosekana kwa utulivu na amani.

Maelezo haya yamelingana na Qur’ani Tukufu. Katika Qur’ani 57 aya ya 1-6, Mwenyezi Mungu anasema kila kilichomo mbinguni na ardhini kinamtaja na kumtukuza yeye, na yeye ndiye aliye juu, mkubwa, muadilifu. Ni yeye aliyeumba uhai na mauti na ni mwenye nguvu katika vyote alivyoviumba. Yeye ni wa mwanzo na wa mwisho, anayajua yote ya siri na ya dhahiri na ana siri ya vyote vilivyomo mbinguni na ardhini. Mola Mtukufu anaendelea kusema kwamba; yeye ndiye aliyeumba mbingu na ardhi kwa siku sita na yuko katika arshi tukufu na anayajua yote yaingiayo na yatokayo ardhini pamoja na malengo ya yote haya. Vilevile yuko na viumbe wake popote walipo na anayaona yote yafanywayo na viumbe hawa.

Ndiye mmiliki wa mbingu na ardhi na yote yanarudi kwake. Ni yeye Mwenyezi Mungu ambaye hubadilisha usiku kuwa mchana na mchana kuwa usiku na ana siri za nafsi zote.

Kulingana na ubeti wa 83 hadi 85, Mwenyezi Mungu huishi katika uwingu wa saba ambako Mtume (S.A.W) alifika huko na kupewa nguzo muhimu ya swala ambayo ni ya pili katika nguzo tano za Uislamu. Pia aliweza kuonyeshwa malipo na adhabu zitakazowakabili wafuasi wake kulingana na matendo yao hapa ulimwenguni. Wema watalipwa mema na miongoni mwao ni kulipwa wanachotamani ikiwemo vinywaji, matunda n.k. na mahali pema pasipokuwa na maudhi ya aina yoyote. Maelezo haya yanashabihiana na Qur'ani Tukufu 67 aya ya 1-3, ambapo Mwenyezi Mungu anatueleza yeye ndiye aliyeumba mbingu na ardhi ili kukujaribuni ni yupi aliye mbora katika vitendo na yeye ndiye aliye juu na msamehevu na aliyeumba mbingu saba moja juu ya nyengine.

Vilevile ni kupitia kwa Mwenyezi Mungu ambapo safari ya Mtume (S.A.W.) ilitekelezwa kutoka uwingu wa kwanza hadi wa saba akishirikishwa na Malaika Jibrili (Ubeti wa 80 hadi 85). Kulingana na utungo huu, Mwenyezi Mungu vilevile anachukua nafasi ya kuwa mhusika mkuu kwa kukamilisha lengo la mazazi ya Mtume kufikia kupewa wahyi, hali kadhalika safari yake ya kwenda hadi uwingu wa saba kwenda kutukuzwa na vilevile kupewa nguzo muhimu ya swala. Mtunzi anasema:

> Akakurubishwa kamuona Mola Jalali
> kuruba maana urefuwe ni nyuta mbili
> ushikapo una kwa mkono uso wa pili
> dhati ya Moliwa kaiona kwa muayana

Mwenyezi Mungu ni mhusika mwenye sifa za kipekee ambazo zinajitokeza katika utungo huu. Awali mwa utungo huu, tunaambiwa Maulidi haya yanaanza na utajo wake Mwenyezi Mungu kuonyesha kwamba kuweko kwa kila kitu na kustawi kwa dunia yote kunamtegemea yeye na hakuna lolote linaloweza kufanyika au kutokea isipokuwa kupitia kwake.

Pia tumeelezwa kwamba yeye ni mkarimu na ndiye mwenye kutoa rehema, heri na neema kwa waja wake bila hitilafu au mapendeleo. Sifa hii muhimu inajitokeza katika utungo wakati mtunzi anapotuelezea kuhusu mazazi ya Mtume (S.AW.) jinsi yalivyokuwa hadi kuzaliwa kwake, kukua kwake na kupelekwa katika safari ya mbinguni ambayo ilichukuwa usiku mmoja pekee. Licha ya kuwa ilikuwa safari ya usiku mmoja Mtume (S.A.W.) aliweza

kuonyeshwa mambo mengi ambayo walioelezewa hawakuweza kuamini na miongoni mwao wakiwa jamaa zake wa karibu sana akiwemo Abu Jahal. Hizi zote ni neema ambazo zilitimizwa kupitia kwa ukarimu wa Mola Mtukufu.

Sifa nyengine ya Mwenyezi Mungu ni kuwa yeye ni mchungaji wa imani na huweka imani yake ndani ya mioyo ya waja wake; huwalinda wenye kujilinda kwake na huwapa waja wake utulivu. Sifa hii muhimu imejitokeza wakati Abubakar alipomuamini Mtume (S.A.W.) lakini Makureishi wa Makka hawakumuamini baada ya Mtume (S.A.W.) kuwaeleza kuhusu safari yake ya usiku mmoja mbinguni na kuonyeshwa matukio mbalimbali na baadaye kukabidhiwa nguzo ya swala na Mwenyezi Mungu. Kama Mwenyezi Mungu hangeweka imani ndani ya moyo wa Abubakari na kumfanya kuwa miongoni mwa waumini wa mwanzo kukubali aliyoyaeleza Mtume (S.A.W.), pengine ingekuwa mwanzo wa kusambaratika kwa wafuasi wa Mtume (S.A.W.). lakini kupitia kwa Abubakar, Mtume (S.A.W) aliweza kupata motisha na kuendeleza dini ya Kiislamu.

Mwenyezi Mungu vilevile ni mwenye nguvu na hakuna mwenye kumshinda. Ni ajabu kwamba safari ya Mtume (S.A.W.) ilitekelezwa kupitia kwa mnyama Buraqi ambaye alikuwa pamoja na Malaika Jibrili kutekeleza safari hii tukufu hadi uwingu wa saba na kukabidhiwa mambo muhimu ya dini ya Kiislamu ikiwemo kuonyeshwa moto na pepo na adhabu na starehe mbalimbali watakazopata wafuasi wa Mtume (S.A.W.) kupitia matendo yao maovu au mema. Vilevile kupitia kwa nguvu zake Mwenyezi Mungu, aliweza kuwakusanya viumbe wengine kama malaika, mitume, manabii n.k na kumfanya Mtume (S.A.W.) kuwaongoza katika swala katika msikiti wa Makdisi mjini Jerusalam kabla ya kupanda kwenye uwingu wa kwanza.

Kulingana na utungo huu, Mwenyezi Mungu ana sifa ya kuwa mjuzi na mwenye kujua mambo yote ya siri na ya dhahiri. Ni ajabu kwamba mimba ya Mtume (S.A.W.) ilijulikana mpaka na wanyama wa Makureishi pamoja na malaika wa mbinguni. Vilevile katika safari za Mtume (S.A.W.) za kibiashara alipokuwa na ami yake, malaika waliweza kumfinika na mbawa zake ili asipate jua. Mambo yote haya tayari yalikuwa yashajulikana na Mwenyezi Mungu ambaye baadaye anamfanya kuwa mtu mtukufu duniani na ahera.

### 3.4 MTUME MUHAMMAD (S.A.W.)

Mhusika huyu anachukua nafasi ya kuwa mhusika mkuu na pia mhusika wa kawaida na uhusika wake unakamilisha malengo ya kuletwa kwake duniani ambapo ni kukamilisha yaliyotangulizwa na mitume waliotangulia na yeye kuwa wa mwisho kwa kukamilisha dini ya Kiislamu. Mtume Muhammad (S.A.W.) anasawiriwa na kuchukua nafasi ya kuwa Jagina kwa sababu mimba yake ilikuwa ya maajabu, kukua kwake kwa maajabu, safari yake ya kwenda mbinguni ilikuwa ya kimaajabu, maisha yake vilevile yalikuwa ya kimaajabu na alipata misukosuko mingi katika kuweka misingi thabiti ya dini ya Kiislamu na alipigwa vita hata na jamaa zake wa karibu zaidi akiwemo ami yake Abu Jahal na Makureishi wengine. Yeye ni mwana wa Abdalla na Amina.

Katika beti za awali, mtunzi anatueleza habari kuwa katika ibada mwanzo ni kumtaja Mwenyezi Mungu kupitia kwa Qur'ani Tukufu ikitangulizwa na Suratul Fatiha na hatimaye sala za Mtume (S.A.W) na salamu kwa Maulana. Mtunzi anatupa maelezo yafuatayo:

Kwanda kwa ibada ni kusoma kwa Kuruani
maneno ya Mungu tangulizi ni Fatihani
kabula kuswifu yakasomwe kwa hadharani
sala za Mtumi na salamu za Maulana ( ubeti wa 2 )

Maelezo haya yanatupa undani kuhusu mhusika huyu kuwa katika kila ibada ni muhimu kutaja jina lake. Katika kutekeleza nguzo mojawapo na muhimu ya Uislamu ambayo ni swala na hutekelezwa mara tano kwa siku katika vipindi maalum ambavyo ni alfajiri, adhuhuri, alasiri, magharibi na isha. Swala hizi hazikubaliwi na Mwenyezi Mungu pasipo kutajwa kwa jina la Mtume (S.A.W.) ambalo limo katika dua maalumu. Katika kila maombi ambayo Muislamu humuomba Mwenyezi Mungu, huwa hayakubaliwi pasipo kumswalia Mtume (S.A.W.), na hata malaika mbinguni humswalia na kumtukuza. Kulingana na mafunzo ya Kiislamu, ukimswalia Mtume (S.A.W.) mara nyingi utapata utulivu na Mwenyezi Mungu atakutatulia shida zako.

Mtume Muhammad (S.A.W.) ametukuzwa na Mwenyezi Mungu ambaye katika kitabu chake Qur'ani Tukufu kuna sura ambayo imeitwa kwa jina lake ambayo ni Suratul Muhammad. Katika Qur'an 47 aya ya 2, Mwenyezi Mungu anasema “Wale ambao wanaamini na kutenda vitendo vyema na kuamini aliyoteremshiwa Mtume Muhammad (S.A.W.) ambayo ni ya kweli kutoka kwa Mwenyezi Mungu atawaondoshea kila madhila na atainua maisha yao.”

Maelezo haya pia yanadhihirisha cheo cha Mtume (S.A.W.) kwa Mwenyezi Mungu na pia wafuasi wake. Kulingana na utungo huu, Mtume (S.A.W.) alitukuzwa kwa kupewa nguzo ya swala katika safari yake mbinguni na alipewa kitabu cha mwisho ambacho ni Qur'ani Tukufu. Alitukuzwa na kuwa Mtume wa mwisho na yeye atapewa nafasi na Mwenyezi Mungu kuwaombea shufaa wafuasi wake siku ambayo hakutakuwa na mtetezi, nayo ni ile siku ya malipo.

Mtunzi ameendelea kusema kwamba ameamua kutafsiri maulidi haya katika lahaja ya Kiamu ili wengine wapate kuzijua na kuzielewa sifa za Mtume (S.A.W.). Katika ubeti wa 4, mtunzi anasema Mtume (S.A.W.) ni nuru kwani ni kupitia kwake ambapo aliweza kuweka msingi thabiti wa dini ya Kiislamu kwa kutoa mwongozo thabiti ambao uliweza kufuatwa na wafuasi wake hadi wakati wa sasa. Kabla ya mhusika huyu kupewa utume, kulikuwa na kipindi cha ujahiliya ambapo mambo mengi maovu yalisheheni hususani katika sehemu ya Uarabuni ikiwemo kuabudu masanamu, kuzikwa kwa watoto wa kike wakiwa hai, ulevi, uzinzi n.k. Kuja kwa Mtume (S.A.W.) kulichangia pakubwa katika kusitisha maovu haya yote.

Mazazi ya Mtume vilevile yalikuwa yenye miujiza sihaba. Katika ubeti wa 41 na 56 mtunzi amesema ujauzito wa Mtume (S.A.W.) ulikuwa umejulikana na viumbe kadhaa wakiwemo wanyama, malaika, binadamu n.k. jambo hili linadhihirisha kuwa Mtume Muhammad (S.A.W.) alikuwa kipenzi cha Mwenyezi Mungu na alikuwa amechaguliwa hata kabla hajaletwa ulimwenguni. Mazazi yake pia yalihudhuriwa na malaika watukufu waliokuwa wanamuombea kwa Mwenyezi Mungu kudhihirisha utukufu wake. Kukua kwake pia kulikuwa na miujiza mingi na baadhi yake ni kupatikana kwa baraka nyingi kwa mnyonyeshaji wake Halima ambaye mbuzi wake ambao hawakuwa na maziwa walipata maziwa mengi. Mbali na maelezo haya, mitume na manabii wa Mola Mtukufu waliomtangulia walibashiri na kuhubiri kuja kwake kwa wafuasi wao. Maelezo haya yanathibitisha kwamba Mtume Muhammad (S.A.W.) ndiye wa mwisho na dini ya Uislamu ndiyo ya walimwengu wote. Vilevile tunaelezewa kwamba kuja kwa Mtume (S.A.W.) ulimwenguni ni bahati kubwa sana kwa walimwengu wote ikizingatiwa sheria zote alizopewa Mtume (S.A.W.) zilikuwa mwangaza ambao uliongoza wafuasi ambao walikuwa wamezama katika maovu chungu nzima kama ulevi, kamari, uzinzi n.k.

Baada ya kuzaliwa, babu yake alifurahi sana na vilevile kumshukuru Mungu na hatimaye alimchukua na kumpeleka kwenye Kaaba na kumuombea ili akue na siha njema. Inaitakidiwa kwamba maombi haya yalikubaliwa kwa sababu tunaelezwa kwamba, uso wa Mtume uling'aa kama mwezi na vilevile alifunikwa na furaha kama kanzu iliyong'aa ambazo zilikuwa dalili za kuwa mtu mtukufu katika maisha yake. Mtunzi katika ubeti wa 59 anasema:

Kamtia Tumwa kaabani kimuombea
akamulindiye kwa baiti na baa pia
hasidi baghidi muyukuwe ngwamuondolea
akue kwa siha na afiya wake kijana

Kukua kwa Mtume nako kulikuwa na miujiza vilevile kwani kuliwastaajabisha wengi na kwa siku moja kulikuwa kama mwezi na baada ya miezi mitatu, alishika guu na katika mwezi wa tano alianza kutembea na mwezi wa tisa, alianza kuzungumza kwa ufasaha ambapo waliokuwa wamempita umri hawakuweza kujibu aliyoyatamka (ubeti wa 62 hadi 68). Maelezo haya yanthibitisha kuwa Mtume (S.A.W.) alikuwa jagina katika Uislamu kutokana na maajabu tofauti tofauti yaliyotokea kwake kama tulivyoeleza. Vilevile alikuwa akiandamana na malaika ambao walimkinga na mbawa zao kutokana na miale ya jua. Maelezo haya yanatosha kusadikisha kuwa Mtume Muhammad (S.A.W.) alichaguliwa kuanzia awali ndiposa aliepushwa na kila balaa na madhara ya ulimwengu huu.

Ndoa ya Mtume (S.A.W.) hali kadhalika haijaachwa nyuma, tunaelezwa kwamba pindi uposi wa Khadija ulipojiri, Mtume (S.A.W.) aliwajulisha ami zake upande wa baba na hatimaye waliridhika na uposi huo. Hadija alimzalia wana sita, waume kwa wake ambao ni: Kassim, Abdalla, Zeinab, Rukayya, Ummu Kulthum na Fatima. Maria Kibtiya naye alimzalia mwana mmoja ajulikanaye kama Ibrahim ambaye pia alilelewa na Khadija. Mtunzi anatueleza katika ubeti wa 74 na 75:

Kwa mezokusanya za nasabu ya Kureshia
na mali na dini na uzuri mezoutia
na kwa kulla mtu kama haya hujazengea
ona na jamaa mashujaa wa muawana

Akazaa naye wana wote waume wake
ila kwa ambao li Halili ni simu yake
huyu mbwa Mariya Kibutiya ndiye mamake
illa hawa sita alozaa ni huyu nana

Kwa Mtume mwanzo wa wahyi ulikuwa kupitia kwa ndoto za ukweli ambapo alionyeshwa kila kitu kwa uwazi. Haikuwa rahisi kwani mwanzoni aliingiwa na hofu nyingi lakini hatimaye alizoea. Aliteremshiwa wahyi ili awe rehema na baraka kwa viumbe wote waliomo ardhini na mbinguni ili wapate kumtii na vilevile alifunzwa ili aweze kukabiliana na wale watakaoipinga dini. Mtunzi anatupa maelezo haya katika ubeti wa 78 anaposema:

Akampekea kwa ziumbe ile rehema
wamtii wote wa tiati na walo sama
mwando wa dunia wamukiri hatta kiyama
kafunda na hoja za kushinda takoshindana

Hatimaye Mtume (S.A.W.) aliingia msikiti wa Makdisi alipokuwa anakwenda kuonana na Mola Mtukufu wakati wa usiku na ni mahala hapa ambapo aliwakusanya mitume, manabii, malaika, maruhani pamoja na majini. Kufikia nukta hii, Mtume aliwaongoza wote hawa katika swala. Tukio hili linadhihirisha kuwa Mtume (S.A.W.) alikuwa mcha Mungu na alitekeleza amri ya Mwenyezi Mungu kama alivyotakikana kufanya.

Baadaye alifupisha swala na kupanda ngazi iliyojaa nakshi nakshi au miiraji kuelekea uwingu wa saba ambako alitukuzwa na Mwenyezi Mungu. Alipitia uwingu mmoja hadi mwingine huku akionyeshwa mambo mbalimabali na adhabu mbalimbali zilizowakabili na zitakazowakabili wafuasi wake iwapo hawatafuata amri za Mwenyezi Mungu. Matukio yote haya yanaonyesha kuwa Mtume (S.A.W.) alikuwa mtiifu na alitii na kufuata yote aliyoambiwa kufanya na aliyoelezewa na Mwenyezi Mungu kupitia kwa Jibrili.

Mtume (S.A.W.) alikuwa mwenye huruma kwani baada ya kukabidhiwa nguzo ya swala ambazo idadi yake ilikuwa kuswali swala hamsini kwa siku kwa wafuasi wake, alirudi mara kadhaa kwa Mola Mtukufu na kumuomba azipunguze swala hizi kwani aliwaonea huruma wafuasi wake na alichelea kwamba kwa wingi wa swala hizi ingekuwa vigumu kwao kutekeleza ibada hii. Baada ya kurudi mara kadhaa kwa Mola Mtukufu, swala hizi zilipunguzwa kidogo kidogo hadi kufikia swala tano kwa siku, lakini malipo yake ni sawa na kutekeleza swala hamsini kwa siku.

Mtume ni kiongozi bora na anashinda viumbe wengine kwa sura, umbo na tabia. Maelezo haya yanathibitisha kauli kuwa maswahaba walitosheka na kufuata walioelezewa na Mtume

(S.A.W.) kwa sababu alikuwa kielelezo chema katika hali zote. Yeye vilevile ni bwana wa mabwana kwa wanadamu na viumbe vyote. Katika safari yake mbinguni Mwenyezi Mungu alimweleza Mtume (S.A.W.) kwamba yeye ndiye Mtume wa mwisho na hivyo anakamilisha yote yaliyotangulizwa na mitume wengine, vilevile kitabu cha Qur'ani ndicho cha mwisho na kinakamilisha yote yaliyomo katika vitabu vitakatifu vilivyotangulia na pia Mtume (S.A.W.) atapewa nafasi na Mola siku ya kiyama kuwaombea shufaa wafuasi wake. Maelezo haya yanathibitishwa katika ubeti wa 105 wakati mtunzi anaposema:

Laula ya Tumwa hangaliko tumwa Adamu
Wala li Halili wala Isa wala Kalimu
Wala Sulemani mulukuwe hunu adhimu
ni sababu yake kuumbiwa ni Subuhana

Miongoni mwa waliomsifu tabia zake walidhani kwamba yeye yuko sawa na viumbe wengine kwa vile alikuwa kiumbe mnyenyekevu na mwenye haya. Maelezo haya yanathibitisha kuwa Mtume (S.A.W.) licha ya kutukuzwa na Mola si mtu aliyekuwa akijiona ni mkuu na mtukufu bali aliishi maisha ya kawaida yakiwemo kushona nguo zake zilipokuwa zinahitaji viraka japokuwa alikuwa Mtume. Maelezo haya yanathibitishwa katika ubeti wa 96 pale mtunzi anaposema;

Ali mungi mno maulana kunyenyekea
alikwenda mno umbo lake kuwa na haya
hwandika zipaku penyi tundu ikitokea
na ikipasuka nguo yake alikishona.

Vilevile mtunzi anaendelea kutupa maelezo zaidi katika ubeti wa 49, 52, 53, 58, 89, 90, 91, 92, 93,94, 97, 103, 104, na 105.

Alikuwa kiumbe mnyeyekevu na viumbe wengine wote walikuwa wakimheshimu Mtume (S.A.W.) wakiwemo wafalme ambao licha ya kuwa walimuogopa kwa sababu ya hadhi yake kwa vile hakujali nguvu pamoja na mali zao, yeye hakuwaonyesha cheo chake kutokana na vile alivyokuwa akiishi. Katika ubeti wa 97 mtunzi anasema:

Wallahi muluki wameyaza nyoyoni mwao
utisho wa Tumwa wamemcha kama bwanao
yeye hawajali wafalume na nguvu zao
wangawa na mali kama taka hakuyaona

Kwa upande mwengine, milima ya Makka vilevile ilimtambua na ikasema kwamba itabadilika iwe dhahabu ili atajirike lakini alikataa akisisitiza kwamba lengo lake lilikuwa ni Janna ya Mola Mtukufu. Maelezo haya yanathibitisha kwamba Mtume Muhammad (S.A.W.) hakuwa na tamaa ya mali ya kidunia. Mtunzi katika ubeti wa 97 anasema:

Wallahi muluki wameyaza nyoyoni mwao
utisho wa Tumwa wamemcha kama bwanao
yeye hawajali wafalume na nguvu zao
wangawa na mali kama taka hakuyaona

## 3.5 JIBRIL

Jibril (A.S.) ni kiumbe cha Mola Mtukufu ambaye anachukua nafasi ya mhusika msaidizi kwa sababu anamkuza mhusika mkuu. Ni mtumishi wa Mola Mtukufu na kazi yake kuu ilikuwa ni kupeleka wahyi kutoka kwa Mola na kumfikishia Mtume (S.A.W.). Kiumbe huyu huishi mbinguni, si wa kawaida na ana nafasi muhimu katika kufanikisha *Maulidi ya Nuni*.

Katika ubeti wa 77 mtunzi anatueleza jinsi mhusika huyu alivyopeleka wahyi kwa Mtume (S.A.W) ambapo alimwambia asome kwa jina la Mwenyezi Mungu ambaye amemuumba mwanadamu kutokana na pande la damu. Mtume (S.A.W.) hakujua kusoma lakini kupitia kwa rehema za Mola aliweza na hapa ndipo mwanzo wa kuteremshwa wahyi ulipoanza. Maelezo haya vilevile yanasadifiana na Qur'an 96. Maelezo haya yanaonyesha kuwa mhusika huyu ni mtiifu kwani anatii na kutekeleza jinsi alivyoagizwa na Mola kwa kufikisha ujumbe kwa Mtume (S.A.W.) bila hiana.

Pindi Mtume (S.A.W.) alipozaliwa, alikuwa ni mwenye kulia na alipochemua, miongoni mwa malaika waliomtilia baraka alikuwa ni Jibrili na Mola Mtukufu alipomtukuza, Jibrili vilevile alikuwa anarudiarudia maneno hayo. Wakati Mtume alipokuwa anarudi kutoka safari akiwa katika msafara wake, Jibrili alikuwa miongoni mwa malaika waliomhifadhi na kumkinga ili asipate miale ya jua (ubeti wa 56 na 70). Maelezo haya yanatosha kuthibitisha kuwa mhusika huyu ni mwaminifu kiasi kwamba anatumwa na Mola na anafikisha yote aliyoambiwa afanye.

Kulingana na ubeti wa 82, Jibrili alikuwa miongoni mwa viumbe waliojumuika katika swala iliyoongozwa na Mtume (S.A.W.) katika msikiti wa Baitul Mukadasi kabla ya safari ya

kwenda mbinguni kuanza. Tukio hili linadhihirisha kuwa mhusika huyu alikuwa ni mcha Mungu. Mtunzi anasema:

Kamtanguliza Jiburili Mtume wetu
kasalisha nduze watukufu mabwana zetu
litukuke mno yina lake kwa kulla mtu
na kulla Mtume lilo haki hakushindana

Kulingana na ubeti wa 84, Jibrili aliandamana na Mtume (S.A.W.) katika safari ya mbinguni kutoka msikiti wa Baitul Mukadasi na kuwa naye pamoja kutoka uwingu wa kwanza hadi wa sita. Katika kila uwingu mhusika huyu ndiye aliyekuwa akijibu maswali yote ambayo Mtume (S.A.W.) alikuwa akiuliza kulingana na matukio mbalimbali yaliokuwa yakifanyika. Katika ubeti wa 82, mtunzi anasema Jibrili aliandamana na Mtume kutoka uwingu mmoja hadi mwengine. Maelezo haya vilevile yanatupa taswira ya kuwa mhusika huyu alikuwa mvumilivu kwa sababu alivumilia yote katika safari ya mbinguni na pia kujibu maswali aliyoulizwa na Mtume (S.A.W.) katika safari hii muhimu. Alikuwa mjuzi na alikuwa ndio kama mwakilishi wa Mwenyezi Mungu kwa kumfunza na kumuelimisha Mtume wake.

### 3.6 MUNKAR

Munkar ni miongoni mwa malaika wa Mungu. Kiumbe huyu huishi mbinguni na anachukua nafasi ya kuwa mhusika asiyekuwa wa kawaida. Pia tunaweza kumchukua kama mhusika mdogo kwa sababu kwa kiasi fulani amepewa nafasi chache au ndogo katika kazi hii. Mhusika huyu ni mtumishi wa Mola Mtukufu na aghalabu hufanya kazi pamoja na Nakir. Kulingana na mafunzo ya Uislamu, Malaika hawa ndio watakaouliza maswali kaburini punde mja anapozikwa. Kulingana na maelezo haya, mhusika huyu anadhihirisha kuwa kiumbe muajibikaji kwa sababu anatekeleza majukumu aliyopewa na Mungu bila uoga.

Tunaelezewa katika utungo kuwa mwenye kusoma Maulidi haya hatapata shida wakati atakapokuwa kaburini, kwa sababu ataweza kujibu maswali yote atakayoulizwa na Munkari. Kwa hivyo kaburi lake litakuwa bustani katika mabustani ya peponi. Maelezo haya yanadhihirisha kuwa mhusika huyu vilevile ni jasiri katika kazi yake na hii imechangia kwa wafuasi wa Mtume (S.A.W.) kujitayarisha vilivyo ili waweze kufaulu katika mtihani huu. Katika ubeti wa 9, mtunzi anasema:

Na faida zake za ahera takozibali
kyenda kaburini Munkari kumsaili
tafunda jawabu la kwokoa lililo ali
kaburiye iwe ni zitangu zema za janna

### 3.7 MALAIKA WENGINE

Hawa vilevile ni viumbe wa Mungu wasiokuwa wa kawaida, huishi mbinguni na wanachukua nafasi muhimu katika kazi hii japo wanajitokeza kama wahusika wadogo. Kulingana na Uislamu, kuna malaika wengi sana ambao idadi yake inajulikana na Mungu, ijapokuwa kuna baadhi ya malaika ambao wana majina na majukumu maalumu k.m Malik ni malaika wa motoni, Ridhwan ni malaika wa peponi n.k. Viumbe hawa ni watumishi wa Mungu na kazi yao ni kumtukuza Mungu. Hutekeleza majukumu yao jinsi wanavyoamrishwa na Mungu.

Mtunzi anasema kuwa malaika wa mbinguni walipokea na kujibu ujauzito wa Mtume (S.A.W.) na kadiri ujauzito huo ulivyokua, ndio malaika walizidi kuzidisha maombi ya heri njema, baraka na rehema. Maelezo haya yanadhihirishwa katika ubeti wa 41 na yathibitisha kuwa viumbe hawa ni wacha Mungu na kazi yao ni kumtukuza Mungu wakati wote na kuendeleza anayoyapendelea Mwenyezi Mungu.

Katika ubeti wa 56, tunaelezewa kuwa malaika walimuombea Mtume (S.A.W.) rehema na baraka kutoka kwa Mungu wakati wa mazazi yake. Kitendo hiki kinaonyesha kuwa malaika wana sehemu kubwa katika maombi kukubaliwa. Kulingana na mafunzo ya dini ya Kiislamu, malaika huwepo kila mahali isipokuwa sehemu za kujisaidia na vilevile sehemu ambazo maovu hufanywa. Vilevile malaika wana mchango mkubwa kwa maombi ya waja kukubaliwa, ndio maana waumini wa dini ya Kiislamu wanahimizwa katika hali zote kuzungumza mazuri na kujiepusha na maovu kwa sababu haijulikani ni wakati upi ambao maombi haya yatapokelewa na malaika kupelekwa kwa Mungu na kujibiwa.

Mtunzi katika ubeti wa 70 anatuelezea kuwa malaika wa mbinguni walikuwa pamoja na Mtume (S.A.W.) alipokuwa akitoka safarini, na katika ubeti wa 71 mtunzi anaendelea kutueleza kuwa malaika alikuwa amemfinika Mtume (S.A.W.) na mbawa zake ili asipatwe na jua. Kitendo hiki kinathibitisha kuwa viumbe hawa ni watiifu na wanatekeleza majukumu yao jinsi wanavyoamrishwa na Mungu. Mtunzi anasema:

Alimuonaye mefuatwa na malaika
na hari ya yua kwa mabawa humufunika
kaonya na wendi walo wote kifurahika
na Maisarati akanena aloyaona.

Malaika ni baadhi ya viumbe ambao walijumuika katika swala ambayo iliongozwa na Mtume (S.A.W.) katika msikiti wa Baitul Mukadasi kabla ya safari ya kwenda mbinguni kuanza. Maelezo haya yanatupa undani kuhusu viumbe hawa ya kuwa ni wacha Mungu na wanatekeleza maamrisho ya Mungu. Mtunzi anatupa maelezo haya katika ubeti wa 81.

Malaika vilevile ni viumbe waliokuwa na ufahamu kuhusu uzuri wa Mtume (S.A.W.) kwa sura na kwa tabia na walikuwa hawajaona kutoka kwa kiumbe chochote. Maelezo haya yanatupa habari kuwa viumbe hawa wametukuzwa na Mungu na ndiposa wamepewa ufahamu wa baadhi ya mambo. Maelezo haya yanapatikana katika ubeti wa 93.

## 3.8 WANAWAKE KWA JUMLA

Wanawake katika utungo huu wanajitokeza kama wahusika wa kawaida na wamepewa nafasi muhimu katika kufanikisha kazi hii. Waliomulikwa hususani ni Amina  Thuweiba, Halima, Khadija pamoja na marafiki zake wema, Maisara, Mariamu binti Imrani, Asiya, Maria Kibtiya, Fatima na  mamake kijana aliyesoma maulidi.

### 3.8.1 AMINA

Amina ambaye alikuwa mke wa Abdallah ni mamake Mtume Muhammad (S.A.W.). Mhusika huyu amesawiriwa  kama mhusika wa kawaida na vilevile mhusika msaidizi. Mhusika huyu ametukuka na ameepushwa na dhambi mbali mbali ikiwemo uzinifu ikizingatiwa kuwa hiki kilikuwa kipindi cha ukafiri. Kulingana na ubeti wa 38, mtunzi anatueleza kuwa Mungu amemtukuza mhusika huyu na kuwa hataingizwa katika moto wa Jahanamu. Mtunzi anasema:

Na mbali Mola na wa arishi alo karimu
katukua radhi kwa wazee wa muadhamu
licha kuwatia moto huo wa Jahannamu
hatta kuuona walidehu hawakuona

Amina alipata heshima kubwa na fahari kwa kumzaa Mtume Muhammad (S.A.W.). Pindi alipopata ujauzito wa Mtume Muhammad (S.A.W.), hata wanyama wa Makureishi walisikika wakizungumza kuhusu ujauzito huu, na kadiri ujauzito huu ulivyokua ndivyo wanyama hawa walivyozidi kuzungumzia. Mtunzi anatupa maelezo haya katika ubeti wa 40 na 41. Maelezo haya yanathibitisha kuwa mhusika huyu alikuwa ametukuzwa na Mungu na ndio maana alizaa kiumbe mtukufu ambaye ni Mtume Muhammad (S.A.W.).

Kulingana na mtunzi, mazazi ya Amina yalihudhuriwa na viumbe vitukufu vya mbinguni na duniani vikiwemo malaika, mahurulaini, na wanawake wema wakiwemo Mariyamu na Asiya. Maelezo haya yanajitokeza katika ubeti wa 42 mpaka 44. Maelezo haya yanatupa undani kuhusu mhusika huyu kuwa ni mcha Mungu ikizingatiwa kuwa viumbe vitukufu ndivyo vilivyohudhuria mazazi yake.

### 3.8.2 THUWEIBA

Mhusika huyu amesawiriwa kama mhusika wa kawaida na vilevile mhusika msaidizi. Ni mhusika ambaye anachangia katika malezi ya Mtume Muhammad (S.A.W.). Mtume alichukuliwa na Thuweiba ambaye alikuwa mwanamke mwenye twaa aliyetoka kabila la Kahtani lilojulikana ambapo alimlea Mtume (S.A.W.) katika nyumba ya mjombake. Mhusika huyu anajitokeza kama mhusika mcha Mungu na hali hii ilichangia kwa yeye kumlea Mtume (S.A.W.). Vilevile ni mhusika mwenye imani na mapenzi ambapo alichukua jukumu la kumlea Mtume (S.A.W.). Maelezo haya yanajitokeza katika ubeti wa 64 ambapo mtunzi anasema:

> Kamwamusha Tumwa mama wake siku saba
> kisa ni Thuweba Juruthumi mungi wa taa
> ali Kahatani ni kabila imezoshaa
> mbwa kwa amu yake huri huyu mulewa jana

### 3.8.3 HALIMA

Huyu ni mhusika wa kawaida na pia mhusika msaidizi ambaye anachangia vilivyo katika kumjenga mhusika mkuu ambaye ni Mtume Muhammad (S.A.W.). Halima alitoka katika kabila la Saadi na ndiye aliyemnyonyesha Mtume Muhammad (S.A.W.).

Kwa vile Mtume Muhammad (S.A.W.) alikuwa ni yatima, baada ya kuondokewa na baba yake akiwa matumboni mwa mama yake, wanyonyeshaji wengi walikataa kumnyonyesha kwa sababu ya tamaa za kilimwengu ikiwemo mali, japokuwa ilikuwa ni katika mila za Kiarabu kwa mtoto kunyonyeshwa na mama mwengine. Maelezo haya yanadhihirisha kuwa mhusika huyu hana tamaa kwa sababu alimnyonyesha na kumlea Mtume (S.A.W.) bila kutaka malipo yoyote, ikizingatiwa kuwa Mtume (S.A.W.) alikuwa yatima.

Kwa upande mwingine, Halima alikuwa maskini na wazazi wengine hawakutaka watoto wao wanyonyeshwe naye kwa sababu walichelea kuwa hangeweza kuwa na maziwa bora kutokana na kukosekana kwa lishe bora kwa sababu ya umasikini wake. Maelezo haya vilevile yanadhihirisha kuwa mhusika huyu alikuwa mvumilivu kwa kuvumilia hali yake ya umasikini. lakini licha ya misukosuko aliyopata, hatimaye alifanikiwa.

Kabla ya bi Halima kuanza kumnyonyesha Mtume (S.A.W.), kifua chake kilikuwa kikavu na punde alipoanza kumnyonyesha Mtume (S.A.W.), kifua chake kilijaa maziwa na ikawa ni miujza na baraka kutoka kwa Mungu. Mtunzi katika ubeti wa 65 anasema:

Na watatu wao ni Saada aloelea
sitina Halima kumwamusha kwa furahia
alishuka ziwa maweeni likamungia
alopata huyu Hamzia ameyanena

Kulingana na maelezo haya, bi Halima ni mhusika asiyekata tamaa na hali hii ilimfanya kumchukua Mtume (S.A.W.) na kumnyonyesha na kumlea licha ya hali aliyokuwa nayo.Mambo mengi ya mhusika huyu yalibadilika punde alipoanza kumnyonyesha na kumlea Mtume (S.A.W.), yakiwemo kwa mfano mifugo yake kama mbuzi, kondoo, ngamia n.k ambao awali walikuwa wamekonda na hawatoi maziwa, walibarikiwa na Mungu na wakapata afya nzuri na maziwa yakawa mengi. Ardhi iliyokuwa kavu vilevile ilipata rutuba na kuneemeka, na hii ilichangia katika kupata mavuno bora na hivyo njaa ikakosekana.

### 3.8.4 MARIYAMU BINTI IMRANI

Mhusika huyu vilevile amesawiriwa kama mhusika wa kawaida na mhusika msaidizi. Mariyamu ni mwana wa Imrani na ni mamake nabii Issa (A.S.) ambaye aliwahi kuteremshiwa kitabu cha injili ili kiwe mwongozo kwa wamchao Mwenyezi Mungu. Kulingana na dini ya Kiislamu, Mariyamu alikuwa ni mwanamke aliyekuwa mcha Mungu sana na hata ujauzito wake wa nabii Issa ulikuwa wa kimiujiza. Vilevile ni mwanamke wa

kipekee ambaye kuna sura nzima katika Qur'ani ambayo Mwenyezi Mungu ameipa jina la " Suratul Maryam" ambayo ina maelezo kiasi kuhusu mhusika huyu na jinsi ucha Mungu wake ulivyodhihirika (Qur'an 19).

Katika ubeti wa 43, mtunzi ametueleza kuwa Mariyamu alikuwa miongoni mwa waliohudhuria mazazi ya Mtume Muhammad (S.A.W.) na alimpa mwana Amina vinywaji vitamutamu ambavyo ladha yake haijawahi kuonjwa, wakati machungu ya mazazi yalipozidi, licha ya kuwa mhusika huyu tayari alikuwa amefariki. Hali hii inadhihirisha utukufu na cheo cha mhusika huyu kwa kumsaidia mamake Mtume (S.A.W.) wakati wa machungu ya mazazi. Mtunzi anasema:

Walohudhuria ni wawili hurulaini
na wake wawili ni wa huku ulimwenguni
sayidatina Mariyamu wa Imrani
na mwana Asiya muongofu na muuminina

Maelezo haya yanadhihirisha kuwa mhusika huyu alikuwa mcha Mungu na mwenye huruma kwa jinsi alivyomshughulikia mwana Amina wakati wa kujifungua kwa kumsaidia kumrahisishia hayo mazazi. Pia mhusika huyu ni muumini na muongofu.

### 3.8.5 MWANA ASIYA

Mwana Asiya anasawiriwa kama mhusika wa kawaida na msaidizi katika utungo huu. Yeye ni mke wa Firauni ambaye alijitangaza kuwa mungu na kuwashurutisha wana wa Izraili kumuamini na kumtegemea yeye. Vilevile ni mhusika aliyemlea Musa ambaye baadaye alipewa Utume na kitabu cha Taurati kuwaongoza wana wa Izraili. Musa alilelewa katika makazi ya Firauni. Licha ya kuwa mumewe Firauni alikuwa muovu, mwana Asiya alikuwa mhusika mcha Mungu sana. Mtunzi katika ubeti wa 43 anasema kuwa mwana Asiya ni muongofu na muumina, ingawa mume wake Firauni alikuwa kinyume cha mwana Asiya.

Katika ubeti wa 43, mtunzi anatueleza kuwa mhusika huyu alihudhuria mazazi ya Mtume (S.A.W) na machungu ya mazazi ya mwana Amina yalipozidi, mhusika huyu alimpa mwana Amina vinywaji vitamutamu ambavyo havijawahi kuonjwa. Kitendo hiki kinadhihirisha kuwa mhusika huyu alikuwa mcha Mungu, mwenye huruma na mapenzi kwa jinsi alivyochangia katika mazazi ya Mtume (S.A.W). Vilevile kwa kumlea Musa katika makazi ya Firauni kunadhihirisha kuwa alikuwa mhusika mwenye huruma na mapenzi.

### 3.8.6 KHADIJA

Mhusika huyu ni wa kawaida na vilevile mhusika msaidizi. Ni mwana wa Khuwalid bin Asad na ni mke wa kwanza wa Mtume Muhammad (S.A.W.) na wa kwanza kukubali Uislamu. Ni mamake Abdullah, Kassim Fatima, Rukayya, Ummu Kulthum na Zeinab. Mtunzi katika ubeti wa 70 anatueleza kuwa bi. Khadija alimuona Mtume (S.A.W.) akiwa pamoja na malaika na pia alimuona Mtume (S.A.W.) akifuatwa na malaika ambaye alikuwa akimkinga na mbawa zake kutokana na miale ya jua. Pia aliwaashiria matukio haya jinsi yalivyotokea wanawake wema ambao walikuwa marafiki zake. Matukio haya yanadhihirisha kuwa mhusika huyu alikuwa ametukuzwa na Mungu kwa sababu aliweza kuona matukio ambayo wengine hawakuweza kuyaona na yote haya ilikuwa kwa rehema zake Mungu. Mtunzi katika ubeti wa 70 anasema:

Pindi kirejea safarini mwenyi daraja
ali ghorofani kitungia mwana Hadija
pamwe na wangine wendaniwe wema wambeja
Tumwa na Malaki wa mbinguni wakyandamana

Katika ubeti wa 72 na 73 mtunzi ametueleza kuwa, bi. Khadija alimtaka Mtume (S.A.W.) amuoe na hatimaye matakwa yake yalikubaliwa kwa sababu jamaa zake Mtume upande wa baba waliridhika na uposi huo na wakasema kwamba Khadija alikuwa ni binamu yake na vilevile mwenye sifa za Kikureishi, mwenye mali, dini na uzuri alopawa na Mola. Kulingana na maelezo haya, mhusika huyu aliweza kutambua utukufu wa Mtume Muhammad (S.A.W) ndiyo sababu akamtaka amuoe ili apate neema, heri na baraka. Vilevile Khadija alitaka kuolewa na Mtume (S.A.W.) kwa sababu alitambua alikuwa mtu mwaminifu. Maelezo haya yanathibitishwa na mtunzi anaposema:

Kataka Mtume amuoe huyu takia
lalitoa jito la nanangu Tumwa kingia
mataka ya nana alotaka yakatimia
jamii dhuria mbwake yeye sayidatina

Katika ubeti wa 77, mtunzi anatueleza kuhusu kuteremshwa kwa wahyi kwa Mtume (S.A.W.) kupitia kwa malaika Jibrili. Wakati huu Mtume (S.A.W.) alikuwa katika nyumba ya bi Khadija. Mtume (S.A.W.) hakuweza kujua kama alikuwa ni malaika au ni shetani. Bi. Khadija, katika kuthibitisha kama ni shetani au wahyi aliwacha kichwa chake wazi na malaika Jibrili alijificha, baadaye bi. Khadija alijifunika kichwa na malaika Jibrili alirudi kwa

Mtume (S.A.W.). Hapa ndipo bi. Khadija alipotambua kuwa, yule Mtume (S.A.W.) aliyemwona alikuwa ni malaika na wala sio shetani.

Kulingana na maelezo haya, bi Khadija alitambua kuwa Mtume (S.A.W.) alikuwa ni mcha Mungu, na vilevile Mtume wa Mwenyezi Mungu. Mhusika huyu alikuwa ni mcha Mungu na mwenye kufikiri sana kwa kitendo cha kutaka kufahamu kama ilikuwa wahyi ama shetani.

### 3.8.7 MAISARA

Huyu ni mhusika wa kawaida na mhusika msaidizi. Ni mtumishi wa bi. Khadija ambaye alikuwa mke wa Mtume (S.A.W.). Katika ubeti wa 71, mtunzi anatueleza kuwa mhusika huyu alikuwa miongoni mwa walioelezewa na bi. Khadija kuhusu Mtume (S.A.W.) kufuatwa na malaika. Mhusika huyu ndiye aliyetumwa na bi. Khadija kwa Mtume (S.A.W.) kumtaka amuoe, na uposi huu ulikubaliwa. Maelezo haya yanadhihirisha kuwa mhusika huyu alikuwa mwaminifu na hali hii ilimpelekea bi. Khadija kumtuma kwa Mtume (S.A.W.).

### 3.8.8 MARIA KIBTIYA

Huyu ni mhusika wa kawaida na vilevile mhusika msaidizi. Ni mke wa Mtume Muhammad (S.A.W.) ambaye alitumwa kama zawadi na mfalme wa Misri alipokuwa Madina. Ni mamake Ibrahim ambaye alizaa na Mtume (S.A.W.). Katika ubeti wa 75, mtunzi anatupa habari kwa uchache kuhusu mhusika huyu ya kuwa Mtume alizaa naye mwana mmoja ambaye ni Ibrahimu. Mhusika huyu anadhihirika kama mcha Mungu kwa kuolewa na Mtume Muhammad (S.A.W.) na vilevile mfalme wa Misri kwa kiasi fulani hangeweza kumpa zawadi Mtume Muhammad (S.A.W.) kama hangekuwa mcha Mungu.

### 3.9.9 WANAWAKE WEMA

Hawa ni wahusika wa kawaida na wahusika wasaidizi. Ni rafiki zake bi. Khadija. Mtunzi anatupa habari zao katika ubeti wa 71 wakati bi. Khadija anapowaelezea kuhusu Mtume (S.A.W) akifuatana na malaika wanaomkinga kutokana na jua. Maelezo haya yanadhihirisha kuwa wahusika hawa ni wacha Mungu ndio maana walikuwa wametangamana na viumbe wacha Mungu kama bi. Khadija. Vilevile ni waaminifu na wanakubali yote wanayoelezewa na bi Khadija kumhusu Mtume (S.A.W.).

### 3.10 WANAUME KWA JUMLA

Wanaume wametekeleza nafasi muhimu katika kufanikisha utungo huu na wamejitokeza kama wahusika wa kawaida. Wahusika hawa ni pamoja na Abdalla, Abdulmuttalib, Abutalib, Mjombake Thuweiba, pamoja na Abubakar**.**

#### 3.10.1 ABDALLA

Abdalla ni babake Mtume (S.A.W.) na mumewe Amina. Mhusika huyu anajitokeza kwa uchache lakini anatekeleza jukumu kubwa sana katika kazi hii. Anajitokeza kama mhusika wa kawaida na pia mhusika msaidizi. Mtunzi katika ubeti wa 38 anasema kuwa Mungu amemtukuza mhusika huyu na kamwe hataingizwa katika moto wa Jahanamu. Maelezo haya yanadhihirisha kuwa, kutokana na kuweka mbegu ya Mtume (S.A.W.) ambaye alikuwa ametukuzwa na Mungu, yeye vilevile alipata neema ya kutukuzwa na Mungu. Licha ya kuwa mhusika huyu alifariki kabla ya kuzaliwa kwa Mtume (S.A.W.) mchango wake unasababisha matukio mengi ambayo Mtume (S.A.W.) aliyapitia kama yanavyojitokeza katika utungo huu.

#### 3.10.2 ABDULMUTTALIB

Huyu ni mhusika wa kawaida na pia msaidizi. Ni babu yake Mtume Muhammad (S.A.W.) na baba yake Abdalla. Punde Mtume Muhammad (S.A.W.) alipozaliwa, alipelekwa kwa mhusika huyu ambaye alifurahi sana na kumshukuru Mungu. Hatimaye alimpeleka Mtume Muhammad (S.A.W.) katika Al Kaaba na kumuombea ili akingwe na kila aina ya mabaya, ikiwemo hasadi na pia akue na siha njema. Mtunzi anatupa maelezo haya katika ubeti wa 57 na 59. Maelezo haya yanadhihirisha kuwa mhusika huyu alikuwa mwenye imani licha ya kuwa hakuukubali Uislamu. Vilevile mhusika huyu alikuwa mwenye huruma na mapenzi ikizingatiwa kuwa Mtume (S.A.W.) alikuwa yatima lakini hakuchelea kumfanyia mema.

#### 3.10.3 ABUTALIB

Mhusika huyu anajitokeza kama mhusika wa kawaida na pia msaidizi. Ni ami yake Mtume (S.A.W), nduguye Abdalla ambaye alikuwa babake Mtume (S.A.W.), na mwana wa Abdulmuttalib ambaye alikuwa babu yake Mtume (S.A.W.). Katika ubeti wa 70 na 73, mtunzi anasema mhusika huyu alikuwa akiandamana na Mtume Muhammad (S.A.W.) katika safari na wakati Khadija alipomtaka Mtume (S.A.W.) amuoe, aliwajulisha jamaa zake upande wa baba na mmoja wao alikuwa ni Abutalib. Maelezo haya yanaonyesha kuwa mhusika huyu alikuwa mwenye huruma na mapenzi kwa kumlea Mtume (S.A.W.) baada ya kufariki babu

yake ijapokuwa hakukubali dini ya Uislamu. Ni mhusika aliyemtakia mema Mtume (S.A.W.) kwa kukubali uposi wa Khadija ambaye alikuwa mke mcha Mungu.

### 3.10.4 MJOMBAKE THUWEIBA

Mhusika huyu ni wa kawaida na vilevile msaidizi. Ni mjombake Thuweiba ambaye alimlea Mtume (S.A.W.). Kulingana na utungo huu, mhusika huyu alichangia katika malezi ya Mtume Muhammad (S.A.W.). Mtunzi katika ubeti wa 64 anatueleza kuwa Mtume (S.A.W.) alilelewa katika nyumba ya mhusika huyu. Maelezo haya yanathibitisha kuwa, mhusika huyu alikuwa mwenye kujali na pia mwenye mapenzi na huruma kwa kukubali Mtume (S.A.W.) ambaye alikuwa ni yatima kulelewa na bi Thuweiba katika nyumba yake.

### 3.10.5 ABUBAKAR

Mhusika huyu ni wa kawaida na pia msaidizi. Ni rafiki yake Mtume (S.A.W.) na ni babake Aisha (R.A.A.) ambaye alikuwa mke wa Mtume (S.A.W.). Alikuwa Khalifa wa kwanza kulingana na historia ya Kiislamu. Mhusika huyu alikuwa mtu mkarimu sana kwa sababu alitumia mali yake katika kueneza dini ya Uislamu.

Katika ubeti wa 86 na 87, mtunzi anasema kuwa mhusika huyu aliyaamini yote aliyoyasema Mtume (S.A.W.), pindi alipotoka safari ya mbinguni na yote aliyoelezewa aliyakubali. Kwa vile alikuwa rafiki wa karibu wa Mtume (S.A.W.), ilichangia kwa mhusika huyu kukubali yote aliyoelezewa na Mtume (S.A.W.) kuhusu safari yake ya kwenda mbinguni na pia aliyoelezewa kuhusu dini ya Uislamu. Alifahamika kama “ As Sidiq” yaani aliyeamini yote aliyoelezewa na Mtume Muhammad (S.A.W.).

Mhusika huyu ni mwenye imani thabiti na vilevile mwaminifu kwa kukubali yote aliyoelezewa na Mtume (S.A.W). Pia ni mwenye mapenzi na huruma kwa kuwa mtu wa karibu sana kwa Mtume (S.A.W.) ambapo hali hii ilichangia katika kuenea kwa dini ya Kiislamu hususan walipohama Makka kwenda Madina ambako watu wengi walimkubali Mtume (S.A.W.) na dini ya Kiislamu. Alitoa mali yake nyingi katika kueneza Uislamu na hakuwa na tamaa za kilimwengu. Kandhalavi (1999).

Kulingana na Sheikh (2006), mhusika huyu aliwakomboa watumwa waliokuwa wakiteswa sana na Makureishi baada ya kuukubali Uislamu. Alitumia mali yake kuwanunua na kuwaacha huru. Alisimamia gharama zote kwa ajili ya ujenzi wa msikiti Nabawi ulioko

Madina. Vilevile alichangia katika ukusanyaji na uhifadhi wa Qur’an Tukufu. Pia alisimamia kwa hali na mali wakati Waislamu walipokuwa wanahama kutoka Makka kwenda Madina.

### 3.11 MITUME

Wahusika hawa ni wa kawaida na pia wasaidizi. Ni viumbe wa Mwenyezi Mungu waliochaguliwa hususan kufikisha ujumbe wa Allah kwa walimwengu. Kulingana na dini ya Kiislamu, kuna Mitume ishirini na tano waliotajwa katika kitabu cha Qur’an wa kwanza akiwa Adam (A.S) na wa mwisho Muhammad (S.A.W). Kuna Mitume mbalimbali waliopewa vitabu na Mwenyezi Mungu (S.W.T). Mtume Ibrahim (A.S) alipewa Suhuf ambapo imethibitishwa katika Qur’an sura ya 87, Mtume Daud (A.S) alipewa Zabur, Musa (A.S) alipewa Taurat, Issa (A.S) alipewa Injil, na Mtume Muhammad (S.A.W) alipewa kitabu cha Qur’an.

Katika ubeti wa 105, Mtunzi anatueleza kwamba, kama si Mtume Muhammad, Mtume Adam hangekuweko, na vilevile mitume Ibrahim, Issa, Musa na Suleiman hawangekuwepo na hata ingawa Suleiman alikuwa mfalme.

Mtunzi katika ubeti wa 91 anasema kwamba, mwisho wa Mtume Muhammad (S.A.W) unaashiria mwisho wa mitume yote. Maelezo haya yanasadifiana na *ukawafi wa Miiraji* ambapo katika ubeti wa 78, 79, 80 na 81na 82 mtunzi anatuelezea kwamba “Mtume alipiga magoti na kusujudu akaambiwa na Mola aseme atakacho, akasema kwamba mja wake Ibrahimu ni kipenzi chake, je yeye Mtume? Mola alimjibu kwamba: Daudi alipewa Zaburi, Suleimani kamiliki majini, na yeye Mtume Muhammad ni mwanzo na mwisho wa mitume. Wakati Issa alipoponya vilema na kufufua wafu na yeye Mtume vilevile atakuwa miongoni mwao na yake ni arshi isiyokwisha na umati wake ni bora ambapo siku ya kiama yeye atakuwa shahidi wakati makafiri watakapoikana dini ya haki.” Mtunzi katika Ukawafi wa Miiraji amesema:

Alipomuona Mola wake aso mithali,
Asiweze neno kutamuka yake kauli;
Akenda sijida. Kamwambia Mola Jalili:
Omba utakalo utapewa yote timama (ubeti wa 78)

Kamba: Mola wangu, mja wako Iburahimu
Ni wako mwendani, nami nini yangu sehemu?
Mola kamwambia: nawe Tumwa wangu fahamu
Ni kipendo kyangu afudhali ya wote Tumwa. (ubeti wa 79)

Kamba tumupele Daaudi yake zaburi,
Na Sulaimani kumiliki jinni na tweri;
Nawe ni awali ya Mitume, ndiwe aheri
Nidhukuriwapo na isimu yako i nyuma (ubeti wa 80)

Na kamaye Isa akipoza kulla kilema,
Na kuwafufua wafieo yake kalima,
Nawe nikupele kufufua na mangi kama
Ni yako kanizi ya arishi isiyokoma (ubeti wa 81)

Na umati wako afudhali kuliko pia,
Siku ya kiama utakuya kushuhudia.
Pindi wakanapo makufari wote nambia
Hawakutabia mambo yao walio tumwa (ubeti wa 82)

Maelezo haya yanadhihirisha kuwa wahusika hawa ni watukufu kwa sababu wamechaguliwa na Mwenyezi Mungu kufikisha ujumbe kuhusu dini kwa uma mbali mbali. Pia wahusika hawa ni wacha Mungu ikizingatiwa kuwa walifuata na kutekeleza maamrisho ya Mwenyezi Mungu. Wahusika hawa vilevile ni wenye subira kwa kuwa waliweza kustahamili yote yaliyowafika kwa lengo la kueneza dini. Pia wamepewa vipawa na uwezo mbalimbali k.m. Mtume Suleimani alipewa kipawa cha kumiliki majini (Qur'an 27 aya ya 17), naye Issa alipewa kipawa cha kufufua wafu (ukawafi wa Miiraji ubeti wa 81). Mtume (S.A.W) naye alifuatwa na mtu ambaye hakuwa na chakula cha kuwapa jamaa zake, Mtume (S.A.W.) alimpa mtama nusu ambao uliweza kukimu familia nzima pamoja na wageni na haukuisha japokuwa ulikuwa kidogo (Nursi 2004).

## 3.12 WATOTO WA MTUME MUHAMMAD (S.A.W)

Wahusika hawa vilevile wanasawiriwa na wanachukua nafasi ya kuwa wahusika wa kawaida na pia wasaidizi. Mtume Muhammad (S.A.W.) alikuwa na watoto watatu wa kiume na wanne wa kike. Watoto sita alizaa na bi Khadija isipokuwa mmoja tu aliyeitwa Ibrahim aliyezaa na Maria Kibtiya.

Kassim ndiye aliyekuwa mwanawe wa kwanza wa kiume aliyezaliwa kabla hajapewa Utume. Kassim alifariki alipokuwa na umri wa miaka miwili. Mtoto wake wa pili wa kiume Abdullahi alizaliwa baada ya kupewa Utume. Pia alikuwa akiitwa kwa majina ya 'Tayyab' na 'Tahir'. Huyu pia alikufa utotoni. Alipokufa, Makureishi walifurahi na wakasema Muhammad hana mwana wa kiume na kwa hivyo atakuwa hana kizazi na akifa jina lake litamalizika.

Ibrahim, mwanawe wa kiume wa tatu na ndiye aliyekuwa mwanawe wa mwisho, alizaliwa Madina katika mwaka wa nane wa Hijra na mamake aliitwa Maria Kibtiya. Mtoto huyu alifariki tarehe kumi mwezi wa Rabiul Awwal mwaka wa kumi wa Hijra.

Zeinab alikuwa bintiye wa kwanza wa Mtume Muhammad (S.A.W.) na alizaliwa katika mwaka wa tano katika ndoa yake ya kwanza ambapo Mtume (S.A.W.) alikuwa na miaka thelathini. Zeinab alisilimu na akaolewa na binamu yake Abul-As bin Rabi.

Ruqayyah alizaliwa miaka mitatu baada ya kuzaliwa Zeinab wakati Mtume (S.A.W.) alipokuwa na miaka thelathini na tatu. Aliolewa na Utbah, mwanawe Abu Lahab ambaye alikuwa ami yake Mtume (S.A.W). Baadaye Ruqayyah alitalikiwa na aliolewa na Uthman (R.A.A) ambaye alikuwa Khalifa wa pili katika Uislamu.

Ummu Kulthum ni binti wa tatu wa Mtume (S.A.W.) ambaye aliolewa na Utaibah mwanawe Abu Lahab. Utaibah alimtaliki Ummu Kulthum baada ya kushuka wahyi wa sura "Al Lahab".Fatima (R.A.A) alikuwa bintiye Mtume (S.A.W.) wa nne na wa mwisho. Alizaliwa katika mwaka wa kwanza wa Utume wakati Mtume (S.A.W.) alipokuwa na umri wa miaka arubaini na moja. Yasemekana kuwa jina la Fatimah ambalo maana yake halisi ni 'Salama' kutokana na moto liliitwa na Allah. Aliolewa na Ali (R.A.A.) katika mwaka wa pili wa Hijra. Fatima alikuwa na miaka kumi na tano na Ali alikuwa na miaka ishirini na moja. Fatimah alikuwa kipenzi cha Mtume (S.A.W.) na alikuwa na watoto watatu wa kiume na watatu wa kike. Hassan alizaliwa katika mwaka wa pili baada ya arusi yake, Hussein akazaliwa mwaka wa tatu naye Muhassan akazaliwa mwaka wa nne lakini alikufa utotoni. Bintiye wa kwanza Ruqayyah alifariki akiwa mchanga na kwa hivyo hakutajwa sana katika historia ya Kiislamu. Bintiye wa pili alikuwa Ummu Kulthum ambaye aliolewa na Aun bin Jaafar na watatu alikuwa ni Zeinab ambaye aliolewa na Abdalla bin Jaafar.

Kulingana na ubeti wa 55 na wa 75, mtunzi anatupa maelezo kuhusu watoto wa Mtume (S.A.W.) kwa kutuelezea kuhusu idadi yao, utukufu wa watoto hawa na vilevile wazazi wao. Maelezo haya yanadhihirisha kuwa watoto hawa walikuwa watukufu na vilevile wacha Mungu na walichangia vilivyo katika kuendeleza Uislamu hususani Fatimah ambaye kulingana na Uislamu ni " kiongozi wa wanawake wa Jannah". Kandhalavi (1999).

## 3.13MAHURULAINI

Mahurulaini ni viumbe vya Allah huishi peponi. Viumbe hawa wamesawiriwa na kuchukua nafasi ya viumbe wasiokuwa wa kawaida. Kur'ani tukufu inawataja viumbe hawa katika sura mbalimbali k.v. Suratul Waqia aya ya 22,23 na 35 mpaka 37, Suratul Fusilat aya ya 31 mpaka 32, Suratul Rahman aya ya 56, 58, 70, 72 na Suratul Baqarah aya ya 25. Kulingana na Kur'an tukufu, wanawake hawa hawajaguswa kimwili na wataolewa na kuwatumikia wale wanaume waliotekeleza amri za Mwenyezi Mungu walipokuwa duniani. Katika ubeti wa 42 na 44 , mtunzi anatueleza kwamba mazazi ya Mtume yalihudhuriwa na wanawake wanne, warembo ajabu ambao wawili wao walikuwa mahurulaini, na machungu ya mazazi yalipozidi kwa mamake Mtume, wema wawa hawa walimpa vinywaji vikiwemo vinywaji vitamutamu ambavyo ladha yake haijawahi kuonjwa. Mtunzi anasema kwamba:

Wakati wa mimba ya Hashimu ikitimia
kiona utungu wa mazazi walikingia
kupiganika kwa Amina kuhudhuria
wanawake wane uzuriwe hawayaona

Walohudhuria ni wawili hurulaini
na wake wawili ni wa huku ulimwenguni
ni sayidatina Mariyamu wa Imrani
na mwana Asiya muogofu na muumina

Kulingana na mtunzi, wahusika hawa wanadhihirika kuwa watukufu kwa sababu walichaguliwa na Mwenyezi Mungu kuhudhuria mazazi ya Mtume (S.A.W) ambaye alikuwa kiongozi mtukufu. Walikuwa wacha Mungu kwa sababu wanatekeleza amri za Mwenyezi Mungu kama inavyotakikana na kama inavyoonekana. Wahusika hawa ni watiifu na wanatekeleza amri za Mwenyezi Mungu na jambo hili linajitokeza wanapompa bi Amina vinywaji vitamu wakati wa mazazi ya Mtume (S.A.W).

## 3.14 MASWAHABA

Wahusika hawa wanasawiriwa na kuchukua nafasi ya kuwa wahusika wa kawaida na pia wasaidizi. Ni wafuasi wa Mtume (S.A.W) na walijitolea kwa hali na mali katika kueneza na kuinusuru dini ya Kiislamu.

Katika ubeti wa 25, maswahaba wanasifiwa kuwa ni viumbe wafanyao vitendo vyema na ambavyo vinajitokeza kwa waumini wale waliohama na Mtume (S.A.W) kutoka Makka. Katika ubeti wa 5, Mtunzi anasema kwamba: Maswahaba walitosheka na yote Mtume aliyowafikishia kabla ya kufa kwake. Mtunzi anasema:

Hao masahaba walitosha kwaye Sayidi
wasiadhimishe mno haya Maulidi
kifa wakakuza kazaliwa kwa Ahmadi
na alio kwanda kutukuza tutamnena

Maelezo haya yanatupa undani kuhusu wahusika hawa, kuwa walikuwa watiifu kwa Mtume (S.A.W.) na walitosheka na yote waliyoyaona na kuyasikia katika kuendeleza dini. Pia wahusika hawa walikuwa wacha Mungu na sifa hii inadhihirika wakati tunapoelezwa kuwa walikuwa viumbe wafanyao vitendo vyema kutokana na kuhama kwao kutoka Makka kwenda Madina kwa ajili ya Uislamu. Vilevile walikuwa hawana tamaa za mali kwa kuwa walipohama kwenda Madina, wengi wao waliwacha mali zao kwa ajili ya Uislamu.

Kulingana na Kandhalavi (1999), maswahaba walichangia sihaba katika kuiendeleza dini ya Kiislam kwa sababu ya msimamo wao thabiti katika kukabili shida. Katika mwaka wa sita wa Hijra wakati Mtume (S.A.W.) na maswahaba wake walipoondoka kwenda Makka kufanya umrah walilazimika kupiga kambi mahali paitwapo Hudeibiyah baada ya Makureishi kuwazuia kuingia Makka na idadi yao ilikuwa elfu moja na mia nne. Maswahaba walikuwa tayari kutetea dini yao lakini hatimaye Mtume aliingia katika mapatano na Makureishi na kuleta mkataba wa Hudeibiyah. Baadhi ya maswahaba walioteseka kwa sababu ya dini yao ni; Bilal, Sumeiya, Khabab bin Kharat n.k.

### 3.15 MUHAJIRUN NA ANSAR

Wahusika hawa wanasawiriwa kama wa kawaida na vilevile wasaidizi. Japokuwa wanajitokeza kwa uchache katika kazi hii, wanachangia vilivyo katika kueneza Uislamu. Muhajirun ni wafuasi wa Mtume (S.A.W) waliohama naye kutoka Makka kwenda Madina wakati Makureishi walipopanga kumuua Mtume (S.A.W). Ni wakati huu ambapo Kalenda ya Kiislamu ilipoanza. Ansar nao ni wafuasi wa Mtume (S.A.W) waliompokea Mtume (S.A.W) pamoja na wafuasi wake katika mji wa Madina.

Kulingana na utungo huu, katika ubeti wa 25 mtunzi anasema: Vitendo vyema ambavyo vinajitokeza kwa waumini vikiwemo kutekeleza na kuamini yote aliyokuja nayo Mtume Muhammad (S.A.W) ambavyo vinajitokeza katika nguzo tano za Uislamu na pia nguzo sita za Imani. Wale waliohama na Mtume (S.A.W.) kutoka Makka yaani Muhajirun na waliowapokea na kuwasaidia ambao ni Ansar. Maelezo haya yanathibitisha kuwa wahusika hawa walikuwa wenye msimamo thabiti. Licha ya kupata misukosuko mingi hawakukata tamaa na walikuwa tayari kuinusuru na kuiendeleza dini ya Kiislamu.

Vilevile ni wahusika wacha Mungu kwa sababu wanasifiwa kuwa wenye vitendo vyema kwa kufuata yote aliyokuja nayo Mtume (S.A.W.). Wanajitokeza kama wahusika wenye umoja kwa kuamua kuhama na Mtume (S.A.W.) na waliowapokea Madina kuwashughulikia kwa pamoja. Vilevile kitendo cha Ansar kuwapokea Muhajirun kinadhihirisha kuwa wahusika hawa walikuwa na mapenzi na huruma. Wahusika hawa pia walikuwa wenye subira na ingawa walipata misukosuko mingi, walistahamili na kuitetea dini ya Uislamu. Vilevile Muhajirun hawakujali kitu wala mali walizoziacha Makka lengo lao kuu lilikuwa kutekeleza amri za Mwenyezi Mungu kwa kufuata aliyokuja nayo Mtume Muhammad (S.A.W.) na Ansar vilevile walikuwa tayari kutumia vyao kuwasaidia Muhajirun (ubeti wa 25).

### 3.16 WANYAMA, MITI YA MITENDE NA MAJABALI

Wanyama, miti ya mitende, milima, na majabali inasawiriwa kuchukua nafasi ya kibinadamu. Viumbe hivi vinachukua nafasi ya wahusika wadogo na vinachangia katika utendakazi wa Mwenyezi Mungu.

Katika ubeti wa 41 na 42, mtunzi anatueleza kuwa wanyama wa Makureishi walikuwa na ufahamu kuhusu mimba ya Mtume (S.A.W.), na kadiri ilivyozidi kukua walizidi kuitangaza kuwa ni bahati kwa walimwengu. Kutokana na maelezo haya, wahusika hawa ni wajuzi wa mambo kutokana na ilimu waliokuwa nayo kuhusu mimba ya Mtume (S.A.W.).

Katika ubeti wa 51, mtunzi anasema kuwa hata kigogo kikavu cha mtende kilimlilia Mtume (S.A.W.) kikitaka nusura sembuse binadamu ambao pia walitaka wanusuriwe. Maelezo haya vilevile yanatupa mwangaza kuhusu utukufu wa Mtume (S.A.W.) mbele ya viumbe wengine. Licha ya kuwa kigogo cha mtende kilikuwa kikavu lakini kilihisi utukufu wa Mtume (S.A.W.).

Mtunzi katika ubeti wa 98 anatueleza kuwa hata majabali yaliyo Makka na yaliyo makuu yalimwambia Mtume (S.A.W.) yatageuka ili yawe dhahabu apate kuwa tajiri lakini Mtume (S.A.W.) alikataa na kusisitiza kuwa haja yake ni Janna. Maelezo haya vilevile yanadhihirisha utukufu wa Mtume (S.A.W.) kwamba hata majabali pia yalikuwa yanamfahamu Mtume (S.A.W.).

### 3.17 WAHUSIKA WENGINE

Kuna wahusika wengine ambao wanajitokeza katika utenzi huu na ambao wanasawiriwa na kuchukua nafasi ya wahusika wadogo na vilevile wa kawaida. Wahusika wadogo aghalabu huwa wanafanya kazi ndogo sana katika kazi yoyote ya fasihi kama vile kujenga maudhui au mandhari. Wahusika hawa wakitolewa kazi ya fasihi inaweza kuendelea bila kubadilika. Wahusika hawa ni kama mayatima, mashahidi, wanazuoni, Mudhaffari, watungao maulidi, kijana, mamake kijana na wafalme.

Katika ubeti wa 18 na 19, mtunzi anasema kuwa katika kisomo cha maulidi haya, ni aula mayatima washughulikiwe na yote haya yafanyike kwa ajili ya kumtukuza Mola Mtukufu na vilevile ili kisomo kikubaliwe. Maelezo haya yanawiana na mafunzo ya dini ya Kiislamu kuhusu umuhimu wa kushughulikia mayatima. Mwenye kumshughulikia yatima atakuwa pamoja na Mtume (S.A.W) peponi. Kulingana na Qur’an 107 aya 1 hadi ya 2, Mwenyezi Mungu (S.W.T) anasisitza kwamba wale wanaokadhibisha dini ni wale wasiowatendea wema mayatima.

Vilevile katika ubeti wa 10, mtunzi anasisitiza kwamba atakayesoma maulidi haya, atafufuliwa pamoja na mitume na mashahidi. Maelezo haya yanakinzana na mafunzo ya dini ya Kiislamu kwa sababu hakuna ushahidi wowote kuhusiana na kalima hii ikizingatiwa kuwa mitume ni viumbe watukufu waliofuata maamrisho ya Mwenyezi Mungu na kuyaeneza kwa umma wao, nao mashahidi ni wale wanaopigana na kufa kwa ajili ya Allah (S.W.T.).

Katika ubeti wa 6, mtunzi anatueleza kuwa miongoni mwa watu wa awali kutukuza maulidi haya alikuwa Mudhaffari ambaye alitumia dinari laki tatu na alipoulizwa kuhusu umuhimu wake, alijibu kwamba ni malipo wakati atakapoondoka ulimwenguni na hali kadhalika miongoni mwa faida za duniani ni kupata amani na baraka mwaka mzima na kuepushwa na mikasa na mitihani kama vile kuibiwa hali kadhalika kuchomeka kwa nyumba kama

inavyojitokeza katika ubeti wa 8. Maelezo haya yanadhihirisha kuwa mhusika huyu alifahamu kuhusu umuhimu wa maulidi haya ndiyo maana akagharamika na kuyatekeleza akichelea yatakayomfika kama hangeyasoma na vilevile manufaa yake kama atayasoma.

Kulingana na ubeti wa 7, mtunzi anatoa wasia kwamba watungao maulidi wanaombwa wanapoyatunga, wasiyafanye marefu ili wasichokeshe watakaoyasoma kwani sifa za Mola Mtukufu hazina mwisho. Maelezo haya yanadhihirisha kuwa wahusika hawa wana kipawa cha kuweza kutunga maulidi na hivyo wanaweza kuyafanya mafupi kutokana na ujuzi walionao.

Mtunzi anaeleza kwamba kuna kijana aliyefiliwa na babake na akaachiwa dinari pekee na alipopita kwa watu waliokuwa wanasoma maulidi, alikaa na kushiriki katika sherehe hii mpaka mwisho na alipolala aliota amefufuliwa siku ya kiyama na kutiwa peponi na baadaye watu walilia sana kutokana na matokeo haya (ubeti wa 10 hadi 11). Wakati wa hesabu, kuna mtu alilipwa nyumba iliyokuwa nzuri zaidi, na kijana alipoiona na alipotaka kuingia, aliambiwa ni ya wasomao maulidi pekee na kulipokucha kijana huyu alitayarisha chakula na dinari alizokuwa nazo, na kama ada alisoma maulidi na alipolala alimuota mamake akimuombea jaza njema kutokana na kitendo alichokifanya. Pindi mamake alipomuona mwanawe ametukuzwa, alijipulizia manukato wakapigana pambaja kudhihirisha furaha aliyokuwa nayo mamake kwa kutekeleza kisomo cha maulidi. Maelezo haya yanatupa undani kuhusu mhusika huyu kuwa licha ya kuwa na dinari pekee, hakujali mali bali alizitumia hizo chache alizokuwa nazo na kutekeleza kisomo cha maulidi haya. Vilevile alifahamu kuhusu umuhimu wa maulidi haya ndio maana aliyasoma ili apate fadhila zake.

Katika ubeti wa 13 na 14 , Mtunzi anatueleza kuhusu mamake kijana aliyemuona mwanawe ametukuzwa na hatimaye alijipulizia manukato na wakapigana pambaja kudhihirisha furaha aliyokuwa nayo mamake kwa kutekeleza kisomo cha maulidi. Maelezo haya yanathibitisha kuwa mhusika huyu anatambua umuhimu wa maulidi na hali hii ilimfanya yeye kufurahia kitendo alichokifanya mwanawe.

Wanazuoni wacha Mungu nao wanasawiriwa na kuchukua nafasi ya wahusika wa kawaida na pia wahusika wadogo. Hawa vilevile ni wafuasi wa Mtume (S.A.W.) na wanachangia katika kuikuza na kuiendeleza dini ya Kiislamu. Kulingana na ubeti wa 60 mtunzi anasema kuwa wanazuoni wacha Mungu wanatuambia tujitahidi kusimama na kunyenyekea pindi

anapotajwa Mtume (S.A.W.) kuonyesha adabu na heshima kwa kiongozi huyu mtukufu. Wahusika hawa wanatambua umuhimu wa Mtume (S.A.W.) kwa wafuasi wake na pia wana ufahamu kuhusu thamani ya Mtume (S.A.W.).

Wafalme nao vilevile wanachukua nafasi ya kuwa wahusika wa kawaida na katika ubeti wa 97 tunaarifiwa kuwa walimheshimu na kumuogopa Mtume lakini licha ya haya, Mtume hakuwajali pamoja na mali na nguvu zao huku tegemeo lake kuu likiwa Mola Mtukufu. Wahusika hawa walitambua utukufu wa Mtume (S.A.W.) na walidhani atawapokonya vyeo vyao, lakini ilikuwa kinyume cha matarajio yao kwani hakuwa na tamaa ya kidunia.

## 3.18 HITIMISHO

Katika sura hii, tumechunguza nafasi ya wahusika na uhusika katika *Maulidi ya Nuni.* Aghalabu tumeweza kuwataja wahusika waliojitokeza katika utenzi huu, baadaye tuliwagawanya katika wahusika wa kawaida na wasiokuwa wa kawaida. Wahusika wa kawaida ni wale ambao wamejitokeza katika hali ya kibinadamu na sifa zao mara nyingi ni za kibinadamu. Kwa upande mwengine wahusika wasiokuwa wa kawaida ni wale ambao wamesawiriwa kuwa na sifa zisizokuwa za kibinadamu kama tulivyoona. Hali kadhalika tumeonyesha jinsi wahusika pamoja na uhusika wao unavyojitokeza katika kazi hii, na kama wanasawiriwa kama wahusika wakuu, wadogo ama wasaidizi. Hatimaye tumeona jinsi wanavyosawiriwa na sifa zao zinavyojitokeza ili kutimiza dhima ya utungo huu.

# SURA YA NNE

## 4.1 MATUMIZI YA LUGHA, TAMATHALI ZA USEMI, TASWIRA AU JAZANDA, UHURU WA MTUNZI, MUUNDO NA MANDHARI KATIKA MAULIDI YA NUNI.

## 4.2 UTANGULIZI

Katika sura ya pili tumeeleza dhana za kimsingi kuhusu matumizi ya lugha, tamathali za usemi, taswira au jazanda, uhuru wa mtunzi, muundo na mandhari kulingana na maelezo ya wataalamu mbalimbali. Katika sura hii tumeshughulikia dhana hizi kama zilivyojitokeza katika *Maulidi ya Nuni.* Mtunzi kwa kiasi kikubwa amefanikiwa katika kutumia mbinu mbalimbali za kifani katika kazi yake. Mbinu za kifani ambazo tumezishughulikia katika sura hii ni matumizi ya lugha, tamathali za usemi, taswira, uhuru wa mtunzi, muundo na mandhari. Tumechunguza mbinu hizi kwa kuzieleza na kuonyesha jinsi zilivyotumika katika *Maulidi ya Nuni.*

## 4.3 MATUMIZI YA LUGHA

Katika sura ya pili tumeeleza kwamba lugha huundwa na msamiati na msamiati ni jumla ya maneno yanayopatikana katika lugha. Ni nyenzo ya kimsingi aliyo nayo mwandishi na ina nafasi na umuhimu mkubwa katika utunzi na uandishi wake. Baadhi ya matumizi ya lugha yaliyojitokeza katika kazi hii ni lahaja ya Kiamu, Kingozi na maneno ya Kiarabu.

### 4.3.1 LAHAJA YA KIAMU

Lugha iliyotumika katika utungo huu ni lahaja ya Kiamu. Katika ubeti wa 4, mtunzi amesema:

K'azitegemea nuru mbili na nuru nami
t'awafasiria kwa Kiamu walo kana-mi
tuziyue swifa za Mtumi nasi 'Ajami
wakifika taji Barazanji na mimi tena

Lahaja hii huzungumzwa sehemu za Amu au Lamu ambacho kilikuwa kituo cha usomi kabla ya karne ya ishirini hadi sasa ndio maana mtunzi akatumia lahaja hii. Katika lahaja hii, kuna tofauti za kifonetiki zilizojitokeza kama tulivyoeleza.

**Mifano ya maneno katika lahaja ya Kiamu**

| **Lahaja ya Kiamu** | **Kiswahili Sanifu** | **Ubeti** | **Tofauti za kifonetiki** |
|---|---|---|---|
| Tuziyue | tuzijue | 4 | Matumizi ya sauti /y/ badala ya /j/ |
| Muyukuu | mjukuu | 3 | Matumizi ya sauti /y/ badala ya /j/ |
| Moya | moja | 3 | Matumizi ya sauti /y/ badala ya /j/ |
| Amekuya | amekuja | 129 | Matumizi ya sauti /y/ badala ya /j/ |
| Yina | jina | 17 | Matumizi ya sauti /i/ badala ya j |
| Katukua | kachukua | 38 | Matumizi ya sauti /t/ badala ya/ch/ |
| Utungu | uchungu | 42 | Matumizi ya sauti /t/ badala ya /ch/ |
| Mato | macho | 45 | Matumizi ya sauti/t/ badala ya /ch/ |
| Mtana | mchana | 55 | Matumizi ya sauti /t/ badala ya /ch/ |
| Wanda | wanja | 45 | Matumizi ya sauti /nd/ badala ya /nj/ |
| Ndia | njia | 113 | Matumizi ya sauti /nd/ badala ya /nj/ |
| Ziumbe | viumbe | 29 | Matumizi ya sauti /z/ badala ya /v/ |

Mifano mengine ya lahaja ya Kiamu katika utungo huu ni kama vile **kwanda** badala ya kwanza (ubeti wa 2), **kabula** badala ya kabla (ubeti wa 2), **mtumi** badala ya mtume (ubeti wa 2), **kyenda** badala ya akenda (ubeti wa 8), **zema** badala ya mema (ubeti wa 8), **hini** badala ya hii (ubeti wa 113), **nyezi** badala ya miezi (ubeti wa 48), **akamuatia** badala ya kumuachia (ubeti wa 10), **mwida** badala ya muda (ubeti wa 55), **wanda** badala ya wanja (ubeti wa 45).

### 4.3.2 KINGOZI

Kama tulivyoelezea katika sura ya pili, Kingozi ni Kiswahili cha kale. Baadhi ya tungo zilizotumia kingozi ni pamoja na utendi wa *Masahibu*, utendi wa *Siu*, utendi wa *Wajiwaji*, *Takhmisa ya Liyongo*, halikadhalika kasida ya *Hamziya*. Kuna miundo ya kisarufi ambayo si ya kawaida kama vile muundo wa vitenzi vya wakati uliopita vya Kibantu, maneno yenye asili ya Kibantu ambayo yamechakaa kabisa na hayapatikani tena katika Kiswahili cha kisasa. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya miundo ya kisarufi iliyopatikana katika kazi hii ambayo ni ya Kingozi japokuwa imetajwa kwa uchache sana.

**Mifano ya maneno ya Kingozi**

| Kingozi | Kiswahili Sanifu | Ubeti | Miundo ya Kisarufi |
|---|---|---|---|
| Anitengeleze | anitengenezee | 27 | Matumizi ya e/le kuashiria wakati uliopita |
| Nilikufumie | ulemee | 1 | Matumizi ya e/le kuashiria wakati uliopita |
| Ulemeze | nilifuma | 1 | Matumizi ya e/le kuashiria wakati uliopita |

Maneno mengine ya Kingozi yaliyopatikana katika utungo huu ni kama yafuatavyo: pote-uzi, unudhuma- unaosema (ubeti wa 1), wamba- wasema (ubeti wa 41), Moliwa- Mola (ubeti wa 47), wambeja- wazuri (ubeti wa 70), wakifika taji- wakivishwa taji (ubeti wa 4), kyenda- akenda (ubeti wa 8), mbwako- ni wako (ubeti wa 48), siyapulika- sijasikia (ubeti wa 48). Ulemeze- uliolemea (ubeti wa 1), tutamnena- tutamsema (ubeti wa5), moya-moja (ubeti wa 7), anitengeleze (ubeti wa 27).

### 4.3.3 MANENO YA KIARABU

Katika kazi hii, kuna maneno mengi ya Kiarabu ambayo yanatupa taarifa kuhusu mtunzi kwamba aliathirika na lugha ya Kiarabu na dini ya Kiislamu. Kwa mnasaba huu, maneno mengi ya Kiarabu yametoholewa ili yasipoteze maana yake halisi ikikumbukwa kwamba maneno haya yanapatikana katika Qur'an tukufu ambacho ni Kitabu cha Allah ( S.W.T.). Hali hii vilevile, inatosheleza kusema kwamba hakuna tafsiri ya moja kwa moja ya maneno haya isipokuwa katika mikabala ya Uislamu ambapo imeruhusiwa kisheria.

**Baadhi ya maneno ya kiarabu yaliyojitokeza katika kazi hii ni kama yafuatayo:**

| Manaeno ya Kiarabu | Kiswahili Sanifu | Ubeti |
|---|---|---|
| Ajami | jamii ya Kiislamu | 4 |
| Sayidi | kiongozi/ Mtume Muhammad (S.A.W.) | 5 |
| Humidi | kumtukuza Mwenyezi Mungu | 6 |
| Salati | swala/ maombi | 6 |
| Munkar | Malaika mwenye kuuliza maswali kaburini | 8 |
| Dinar | pesa alizoachiwa kijana aliefiwa na mamake | 10 |

| | | |
|---|---|---|
| Khatima | mwisho/ kijana alikaa katika kisomo cha maulidi haya hadi mwisho | 11 |
| Qiyamah | siku ya malipo ambapo kijana aliota amefufuliwa | 11 |
| Kulla | kila/Mwenyezi Mungu ampe kijana aliyesoma maulidi haya kila mema | 13 |
| Fatiha | sura ya kwanza katika Qur'an Tukufu | 16 |
| Asma-ul-Husna | majina tisini na tisa ya Mwenyezi Mungu | 17 |
| Jalla Jallal | aliye juu ambaye ni Mtukufu na husifiwa katika maulidi haya | 17 |
| Ikhlas | kutakasa nia maulidi haya yanaposomwa iwe ni kwa ajili ya Allah | 19 |
| Ihsan | kumuamini Mola kama ambaye wamuona ikiwa humuoni anakuona | 21 |
| Sala na tahiya 22 | maombi na salamu yamfikie Mtume (S.A.W.) | 22 |
| Musharafu | aliyetukuzwa ambaye ni Mtume (S.A.W) | 24 |
| Dhuria | kizazi cha Mtume (S.A.W) | 24 |
| Mutatahirin | waliotakasika kwa kumfuata Mtume (S.A.W.) | 24 |
| Akrabu | jamaa waliokuwa wa karibu kwa Mtume (S.A.W.) | 24 |
| Sahaba | wafuasi wa kwanza wa Mtume (S.A.W.) | 24 |
| Muhajirun | wafuasi wa Mtume (S.A.W) waliohama kutoka Makka hadi Madina | 24 |
| Ansar | wafuasi wa Mtume (S.A.W) walioishi Madina na waliowapokea Muhajiru | 24 |
| Taufiki | mafanikio mtunzi anamuomba Mola amjaalie mazuri | 26 |
| Nasirina | mwenye kunusuru/ mtunzi anamuomba Mola amnusuru | 27 |
| Auni | usaidizi/ Mtunzi anamuomba Mola amsaidiye kutafsiri maulidi | 27 |
| Karim | jina mojawapo la Mwenyezi Mungu aliye mkarimu | 28 |
| Musitafa | aliyechaguliwa ambaye ni Mtume (S.A.W.) | 28 |
| Rabbana | Mwenyezi Mungu | 32 |
| Haram | isiyoruhusiwa/ kukubaliwa katika dini ya Kiislamu | 33 |
| Nikah | ndoa/ watoto wa Mtume (S.A.W.) walizaliwa katika ndoa ya Kiislam | 33 |

| | | |
|---|---|---|
| Allah Rabuka | Mwenyezi Mungu aliye mkubwa | 36 |
| Mu'minina | wafuasi walioongoka ambao walimfuata Mtume (S.A.W) | 36 |
| Imamu | kiongozi katika dini ya Kiislamu | 37 |
| Arsh | mwenye kiti cha enzi ambaye ni Mola Mtukufu | 38 |
| Waliwalidayya | wazazi wawili wa Mtume (S.A.W.) | 38 |
| Sayidatina | wanawake wawili waongofu waliohudhuria mazazi ya Mtume | 43 |
| Hurulain | wanawake wema na wazuri wa peponi | 43 |
| Nabia | nabia aliyechaguliwa na Mwenyezi Mungu, Mtume Muhammad (S.A.W.) | 61 |
| Maulana | Mwenyezi Mungu | 61 |
| Aziz | mwenye nguvu na ni jina mojawapo la Mwenyezi Mungu | 67 |
| Baitul Mukaddas | msikiti ulioko Jerusalem | 81 |
| Jibril | malaika aliyepeleka wahyi kwa Mtume (S.A.W.) | 82 |
| Dhuha | wakati kabla ya adhuhuri | 90 |
| Wallahi | Mwenyezi Mungu ni mmoja | 94 |
| Billahi | kwa ajili ya Mwenyezi Mungu | 94 |
| Subhana | aliyetakasika ambaye ni Mwenyezi Mungu | 105 |
| Shari | mabaya ambayo mtunzi anaomba aepushwe nayo | 114 |
| Maghfira | mtunzi anaomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu | 115 |
| Rasul | mitume waliopewa vitabu vitakatifu na Mwenyezi Mungu | 123 |
| Ulul Azm | mitume waliopata misukosuko mingi lakini walisubiri | 123 |
| Malik | malaika wa motoni | 123 |
| Ridhwan | malaika wa peponi | 123 |
| Ulama | wasomi katika dini ya Kiislamu | 126 |
| Tammati | mwisho wa utungo huu | 127 |
| Dua | maombi ambayo mtunzi anamalizia katika utungo | 128 |
| Janna | pepo ambayo mtunzi anawaombea wafuasi wa Mtume (S.A.W.) | 130 |

Kwa kuwa haya Maulidi ya Nuni ni kipengele cha kidini, mtunzi hakuwa na budi kutumia msamiati wa Kiarabu.

## 4.4 TAMATHALI ZA USEMI

Katika sura ya pili tumeeleza kuwa tamathali za usemi ni dhana inayotumiwa kuelezea mbinu za matumizi ya lugha ambazo kimsingi zinahusisha ukiushi au ukiukaji wa aina fulani ambapo neno au kifungu hutumiwa kwa maana ambayo ni tofauti na maana ya kimsingi. Tamathali za usemi hurejelea mbinu ambayo inahusisha maana na kuna maana ambayo haiko wazi na ambayo msomaji anahitaji kufikiri kwa kina ili aweze kuielewa.

Katika kazi hii, mtunzi ametumia tamathali za usemi tofauti tofauti ambazo kwa kiasi fulani zinaingiliana na vilevile kutofautiana kwa njia moja au nyengine. Mtunzi vilevile ametumia ukiushi mwingi ambao ni uvunjaji wa kaida za lugha kimakusudi ili kubuni njia mpya za kujieleza. Tamathali za usemi tulizozishughulikia ni takriri, tashbihi, istiari, uhuishaji/tashihisi pamoja na chuku.

### 4.4.1 TAKRIRI

Mbinu hii hutumiwa na mtunzi ili kusisitiza ujumbe aliokusudia kwa hadhira lengwa na hali hii humfanya mtu atafakari. Katika mbinu hii, mtunzi husisitiza kimakusudi ili ujumbe uwe na athari kwa msomaji. Vilevile mtunzi hurudia sauti fulani za konsonanti, irabu, neno au maneno katika mshororo ili kusisitiza jambo au kuteka nadhari ya msomaji.

Baadhi ya takriri za maneno ambazo mtunzi amezitumia katika kazi hii ni kama vile salamu ya **radhi radhi** yake izifunike. Mtunzi anamuomba Mwenyezi Mungu awape baraka zisizo na mwisho wafuasi wa Mtume Muhammad (S.A.W.) (ubeti wa 23), ngwatwokoa nasi Mola **wetu na wetu** wana. Mtunzi anamuomba Mwenyezi Mungu awanusuru pamoja na vizazi vyao (ubeti wa 37), kyombo kyaloyaa **tamu tamu** isotukiwa- chombo kilichokuwa kimejaa kinywaji kitamu alichopewa mamake Mtume (S.A.W.) wakati wa machungu ya mazazi yalipozidi (ubeti wa 44), na **uladha** wake ni **uladha** hawayaona- ladha ya kinywaji kitamu alichopewa bi. Amina ambacho ladha yake haijawahi kuonjeka (ubeti wa 44), haku mtukufu **kamwe kamwe** baba na mama- hakuna aliyekuwa mtukufu ila Fatuma ambaye alikuwa mamake Husseini ( ubeti wa 55 ), kuyua swifazo **njema njema** ziumbe pia- ni muhimu kwa wafuasi wa Mtume (S.A.W.) kuzijua sifa zake (ubeti wa 52), **kazipita pita** mbingu zote na mapazia- wakati wa safari ya kwenda mbinguni Mtume (S.A.W.) alipita uwingu mmoja hadi mwengine mpaka uwingu wa saba (ubeti wa 84), kulla **yema yema** lihusiwe nda Maulana- mambo yote mema yanahusishwa na Mwenyezi Mungu (ubeti wa 93), napenda **mapendi na**

**mapendi** yangumi haya- mtunzi anasisitiza kuhusu umuhimu wa kumpenda Mtume (S.A.W.) na aliyokuja nayo pamoja na kupenda mauti (ubeti wa 102), maulidi haya **kweli kweli** yamesazani- maulidi haya yameangazia mambo mengi yakiwemo mazazi ya Mtume (S.A.W.) na pia safari yake ya kwenda mbinguni na kupewa nguzo ya swala (ubeti wa 128), **amina amina** tuinene thumma **amina-** mtunzi anamuomba Mwenyezi Mungu aitikie maombi ya waumini wake (ubeti wa 128).

Mtunzi ameanza na takriri ya neno au maneno katika baadhi ya beti, lengo kuu likiwa ni kusisitiza jambo alilotaka kufikisha kwa hadhira yake. Kwa mfano katika ubeti wa 47, mtunzi ameanza na neno **ewe** kutoka mshororo wa kwanza hadi wa tatu kusisitiza utukufu wa Mtume Muhammad (S.A.W.) kutoka kwa Mwenyezi Mungu kuwa ndiye kipenzi chake.
Mtunzi amesema :

**Ewe** muhubiri kulla siri salamu ndako
**ewe** walotumwa kwa rehema salamu kwako
**ewe** walopendwa umependa Moliwa wako
na salamu hushukia kwako dawama(ubeti wa 47)

Pia katika ubeti wa 49, mtunzi ameanza na takriri ya maneno **wewe ndiwe** katika mshororo wa kwanza na wa pili kusisitiza kuwa Mtume Muhammad (S.A.W.) ni jua, mwezi na nuru kutokana na utukufu na tabia zake ambapo wafuasi wake wanasoma kupitia kwake kwa kupata mengi kuhusu Uislamu. Katika ubeti wa 100, neno **wala** limerudiwa katika mshororo wa kwanza na wa pili kusisitiza kuwa wafuasi wa Mtume (S.A.W.) hawakomi wala hawatakoma kumpenda Mtume (S.A.W.).

Mtunzi ametumia takriri ya vina katika mistari mitatu ya mwanzo katika baadhi ya beti ili kufuata arudhi kupata kina. Takriri ya vina inajitokeza katika vina vya mwisho. Mifano ya takriri ya vina ni kama vile katika ubeti wa 1 ambapo kina ma kimerudiwa katika mshororo wa kwanza hadi wa tatu. Vilevile katika ubeti wa 2, kina ni kimerudiwa katika mshororo wa kwanza hadi wa tatu, na pia kina ti kimerudiwa katika ubeti wa 125. Mtunzi amesema:

Nilikufumie kwa upote wa unudhu**ma**
nguo wa sanaa nakishiye hawakufu**ma**
fikirani mbili ya hadhiki na njinga nya**ma**
ulemeze durra utungowe pakalingana (ubeti wa 1)

Kwanda kwa ibada ni kusoma kwa Kurua**ni**
maneno ya Mungu tangulizi ni Fatiha**ni**

kabula kuswifu yakasomwe kwa hadhara**ni**
sala za Mtumi na salamu za Maulana (ubeti wa 2)

Wakazainisha majilisi kwa abia**ti**
kitukufu mno kifungokye kya madiha**ti**
kitunga kwa uzi wa Johari kukidhibi**ti**
kiswifu Mtume munshidi na salihina (ubeti wa 125)

Mtunzi vilevile ametumia takriri sauti. Mfano mzuri unajitokeza katika ubeti wa 53 wakati mtunzi anaposisitiza kuwa viumbe dhaifu na wanyonge wote hutaraji malipo kutoka kwa Mwenyezi Mungu kupitia kwa aliyoyaleta Mtume (S.A.W.).

**Dhalilu dhaifu** hutaraji **fadhili nyingi**
**ungiwe ni ungi** na ziumbe **hawauwangi**
hutumiminia kama seli wala **hayongi**
tupe ukitupa **mazoweya yongeze** tena

Vilevile mtunzi ametumia takriri sauti katika ubeti wa 66 anaposisitiza kuhusu kukua kwa Mtume (S.A.W) ambapo kulikuwa na maajabu chungu nzima.

Mwendewa na **sala na salamu alikikua**
na **kukua kwake ni ajabu isosikiwa**
**hupita zijana walishwao kama za ndiwa**
ni ajabu **kuu kukuakwe** walomuona

### 4.4.2 TASHBIHI/TASHBIHA

Mbinu hii huitwa tashbihi, tashbiha au mshabaha na ni lugha ya ulinganishaji. Vitu viwili halisi vinavyolinganishwa huwa vinaonyesha mshabaha fulani wa sifa sura au tabia. Mbinu hii hususan hutumia maneno kama, mithili ya, ni sawa na, ni kama, kana kwamba, kama vile, ja, mfano wa, utadhani, utafikiri na kadhalika.

Katika ubeti wa 58 mtunzi anafananisha uso wa Mtume (S.A.W.) kama jua na mwezi. Maelezo haya yanatupa undani kuhusu Mtume (S.A.W.) kwamba yeye ni kiongozi mtukufu aliyechaguliwa na Mwenyezi Mungu kuongoza wafuasi wake katika kufuata na kutekeleza amri za Mwenyezi Mungu. Jua na mwezi hutoa mwangaza ambao aghalabu huwapa watu mwangaza wa kutekeleza walioamrishwa. Kwa vile Mtume Muhammad (S.A.W.) amekamilika kidini na kitabia, hali hii imechangia kwa wafuasi wake kumuenzi na kumfuata ili wapate kuongoka duniani na ahera. Vilevile mtunzi amesema: Kavaa furaha kama kanzu ilo nzuri. Mtume (S.A.W.) anafananishwa na mtu anaye vaa vazi zuri kwani humfanya

kujiamini licha ya kupata misukosuko kutoka kwa jamaa zake wa karibu wakiwemo baadhi ya Makureishi ambao walipinga yote aliyowaeleza ikiwemo safari yake ya kwenda mbinguni. Mtunzi amesema:

Alipoiona nuru illahi ikinawiri
Uso huzagaa kama yua au kamari
kavaa furaha kama kanzu ilo nzuri
zishali ziwili kazivaa zizuri sana (ubeti wa 58)

Katika ubeti wa 53, mtunzi ametueleza kwamba, walo dhaifu na wanyonge hutaraji fadhila nyingi kutoka kwa Mtume (S.A.W.) ambapo fadhila hizi huwafikia kama seli na huzidi mapenzi yanapozidi. Maelezo haya yanadhihirisha kuwa malipo ya kumfuata Mtume (S.A.W.) ni mengi sana. Kwa kufuata na kutekeleza aliyoyaleta Mtume (S.A.W.), wafuasi wake watafaidika duniani na ahera kwa kulipwa mema na Mwenyezi Mungu. Kuthibitisha maelezo haya mtunzi amesema:

Dhalilu dhaifu hutaraji fadhili nyingi
ungiwe ni ungi na ziumbe hawauwangi
**hutumiminia kama seli wala hayongi**
tupe ukitupa mazoweya yongeze tena.

Katika ubeti wa 66, mtunzi anatupa maelezo kuhusu kukua kwa Mtume (S.A.W.) ambapo kulikuwa na maajabu kwa waliomuona ambapo kukua kwake hakuwezi kulinganishwa na hushinda makinda ya njiwa jinsi wanavyolishwa. Maelezo haya yanadhihirisha kuwa kukua kwa Mtume (S.A.W.) hakuwezi kufananishwa na vijana wengine waliokuwa na umri sawa na Mtume (S.A.W) kwa sababu alikuwa kiumbe mtukufu. Mtunzi anasema:

Mwendewa na sala na salamu alikikua
na kukua kwake ni ajabu isosikiwa
**hupita zijana walishwao kama za ndiwa**
ni ajabu kuu kukuakwe walomuona

Kulingana na ubeti wa 67, mtunzi ametueleza kuwa Mtume (S.A.W.) alikua kwa haraka na kwa siku moja ilikuwa kama mwezi, pia alitembea kwa haraka ikilinganishwa na watoto wengine waliokuwa umri sawa na yeye. Jambo hili linathibitisha kuwa alikuwa kiumbe mtukufu. Mtunzi anasema:

Kukua kwa Tumwa siku moja ni kama mwezi
wa mwana mungine alijua ali azizi
na nyezi mitatu ikitimu kwa muombezi
alishua guu kainuka si kama wana

### 4.4.3 ISTIARI

Katika mbinu hii mtunzi hulinganisha au kuhusisha vitu viwili tofauti kimaumbile na kitabia kwa kutumia neno 'ni', ja, mfano wa, mithili ya. Mbinu hii aghalabu hujenga picha au taswira kwa msomaji na pia huweza kufumba maana ili kutilia mkazo jambo linaloelezewa.

Kulingana na ubeti wa 4 na 35, Mtume (S.A.W) analinganishwa na nuru, kuonyesha kuwa yeye ni kiumbe mtukufu aliyewaonyesha wafuasi wake njia ya sawa kwa kufuata aliyoamrishwa na Mwenyezi Mungu na kuepuka makatazo yake. Mtunzi katika ubeti wa 4 mshororo wa kwanza anasema:

**Kazitegemea nuru mbili ni nuru nami**

Vilevile wema wake umelinganishwa na nukato maungoni mwake lililotoa harufu nzuri na muangaza ulotoka ndani ya kifua chake kuonyesha kuwa wema wa Mtume (S.A.W.) umeenea kwa wafuasi wake ambao wanamfuata na kutekeleza walioamrishwa na Mwenyezi Mungu.

Katika ubeti wa 36, Mtume analinganishwa na kiumbe alotoka kwenye matumbo safi ya mamake Amina na vilevile Mola ameitukuza mimba hii kwani tayari wazazi wake wawili walikuwa wameshatukuzwa. Maelezo haya yanaonyesha utukufu wa Mtume (S.A.W) kuanzia matumboni mwa mamake. Mtunzi amesema:

Ikyendea nyengo ya Sayidi mwenye baraka
**Matumboni safi ya sayida yalo safika**
ameiongoa Mola wetu Alla Rabuka
walidani wali wo wawili muminina(ubeti wa 36)

### 4.4.4 UHUISHAJI/ TASHIHISI

Katika mbinu hii,vitu au hali isiyokuwa na uhai hupewa sifa za uhai au aghalabu sifa za kibinadamu. Katika kazi hii, mtunzi amefanikiwa katika kutumia mbinu hii kwa kuvipatia vitu vyenye uhai kama vile wanyama, miti sifa za kibinadamu.

Katika  ubeti wa 40 na 41, wanyama wa Makureishi waliweza kuzungumza na kusifu mimba ya Mtume (S.A.W) pindi mamake alipopata ujauzito na kadri miezi ilivyozidi kusonga wanyama hawa waliendelea kuizungumzia na kunadi kwamba mimba hiyo ilikuwa bahati kwa walimwengu. Wanyama hawa walipewa sifa ya kuzungumza na ajabu ni kuwa, wanyama hawa hata walikuwa wanalitaja jina la Mtume (S.A.W) kuthibitisha kuwa walikuwa na ufahamu kuhusu kiumbe huyu mtukufu na yote haya ni kwa rehema zake Mwenyezi Mungu.Mtunzi anasema:

Na kwa mimba yake walinena wakisikiwa
nyama za Kureshi kwa fasaha wakatongoa
mimba ya Mtume yeo hapa imetukua
kumekurubia kudhihiri kwa sayidina

Na kwa kula mwezi wa mimbaye walikinadi
nyama za Kureshi wamba mimba ya Ahamadi
kudhihiri kwake duniyani kila suudi
Malaki mbinguni waradidi na kuyanena

Katika ubeti wa 51 mtunzi anatueleza kuwa hata kigogo cha mtende kilichokuwa kikavu kililia seuze wanadamu, wote wakitaradhilia nusura au kuokolewa kutoka kwa Mola Mtukufu kupitia kwa kiumbe aliyesifika ambaye ni Mtume (S.A.W).  Pia paa alikuwa amefumbata na kutafuta nusura kutoka kwa Mtume (S.A.W.)  Maelezo haya yanatupa undani kuhusu cheo cha Mtume (S.A.W) kwamba vilivyomo ardhini vilitaraji nusura kutoka kwa Mtume (S.A.W.)  ikiwemo miti na wanyama. Mtunzi anasema:

Kigogo kikavu kya mtende hukulilia
na paa mkenge utefuwe mekushikia
wataka nusura wote hao kwako Nabiya
fa kaifa sisi ya Illahi unusuruna (ubeti 51)

Mtunzi vilevile anatupa habari kwamba hata majabali yaliyokuwa Makka yalimwambia Mtume (S.A.W) yatabadilika yawe dhahabu ili awe tajiri, lakini alikataa kata kata azma yake kuu ikiwa ni pepo ya Mwenyezi Mungu. Katika ubeti wa 98, mtunzi anasema:

Yalitaka naye majabali yaliyo Maka
yaliyo makuu humwambia tutageuka
tuwe ni dhahabu utumie utakotaka
kajibu sitaki epukani nataka janna

Maelezo haya yanatosheleza kuwa mtunzi amefikisha ujumbe kuhusu mazazi ya Mtume (S.A.W) kwa kutumia ufundi wake wa lugha na hii ndio azma kuu ya utungo huu.

### 4.4.5 CHUKU

Hii ni tamathali ya usemi inayoeleza hali ya sifa za kitu kuelezwa kwa namna inayokuza sifa zake au kuzidunisha sifa hizo kuliko hali yake ya kawaida. Kwa msingi huu basi huwa pana ukinzani kati ya hali inayosemwa na ukweli wenyewe. Maelezo haya ni kulingana na Wamitila (2008). Katika kazi hii, tumeelezwa katika ubeti wa 8, 9 na 10 kuwa kusoma maulidi haya kuna faida za duniani na ahera. Faida za duniani ni kuwa mtu atapata baraka na bahati mwaka mzima na ataepushwa na balaa za moto na wizi na atakapoondoka ulimwenguni itakuwa rahisi kwake kujibu maswali atakayoulizwa na malaika Munkar atakapokuwa kaburini, vilevile atafufuliwa na mitume na mashahidi. Maelezo haya yanakinzana na mafunzo ya dini ya Kiislamu ambayo yanasisitiza kuwa baraka zote hutoka kwa Mwenyezi Mungu kupitia kufanya vitendo vyema ambavyo vinasisitizwa katika nguzo tano za Uislamu na pia nguzo sita za Iman. Vilevile kuweza kujibu maswali kaburini hutegemea vitendo vyema alivyofanya kiumbe akiwa duniani na pia kufufuliwa na mitume na mashahidi hutegemea vitendo vyema vya mja na pia rehema zake Mwenyezi Mungu.

Mtunzi ametueleza kuhusu kukua kwa Mtume (S.A.W.) ambako kulijaa maajabu chungu nzima. Alipokuwa na miezi mitano alitembea na mwezi wa tisa alianza kuzungumza kwa ufasaha ambapo aliwashinda watoto wengine waliokuwa umri sawa na yeye. Maelezo haya kwa hakika ni chuku kwani haimkiniki kwa mtoto wa miezi mitano kuwa anatembea na miezi tisa anazungumza kwa ufasaha (ubeti wa 67).

## 4.5 TASWIRA/ JAZANDA

Kama tulivyoeleza katika sura ya pili, jazanda ni neno ambalo hutumiwa kurejelea ile hali ya kutumia picha au taswira katika kazi ya kifasihi. Taswira au jazanda zaweza kuwa za kimaelezo au za kiishara. Jazanda za kimaelezo huweza kuundwa kutokana na maelezo ya msimulizi hususan mtunzi anapoeleza kitu fulani ambapo msomaji huweza kujenga picha kutokana na maelezo yenyewe. Jazanda za kiishara huweza kuunda picha kwenye akili ya msomaji lakini taswira au picha hizo huwa na maana nyengine ya ziada.

Katika *Maulidi ya Nuni* taswira au jazanda inajitokeza hususan katika kazi yote. Awali tunaelezwa jinsi mambo yanavyotakikana wakati wa kusomwa maulidi. Katika ubeti wa 2, mtunzi anatueleza kwamba kabla ya kusoma maulidi, ni muhimu kuanza na kisomo cha Kur'ani kwa kuanza na suratul Fatiha na maulidi yenyewe yasomwe hadharani. Kulingana na

maelezo haya, tunapata taswira ya kuweko kwa mkusanyiko wa watu waliokaa sehemu iliyo wazi huku wakisoma suratul Fatiha kabla ya kuanza kisomo cha maulidi haya.

Katika ubeti wa 10 na 11 tunapata taswira ya kijana ambaye alikuwa amefiliwa na wazazi wake na kuachiwa kidinari, katika pita pita zake aliona watu wamekaa hadharani wakisoma maulidi. Kijana huyu aliamua kukaa katika kikao hicho na alipolala aliota amefufuliwa siku ya kiama akiwa janna na jamaa wote aliokuwa nao katika kikao hicho. Baadaye kila mmoja alipewa nyumba lakini kijana huyu aliona nyumba nyengine ambayo ilikuwa nzuri zaidi na akaitamani, alielezwa kwamba nyumba iliyokuwa nzuri zaidi ilikuwa ni ya wale ambao husoma maulidi. Kulipopambauka, kijana huyu aliandaa maulidi akitumia kidinari alichokuwa ameachiwa na mama yake akizingatia sharuti zote za maulidi na alipolala alimuota mama yake akimuombea Mungu amjaze heri na pia alimtia manukato na hatimaye wakabusiana. Vilevile mtunzi anatupa taswira kuhusu maandalizi ya kusoma maulidi haya, kuwa ni muhimu mtu atie nia, avae nguo nzuri na atie manukato ili kisomo hiki kikubaliwe. Maelezo haya yamo  katika ubeti wa 16 na unaweza kupata picha akilini ya haya yote.

Wakati wa mimba ya Mtume (S.A.W.) ilipotimia, Amina alihisi machungu na tunaelezwa kwamba wanawake wanne ambao uzuri wao haujawahi kuonekana ulimwenguni walihudhuria mazazi haya wakiwemo wawili wa duniani na wawili wa peponi. Maelezo haya yanatupa taswira ya jinsi mazazi ya Mtume (S.A.W.) yalivyotukuzwa kwa kuhudhuriwa na kushughulikiwa na viumbe vitukufu ( ubeti wa 42, 43 na 44 ).

Taswira inajitokeza pindi Mtume alipozaliwa, alichemua na kutaja jina la Mwenyezi Mungu na malaika nao wakamuombea rehema kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Baadaye babu yake aliyekuwa na furaha tele alimchukua mjukuu wake na kumpeleka katika Al Kaaba na kumuombea Mungu ili amhifadhi na balaa na kila hasadi. Maelezo haya yanatupa picha akilini ya jinsi Mtume (S.AW.) alivyochukuliwa na babu yake na kufanyiwa maombi maalum katika Al Kaaba. Mtunzi anasema:

> Kwalikuya T'umwa kwa bibiye kamubashiri
> kinenda upesi kwa Amina mwenye fahari
> alipomuona muyukuwe alishukuri
> akafurahika furahaze ni nyingi sana ( ubeti wa 57 )
>
> Kamtia  T'umwa  Ka' abani  kimuombea
> akamulindaye kwa baiti na baa pia
> hasidi baghidhi muyukuwe ngwamuondolea
> akue kwa siha na afiya wake kijana ( ubeti wa 59 )

Mtume alinyonyeshwa na mamake kwa muda wa siku saba, baadaye alichukuliwa na Thuweba Juruthumi na watatu wao alikuwa ni Halima ambaye japo kifua chake kilikuwa kikavu, Mwenyezi Mungu kwa rehema zake alijaalia kifua chake kujaa maziwa na hivyo kuweza kumnyonyesha Mtume bila shida. Maelezo haya yanatupa taswira ya jinsi Mtume (S.A.W.) alivyopitia katika mikono ya wanyonyeshaji mbalimbali na pia taswira ya jinsi maziwa yalivyokuwa yamejaa hususan kwa bi. Halima ambaye awali kifua chake kilikuwa hakina maziwa (ubeti wa 64 na 65).

Katika ubeti wa 66, 67, na 68 tunasawiriwa kukua kwa Mtume (S.A.W.) ambako kulikuwa kwa maajabu, tunapewa maelezo kwamba alikuwa anakua kwa kasi sana kuliko watoto wengine waliokuwa wakilishwa kama watoto wa njiwa. Kwa siku moja kukua kwake kulikuwa kama mwezi na kwa muda wa miezi mitatu alikuwa tayari keshashika guu. Katika mwezi wa tano alikuwa tayari ameanza kutembea na katika mwezi wa tisa alikuwa akizungumza kwa ufasaha. Kulingana na maelezo haya, mtu anapata picha ya jinsi Mtume (S.A.W.) alivyokuwa akikua kwa kasi.

Mtume (S.A.W.) alipokuwa anarejea kutoka safarini, kuna taswira ya jinsi Khadija alivyokuwa juu ghorofani akiwa pamoja na rafiki zake akiwemo Maisara pamoja na wanawake wema. Pia kuna taswira inayojitokeza wakati Maisara alipotumwa na Khadija kwa Mtume apate kumuoa (ubeti wa 70, 71,72, 73 na 74).

Mtunzi vilevile anatupa taswira ya jinsi hali ya Mtume (S.A.W.) ilivyokuwa wakati wa kupewa wahyi kutoka kwa Mwenyezi Mungu, mwanzoni zilikuwa ndoto za kweli lakini baadaye alizoea (ubeti wa 77) lakini maelezo haya ni finyu sana kwani kulingana na Qureish (2008), ndoto hizi zilimuogopesha Mtume sihaba alipokuwa katika jabali la Hiraa ambapo alikimbilia kwa mke wake Khadija akimwambia amfinike. Khadija alimfinika na kumpa moyo na baadaye alizoea. Huu ndio wakati ambapo Malaika Jibrili alimpa Mtume wahyi kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwamba yeye ni Mtume.

Safari ya Mtume (S.A.W.) kwenda mbinguni nayo inatupa taswira za kiajabu. Kwa rehema zake Mola, aliongozwa na malaika Jibrili kupitia msikiti wa Mukadasi ambapo taswira inajitokeza wakati alipowakusanya malaika na manabii pamoja na majini na akawaongoza katika sala. Kutoka sehemu hii, Mtume (S.A.W.) alipanda ngazi na kupita uwingu mmoja hadi mwengine mpaka uwingu wa saba ambapo aliweza kukabidhiwa nguzo ya swala na

Mwenyezi Mungu (ubeti wa 81 hadi 85). Katika *ukawafi wa Miiraji* taswira inajitokeza wakati Mtume (S.A.W.) alivyoonyeshwa yote yaliokuwa yakifanyika kutoka uwingu wa kwanza hadi wa saba na pia alivyoonyeshwa pepo na moto na yote yaliyokuwa yakifanyika, yakiwemo adhabu za motoni na starehe katika pepo ya Mwenyezi Mungu. Pia kuna taswira ya jinsi Mtume (S.A.W.) alivyokutana na Mitume wengine katika kila uwingu na vilevile walivyomrai kurudi kwa Mwenyezi Mungu azipunguze swala kutoka hamsini hadi tano lakini malipo yake ni sawa na kuswali swala hamsini.

Taswira ya Abubakar nayo haikusahauliwa, ikizingatiwa kuwa alikuwa pamoja na Makureishi wengine akiwemo Abu Jahal. Wote waliokuwa katika mkusanyiko huo hawakumuamini Mtume (S.A.W.) aliyoyasema isipokuwa Abubakar ( ubeti wa 86 ). Maelezo haya yanatupa taswira jinsi mambo yalivyokuwa wakati huo.

## 4.6 UHURU WA MTUNZI

Katika utungo huu, mtunzi vilevile ametumia uhuru wa mtunzi ambacho ni kibali walichonacho watunzi wa tungo kutumia miundo, msamiati au mpangilio wa lugha kisanaa na kukiuka misingi ya lugha kwa lengo la kujenga utungo wao. Mtunzi ana uhuru wa kutumia lugha ya mkato, kurefusha maneno, kufupisha maneno, kubadilisha tahajia n.k. Kulingana na utungo huu, mtunzi ametumia inkisari, tabdila na mazida ili kufanikisha maudhui yake.

### 4.6.1 INKISARI

Katika sura ya pili, tulieleza inkisari kama ufupishaji wa maneno katika tungo. Mbinu ya inkisari imetumika katika *Maulidi ya Nuni.* Mtunzi ametumia inkisari ili kuleta utoshelezo wa mizani katika mshororo. Vilevile mtunzi amekiuka kaida za Kiswahili sanifu katika viwango vya kimofolojia na kifonolojia. Mifano ya inkisari katika kazi hii ni kama ifuatayo:

**Mifano ya inkisari**

| INKISARI | KISWAHILI SANIFU | UBETI |
|---|---|---|
| Utungowe | utungo wake | 1 |
| Kifa | akifa | 5 |
| Nafuuye | nafuu yake | 6 |
| Vua | mvua | 7 |
| Kaburiye | kaburi yake | 8 |
| Wakita | wakiita | 11 |

| | | |
|---|---|---|
| Kungia | kuingia | 17 |
| Adabuye | adabu yake | 17 |
| Dhatiyo | dhati yako | 21 |
| Nandeleza | naendeleza | 22 |
| Rehemaze | rehema zake | 23 |
| Mimbaye | mimba yake | 41 |
| Kiona | akiona | 42 |
| Swifazo | sifa zako | 52 |
| Sahibuye | sahibu yake | 86 |
| Nuruye | nuru yake | 86 |
| Mahabayo | mahaba yako | 101 |
| Yangumi | yangu mimi | 102 |
| Twalizozipata | tulizozipata | 112 |
| Atakosoma | atakaye soma | 121 |
| Ngwamusetiri | Mungu amstiri | 121 |
| Ilo | iliyo | 124 |
| Yamesazani | yamesaza nini | 128 |
| Kwaye | kwake yeye | 5 |

### 4.6.2 MAZIDA

Katika sura ya pili, tulieleza mazida kama uhuru wa kurefusha neno kwa ajili ya kupata urari wa mizani bila kupotosha maana asili. Mifano ya mazida katika kazi hii ni kama ifuatayo:

**Mifano ya mazida**

| **MAZIDA** | **KISWAHILI SANIFU** | **UBETI** |
|---|---|---|
| Hadhirina | hadhira | 16 |
| Niati | nia | 18 |
| Nabiina | nabii | 18 |
| Wakiiona | wakiona | 19 |
| Ihisani | hisani | 21 |
| Kuruania | Kur’an | 37 |
| Kuuona | kuona | 38 |

| | | |
|---|---|---|
| Kupiganikia | kupigania | 42 |
| Akamulindaye | akamlinde | 59 |
| Fedhati | fedha | 119 |
| Nuniya | nuni | 127 |
| Nabia | nabii | 61 |

### 4.6.3 TABDILA

Katika sura ya pili, tulieleza tabdila kama mbinu ambayo mtunzi hubadilisha tahajia za maneno bila kupunguza wala kuzidisha mizani kwa lengo la kupata vina. Mifano ya tabdila katika kazi hii ni kama ifuatayo:

**Mifano ya Tabdila**

| TABDILA | KISWAHILI SANIFU | UBETI |
|---|---|---|
| Kyenda | akenda | 7 |
| Kuwelea | kuelewa | 26 |
| Mwenyi | mwenye | 29 |
| Nasabu | nasaba | 30 |
| Harama | haramu | 33 |
| Kwokoka | kuokoka | 36 |
| Alishukuri | alishukuru | 57 |
| Nyawo | nyayo | 60 |
| Wakyandamana | wakiandamana | 70 |
| Kwandika | kuandika | 121 |

## 4.7 MUUNDO

Kulingana na Wamitila (2008), muundo aghalabu hurejelea umbo na mpatano, mshikamano na uhusiano wa visehemu tofauti vya kazi husika. Mpatano huu huweza kuunda kazi nzima. Wamutiso (2005), anasema muundo ni umbo la kitu kutokana na jinsi kilivyoundwa au kutengenezwa. Ni jumla ya vijisehemu mbalimbali vya kazi za kifasihi na jinsi vijisehemu hivi vinavyohusiana na kuunda kazi nzima. Kingei na Kemoli (2001), wanasema muundo hutumiwa kueleza sura ya nje na ya ndani ya utungo na pia ni sura ya utungo kama unavyoonekana au kusikika kutokana na midundo ya mapigo yake.

## 4.8 UMBO LA UTUNGO

*Maulidi ya Nuni* ni utungo wenye beti mia moja na thelathini. Kila ubeti una mishororo minne na vina vya mwisho vinafanana katika mistari mitatu ya kwanza kutoka ubeti wa kwanza hadi wa mwisho na mstari wa mwisho umebadilika kutoka ubeti wa kwanza hadi wa mwisho. Kila mshororo una mizani 15. Maelezo haya yanathibitishwa kama ifuatavyo:

Nilikufumie kwa upote wa unudhuma
nguo wa sanaa nakishiye hawakufuma
fikirani mbili ya hadhiki na njinga nyama
ulemeze durra utungowe pakalingana. (ubeti wa 1 )

Tupowe bahati na baraka na kulla yema
la ulimwenguni na ahera twende Na'ima
na tuyaombao Kiyamani tupowe mema
na mama na baba na hawani wapweke Janna (ubeti wa 130 )

Kazi hii imegawika katika sehemu tatu kuu ambazo ni: Utangulizi kuhusu mtunzi halikadhalika sharuti za maulidi haya pamoja na umuhimu wake (beti 19), kazi asilia iliyotungwa kwa Kiarabu na mtunzi ( beti 89 ), na mwisho wa utungo ( beti 22 ).

## 4.9 MANDHARI/MAHALI

Mandhari au mahali ni sehemu ambapo tukio hufanyika katika kazi yoyote ya fasihi kama tulivyoeleza katika sura ya pili. Katika kazi hii, mtunzi ametusimulia mandhari ya kijiografia ambapo ametupa habari kuhusu mazazi ya Mtume (S.A.W) ambayo yalitokea katika mji wa Makka. Vilevile tunapewa maelezo kuhusu Al Kaaba iliyoko Makka ambapo baada ya Mtume kuzaliwa, Babu yake alimpeleka sehemu hiyo na kumuombea ili asipate madhara yeyote. Sehemu hii ni muhimu kwa waumini wa Kiislam wanapokwenda Makka na kutekeleza nguzo ya mwisho ya Uislamu ambayo ni Hajj. Isitoshe, sehemu hii ni muhimu na takatifu kwa Waislamu kwa sababu wanapotekeleza nguzo ya swala hupaswa kuelekea kibla ambacho usuli wake ni Makka. Vilevile Makka ni sehemu tukufu na siku ya kiama watu wote watakusanywa katika sehemu hii tukufu ili walipwe kulingana na matendo yao. Vilevile tunapewa maelezo kuhusu safari ya Mtume (S.A.W) kutoka Makka hadi Jerusalaem.

Kuna mandhari yasiyo halisi yaliyojitokeza katika kazi hii, wakati Mtume (S.A.W) alipopaa kutoka uwingu wa kwanza hadi wa saba. Ajabu ni kuwa safari hii ilichukua usiku mmoja pekee na Mtume (S.A.W) alionyeshwa matukio mbalimbali yaliyokuwemo motoni na peponi na hatimaye kukabidhiwa nguzo ya pili ya Uislamu ambayo ni swala.

Kuna mandhari ya maeneo ya Uarabuni na hili linathibitishwa kwa kuweko kwa majabali na mitende. Mtunzi ametupa maelezo haya katika ubeti wa 51 na pia ubeti wa 98.

Vilevile tumepata mandhari ya kiishara ambapo tunapata maelezo kuhusu jinsi mahali panapofanywa maulidi panavyotakikana kuwe au masharti yake ambayo ni pamoja na kutengeneza mahali maalum, taa ziwashwe, pawe na vitu vitamutamu na marashi na udi visikosekane.

Kuna mandhari ya kimapatano ambayo yamejitokeza katika kazi hii wakati Abubakar alipokubali yote aliyokuja nayo Mtume Muhammad (S.A.W) na kuyafuata. Vilevile kitendo cha Muhajirun kuhama Madina pamoja na Mtume (S.A.W) kunaonyesha kumuunga na kumfuata Mtume (S.A.W). Hali kadhalika kitendo cha Ansar kuwapokea Muhajirun kunathibitisha mapatano ambayo yanachangia katika maenezi ya Uislamu. Maelezo haya yamejitokeza katika ubeti wa 86, 87 na 25.

Matukio mengi ambayo yamejitokeza katika kazi hii yameangaziwa katika mawanda mafupi kuliko inavyotarajiwa. Kwa mfano hakuna maelezo yanayojitokeza kuhusu ujana wa Mtume (S.A.W) na jinsi matukio yalivyokuwa hadi kupewa utume na Mola Mtukufu. Tunapewa taswira kwamba kukua kwake kulikuwa kwa maajabu ambapo baada ya miezi kadhaa alikuwa tayari kesha shika guu na hatimaye kuanza kuzungumza. ( ubeti wa 40 na 41).

## 4.10 HITIMISHO

Katika sura hii, tumeangazia matumizi ya lugha, tamathali za usemi, taswira muundo, uhuru wa kishairi na mandhari katika *Maulidi ya Nuni*. Tumeanza kwa kueleza vipengele vya fani na baadaye tukaangalia vipengele mbalimbali tulivyovishughulikia katika kazi hii ambavyo ni matumizi ya lugha, tamathali za usemi, muundo na mandhari au mahali. Katika matumizi ya lugha, tumeweza kuona kuwa kuna matumizi ya Kiamu, Kingozi, na maneno ya Kiarabu. Kwa upande wa tamathali za usemi tumepata matumizi ya takriri, tashbihi au tashbiha, istiari, uhuishaji au tashihisi, chuku na taswira au jazanda. Pia tumechanganua kipengele cha muundo kwa kuangalia umbo la utungo huu. Vilevile tumechunguza uhuru wa mshairi na kupata matumizi ya inkisari, mazida na tabdila. Tumechunguza kipengele cha mandhari na kupata mandhari ya kijiografia, mandhari yasiyo halisi, mandhari ya kiishara, na mandhari ya maeneo ya Uarabuni.

## SURA YA TANO

### 5.1 HITIMISHO

### 5.2 UTANGULIZI

Katika sehemu hii, tumeeleza hitimisho la kazi yetu kwa kutoa muhtasari wa yale tuliyoyatekeleza na kuibua kulingana na somo letu la utafiti ambalo ni fani katika *Maulidi ya Nun*i kwa kurejelea malengo na maswali yetu ya utafiti. Kazi hii tumeitekeleza kwa kutumia nadharia ya mtindo. Mwishowe tumetoa mapendekezo ya tafiti za baadaye.

### 5.3 MUHTASARI WA UTAFITI WETU

Katika utafiti wetu, tuliazimia kutekeleza malengo mawili ambayo ni; kuchunguza nafasi ya wahusika na uhusika katika *Maulidi ya Nuni* na la pili kuchanganua dhana za matumizi ya lugha, tamathali za usemi, taswira au jazanda, uhuru wa mtunzi, muundo na mandhari katika *Maulidi ya Nuni*.

Katika kuchunguza nafasi ya wahusika na uhusika katika *Maulidi ya Nuni* ambalo lilikuwa lengo letu la kwanza, tuligundua kuwa wahusika pamoja na uhusika wao wana umuhimu mkubwa na wametumiwa kwa ufanifu mkubwa katika kufanikisha utungo huu. Kuna aina mbalimbali ya wahusika waliojitokeza katika utungo huu ambao ni wahusika wa kawaida na wasio wa kawaida, wahusika wakuu, wahusika wasaidizi na pia wahusika wadogo na kupitia kwa nafasi zao, haswa jinsi wanavyosawiriwa na sifa zao, tumeona kuwa wametimiza dhima ya utungo huu. Mtunzi kwa kiwango kikubwa amewasawiri wahusika na uhusika wao kwa ubunifu mkubwa. Vilevile tumepata kuwa wahusika hawa pamoja na uhusika wao wamesawiriwa kwa uchache sana kiasi cha kuwa hatupati maelezo ya kina kuhusu kukua kwao. Kwa kuwa utungo huu uko katika mawanda ya dini ya Kiislamu, imekuwa vigumu kuingilia kwa kina kuhusu utendakazi wa baadhi ya wahusika na mambo wanayoyatekeleza hususan Mwenyezi Mungu ambaye alimchagua Mtume Muhammad (S.A.W) na kufanikisha safari yake ya mbinguni ambayo ilichukua usiku mmoja pekee.

Katika kuchunguza lengo letu la pili, tumeshughulikia matumizi ya lugha, tamathali za usemi, taswira au jazanda, uhuru wa mtunzi, muundo na mandhari katika *Maulidi ya Nuni.* Baadhi ya matumizi ya lugha tuliyochanganua ni: Kiamu, Kingozi na maneno ya Kiarabu na tumeona mifano mingi ya maneno ya lugha hizi na jinsi yalivyotumika katika kazi hii.

Tamathali za usemi tulizozishughulikia ni pamoja na takriri, tashbihi au tashbiha, istiari, uhuishaji au tashihisi, chuku na pia tumechunguza taswira au jazanda na tumeona jinsi mtunzi alivyozitumia katika kufanikisha kazi yake. Katika uhuru wa mtunzi, tumechunguza na kupata matumizi ya inkisari, mazida na tabdila na tumegundua mtunzi amefanikiwa kwa kiwango kikubwa kama tulivyoona. Katika muundo tumeshughulikia umbo na mtindo wa utungo huu. Tumemalizia na mandhari au mahali ambapo tumeweza kupata mandhari aina mbalimbali kama vile mandhari ya kijiografia, mandhari ya kiishara, mandhari ya kidini na mandhari yasiyohalisi. Utafiti wetu umeonyesha mchango mkubwa uliotekelezwa na mbinu hizi za kifani katika uwasilishaji wa maudhui kwa hadhira pamoja na kukuza na kuendeleza dhamira zake mbalimbali. Tumeweza kuyajibu maswali yetu ya utafiti kwa kuthibitisha kuwa wahusika na uhusika wana umuhimu mkubwa katika kufanikisha kazi hii kama tulivyoona na vilevile tumeona jinsi matumizi ya lugha, tamathali za usemi, taswira au jazanda, uhuru wa mtunzi, muundo na mandhari zimechangia kutimiza dhima ya kazi hii.

## 5.3 UFAAFU WA NADHARIA

Tumeweza kutumia nadharia ya mtindo katika kazi yetu ambayo ni fani katika *Maulidi ya Nuni* na imetufaa katika kuchanganua somo letu la utafiti. Vilevile imetusaidia kuchanganua vipengele vya fani hususan; wahusika na uhusika, matumizi ya lugha, tamathali za semi, muundo na mandhari au mahali.

## 5.4 MAPENDEKEZO

Katika utafiti wetu, tumeweza kushughulikia fani katika *maulidi ya Nuni*. Tunapendekeza kuwa watafiti wa baadaye washughulikie kipengele cha maudhui katika *Maulidi ya Nuni* ambacho hatukukigusa. Katika kazi yetu tumeweza kutumia nadharia ya mtindo na tunapendekeza watafiti wa baadaye watumie nadharia nyengine katika *Maulidi ya Nuni* ama tungo nyengine zozote.

# MAREJELEO


Allen, J. (1971). *Tendi*. Nairobi: Heinemann.

Aristotle (1965). *Poetics* katika S.T. Dorsch, Aristotle/Horace/ Longinus. Harmondsworth: Penguin.

Busiri, A.M (2006). *Qasidah Burdah*. India: Kutub Khana Ishayat-ul- Islam.

Bakari, M. (1982). *The Morphopphonology of the Kenyan Swahili Dialects.* Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa Chuo Kikuu cha Nairobi.

Crystal, D.& Davy.D.(1969). *Investigating English Style.* London: Longman Group.

Crystal, D. (1997). *Dictionary of Linguistics and Phonetics*. 4th edition Oxford: Blackwell.

Forster, E.M.(1927). *Aspects of the Novel*. London: Penguin Books.

Gill, R. (1985). *Mastering English Literature.* London: The Macmillan Press Ltd.

Harries, L. (1962). *Swahili Poetry*. Oxford: Claredon.

Iribemwangi, P.& Mukhwana, A. (2011). *Isimujamii*. Nairobi: Printpak.

Issa et al. (1981). *Misingi ya Nadharia ya Fasihi*. Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni Zanzibar: Tanzania.

Kandhalavi, Z.M. (1999). *Visa vya Maswahaba.* Mombasa. Adam Traders.

Kasilu, P.N. ( 2003 ). *Mwingiliano wa Fani na Maudhui katika Ushairi wa Kithaka wa Mberia.* Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi ambayo haijachapishwa.

Kimani, N. na Rocha C. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Kingei, K. na Kemoli J. (2001). *Taaluma ya Ushairi*. Nairobi: Futa Form Ltd.

Knappert, J. (1964). *Four Swahili Epics.* Leiden: Drukkerij, Luctor et Emergo.

Knappert, J, (1967). *Traditional Swahili Poetry.* An Investigation in to the concept of East African Islam as reflected in the utenzi Literature. Leiden: E.J Brill.

Knappert, J. (1971). *Swahili Islamic Poetry. Leiden:* E J. Brill.

Knappert, J. (1971). *Mi'raj and Maulid*. Leiden: E J. Brill.

Knappert, J. (1979). *Four Centuries of Swahili Verse.* London: Duke University Press.

Leech, G.N. (1969). A *Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman Group Ltd.

Leech, G.N. & Short M. (1981). *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to English Fictional Prose* 2nd Edition. Harlow: Longman Group Ltd.

Madumulla, J.S. (1991). *Uchambuzi wa Riwaya.* Dar es salaam University Press.

Massamba, P.(2002). *Historia ya Kiswahili* Nairobi: The Jommo Kenyatta Foundation.

Mbatiah, M.(2001). *Kamusi ya Fasihi* Nairobi: Standard Textbooks Group & publishing.

Mungai, P. ( 2005 ). *Ulinganishi wa Kifani wa Tenzi za Swifa ya Nguvumali na Mikidadi na Mayasa.* Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi ambayo haijachapishwa.

Mung'ania, B.G. (1985 ). *Maudhui Mbali Mbali katika Ushairi wa Mathias E. Mnyampala* ( Penda- Chako ). Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi ambayo haijachapishwa.

Mwilaria, R.  (2011). *Fani katika Utenzi wa Ayubu*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi ambayo haijachapishwa.

Nassir, A. (2002). *Maulidi si Bida si Haramu*. Mombasa: Bilal Muslim Mission of Kenya.

Nursi,S. (2004). *The Miracles of Muhammad*. Ankara: Sanayi Han A- Blok.

Ngara, E. (1982). *Stylistic Criticism & The African Novel.* London: Heinemann.

Njogu, K. na Chimerah R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Omar, S.M. (2012). *Uchambuzi wa Tamathali za Usemi pamoja na Mbinu Nyengine za Matumizi ya Lugha katika Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*. Tasnifu ya Uzamili Chuo kikuu cha Nairobi ambayo haijachapishwa.

Omwoyo, O. (1997 ). *Fani katika Ushairi wa Hassan Mwalimu Mbega: Uhakiki wa Upisho wa Malenga na Dafina ya Malenga.* Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi ambayo haijachapishwa.

Senkoro, E. (1982). *Fasihi.* Dar es salaam University Press.

Sheikh, A. (2006). *Islamic Religious Education book 1.* Nairobi: Jurrey Publishers.

TUKI (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es salaam: TUKI.

Quraishy, M. A. (2008). *Text book of Islam book 1.*Nairobi: The Islamic Foundation.

Vutagwa, F. (2013). *Sifa za Kiuhalisiajabu na Umuhimu wake katika Utenzi wa Mwana Fatuma*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi ambayo haijachapishwa.

Wa Mberia, K. (1989). "Fumo *Liyongo"* TUKI. Katika Mulika nambari ya 21 uk 25-43. Daresalaam.

Wa Mutiso, (1985). *Hurafa na Uyakinifu katika Utenzi wa Hamziyya.* Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi ambayo haijachapishwa.

Wa Mutiso, K. (1996). *Archetypal Motifs in Swahili Poetry*. Dar es Salaam.

Wa Mutiso,K. (2005). *Kasida ya Hamziyah.* Chuo Kikuu cha Nairobi ambayo haijachapishwa.

Wa Mutiso,K. (2005). *Utenzi wa Hamziyah.* Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili – Dares Salaam

Wamitila, K.W (2003). *Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publishers.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Wamitila, K.W.  (2008). *Kanzi ya Fasihi. Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide Muwa Publishers Limited

Wesa W. (2005). "*Uhakiki na Uchambuzi wa Kifani katika Utenzi wa Mwana Fatuma na Siri li Asirali".* Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi ambayo haijachapishwa.